

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **BUNGE LA TANZANIA**

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

#### **MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**(Kikao cha Thelathini na Sita - Tarehe 31 Julai, 2003)**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

##### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Taarifa ya Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha kuhusu shughuli zao Chuo kwa Mwaka 2001/2002 (*Report on the Activities of the Institute of Finance Management for the Year 2001/2002*).

##### **NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:**

Hotuba ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka 2003/2004.

##### **MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ (k.n.y. MHE. WILLIAM A. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ushirika na Masoko katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 349

##### **Usafiri kwa Madiwani**

##### **MHE ISMAIL J. R. IWVATTA (k.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA) aliuliza:-**

Kwa kuwa tatizo la usafiri kwa Waheshimiwa Madiwani ni la kweli na ni la msingi; na kwa kuwa imeshindikana kuwakopesha Waheshimiwa Madiwani pikipiki kutokana na uhaba wa fedha Serikalini; je, Serikali haioni kuwa ni muhimu kuwatatulia Madiwani tatizo la usafiri kwa kuwakopesha baiskeli ambazo bei yake ni kiasi cha Sh. 70,000/= na kisha kuwakata walau Sh. 3,000/= kwa mwezi kwa kipindi cha miaka miwili kutoka katika posho yao wanayolipwa kila mwezi isiyopungua Sh. 30,000/=?

##### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuliirifu Bunge lako Tukufu kwamba, hii ni mara ya nne mfululizo kwa Bunge lako kuulizia suala la mikopo kwa Waheshimiwa Madiwani na masuala mengine yanayohusiana na mafao yao. Hii inadhihirisha jinsi Waheshimiwa Wabunge, wanavyoguswa na tatizo hili. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali pia inaguswa na inatambua sasa juu ya kuwepo kwa tatizo hili la Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali haijaweka utaratibu wa kuwawezesha madiwani kupata mikopo, iwe ya baiskeli, magari, pikipiki na kadhalika kutatua shida ya usafiri. Kwa mujibu wa taratibu zilivyo sasa, Diwani anaweza tu kukopo chombo chochote cha usafiri ikiwemo baiskeli kwa maelewano binafsi na mkopeshaji. Lakini Halmashauri haikatazwi hata kidogo kutoa dhamana kwa maana ya kumhakikishia mkopeshaji kwamba, makato ya posho ya Diwani yatakatwa na Halmashauri na kuwasilishwa kwake na siyo kwa kutumia moja kwa moja fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Madiwani ni Wasimamizi Wakuu wa mapato ya Halmashauri na maendeleo yake, lakini vile vile hawana budi kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naendelea kuwaagiza tena Wakurugenzi wa Halmashauri, kufuata sheria na miongozo mbalimbali na kuelekeza mapato ya Halmashauri katika kuimarisha huduma za jamii na kutekeleza miradi ya maendeleo ili iwe chachu ya kuendeleza Halmashauri zetu. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hawa Madiwani kuna wengine wana uwezo wa kujinunulia vyombo hivi vya usafiri, sasa Serikali itakubali angalau kuwasamehe kodi za VAT kama inavyofanya kwa walimu na watumishi wengine wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge, ni mzuri na tayari katika ofisi yetu tulikwishaanza kulifanyia kazi, kwa maana ya kuona kama hilo Serikali inaweza ikalikubali. *(Makofi)*

Lakini la pili ambalo Mheshimiwa Waziri, analifanyia kazi vile vile ni kujaribu kuona uwezekano wa kuona kama posho zilivyo sasa zinaweza zikapandishwa angalau kidogo. *(Makofi)*

Na. 350

#### **Usafiri kwa Makatibu Tarafa**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y. MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imewapa Makatibu Tarafa usafiri wa pikipiki; na kwa kuwa Makatibu Tarafa wa Jimbo la Peramiho wameeleza kuwa hawapati mafuta ya kuendeshea pikipiki hizo; je, Serikali ina mpango wa kuwapa mafuta/petrol?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha wahi kueleza hapa Bungeni, naomba kurudia tena kuwa, pikipiki zilizotolewa kwa Makatibu Tarafa bado ni mali ya Serikali. Hivyo, bado Serikali kwa kupitia Makatibu Tawala wa Mikoa itaendelea kuzipatia mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, Serikali imeziagiza Ofisi ya Wakuu wa Mikoa nchini kutenga katika Bajeti zao kiasi cha fedha kwa ajili ya kuhudumia pikipiki za Makatibu Tarafa. Mkoa wa Ruvuma ni mmojawapo wa Mikoa iliyofanya hivyo na jumla ya Sh. 4,842,400/= zimetengwa kwa madhumni hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha taratibu za kuwakopesha Makatibu Tarafa pikipiki hizo na mara tu pikipiki hizo zitakapokopeshwa kwa Makatibu Tarafa, Serikali itatoa maelezo mengine kuhusu namna tutakavyopata huduma nyingine. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Tarafa nyingi zinatofautiana kwa ukubwa wa maeneo; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuhakikisha kwamba mafuta au gharama za kutengeneza pikipiki hizo ziwe zinatolewa kulingana na ukubwa wa Tarafa hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza nimesema wazi kabisa kwamba, ndiyo maana tuliagiza Mikoa itenge katika Bajeti zao viwango ambavyo wanaona vifaa kwa ajili ya kutoa mafuta na vile vile kuhudumia pikipiki hizo. Naamini watakuwa wamezingatia ukubwa wa Tarafa pengine na matatizo mengine yaliyomo katika Tarafa husika. *(Makofi)*

**MHE ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linasema Makatibu Tarafa hawapati hela za mafuta; na kwa kuwa tatizo kama hilo walikuwa wanalipata Wakuu wa Wilaya na Serikali hii hii badala ya kupitisha fedha hizo kupitia Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa imeamua kuzipeleka moja kwa moja; je, utaratibu kama huo hauwezi ukafanywa kwa Makatibu Tarafa ili wawe wanazipata moja kwa moja kupitia mishahara yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali muda wote ni kutafuta njia nyepesi na rahisi kuwezesha shughuli kuweza kuendeshwa vizuri. Kwa hiyo, uamuzi wa kupeleka fedha moja kwa moja kwa Ma-DC ulitokana na msingi huo. *RAC* anatajwa kwa kuwa ndiyo *Accounting Officer* na ndiye anayetakiwa kupanga mipango ya Bajeti. Lakini hilo ninalosema kama halijazingatiwa, basi tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 351

### **Vituo vya Watoto Yatima na Wasiojiweza**

**MHE. GWASSA A. SEBABI** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu kabla ya Uhuru kulikuwa na vituo vya kulelea watoto nchini japokuwa vilikuwa vichache ambavyo viliongezeka baada ya Uhuru; na kwa kuwa wakati wote huo mpaka miaka ya 1990 vituo vya yatima vilikuwa vikipata ruzuku toka Wizara ya Afya pamoja na zilizokuwa Hospitali za Mashirika ya Dini, misaada ambayo ilisitishwa kwa vituo hivyo; na kwa kuwa tangu miaka ya 1980 lilipojitokeza janga la Ukimwi vituo vya yatima vimeongezeka mno na watoto yatima wanazidi kuongezeka kila wakati kiasi kwamba hali hiyo huko vijijini sasa ni balaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kukabiliana na tatizo hilo zito linaloongezeka kwa kasi nchini na fedha kiasi gani zilizotengwa kwa vituo hivyo nchini kila mwaka tangu 1998 na ni vituo vingapi vilivyopata fedha kuviendesha na kiasi gani kwa kituo tangu mwaka 1998?

(b) Je, Vituo vya Shirika la Mtakatifu Bernadeta na Masista wa Thereza wa Calcuta katika Jimbo la Katoliki Rulenge Wilayani Ngara vinavyopokea watoto tangu wa siku moja, vinawatunza vilema wasio na jamaa, wakongwe wasiojiweza, shule ya awali, wanasomesha yatima shule ya Msingi Rulenge na wengine katika sekondari, vilisaidiwaje katika kipindi hicho?

(c) Je, kwa jumla vituo vingapi vya aina hiyo nchini kwa mgawanyo vinavyoendeshwa na Serikali, Mashirika yasiyo ya Serikali na watu binafsi?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali chini ya Wizara yangu ilikuwa na utaratibu wa kutoa ruzuku kwa wakala za hiari, Mashirika ya Dini na watu binafsi ambao hupokea na kutunza watoto yatima na wenye shida kwenye makao. Mpango huu ulisimama mwaka 1994 kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Mwaka wa fedha 2000/2001, Wizara yangu ilianza tena kutoa ruzuku kwa makao hayo kama ifuatavyo: Mwaka 2000/2001 tulitoa Sh. 1,500,000/= kwa vituo 15, mwaka 2001/2002 tulitoa Sh. 1,000,000/= kwa vituo 10.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, tumetoa ruzuku kwa vituo mbalimbali kama ifuatavyo: Oktoba hadi Desemba Sh. 7,00,000/= kwa vituo 5, Januari hadi Machi Sh. 1,925,000/= kwa vituo 15, Aprili hadi Juni Sh. 2,000,000/= kwa vituo 20. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2000/2001 hadi mwaka 2002/2003, Wizara yangu imetoa kiasi cha Sh. 7,125,000/= kwa vituo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa orodha ya vituo vyote vilivyopata ruzuku ni ndefu, naomba nimpatie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wengine watakaopenda kupata orodha hiyo baadaye.

(b) Mheshimiwa Spika, makao ya watoto yatima yanayoendeshwa na Mtakatifu Bernadeta na Masista wa Thereza wa Calcuta katika Jimbo la Katoliki Rulenge Wilayani Ngara ni kati ya Makao ambayo yamepewa ruzuku ya Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, yapo makao 55 Tanzania Bara ambayo yamesajiliwa na kutambuliwa na Serikali ambayo yanapokea na kutunza watoto yatima na wenye shida. Mgawanyo wa wamiliki wa Makao hayo uko kama ifuatavyo:-

- Makao yanayomilikiwa na Serikali ni kimoja kilichopo Kurasini.
- Makao yanayomilikiwa na Mashirika ya Dini ya Wakala za Hiari ni 52.
- Makao yanayomilikiwa na watu binafsi yapo Morogoro moja na Tanga moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa orodha ya vituo ni ndefu, naomba nimpatie Mheshimiwa Mbunge na wengine watakaotaka baadaye. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa pamoja na fedha inayoonekana kwamba imekuwa ikitolewa kulingana na hali halisi ilivyo nchini baada ya janga la Ukimwi mzigo huu sasa umekuwa ni mkubwa kwa vituo vinavyolea watoto yatima:-

(i) Serikali iko tayari kutenga fedha katika Bajeti yake ya kila mwaka mahsus kwa sababu ya kuendesha vituo hivyo ili hawa watoto wapate kuishi? *(Makofi)*

(ii) Kwa nini watoto hawa wasiweze kuondoka katika Wizara hii wakaingia katika nafasi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili hili neno watoto lionekane tofauti kiasi cha kutosha na tunapozungumzia Maendeleo ya Vijana na Michezo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, hata vituo hivyo vilivyopo ilikuwa ni kazi kuweza kuifuatilia fedha, ilibidi hapa katikati tusitishwe kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hivi sasa hali ya uchumi inaendelea kuwa nzuri na tutaendelea kuangalia ni vipi ambavyo tunaweza tukashirikiana zaidi au hata Serikali yenyewe kuendelea kufungua vituo vingine.

Pili, kuhusu watoto hawa wahamie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Serikali inayo utaratibu wa kuunda Wizara zake hapo itakapoonekana haja hiyo ipo, bila shaka hilo linaweza likatekelezeka. Lakini kwa hivi sasa watoto hawa wako chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na tunaamini tunafanya kazi ya ulezi vizuri sana kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Si kwamba tunafanya kazi kwa kujitenga, hapana, mara nyingi tunashauriana na tunakwenda pamoja. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. Kwa kuwa ni jana tu Mheshimiwa Jenista Mhagama, aliuliza swali linalohusiana na maendeleo ya makuzi ya akili ya mtoto; na kwa kuwa kila anayejanga hujali zaidi kutengeneza msingi imara na sisi tunasema tunataka kuimarisha elimu, kama Wizara inashughulikia watoto yatima tu, watoto wale wengine tunawajengeaje msingi; je, Wizara haiwezi kufuata mawaidha ya *psychologist*? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara yenyewe ina *psychologists* wake kwa hiyo, tunapotengeneza miongozo ya kulea watoto yatima na miongozo ya kulea watoto wanaokwenda katika *kindergarten* tunahakikisha kwamba, misingi ya kisaikolojia imezingatiwa. (*Makofi*)

Na. 352

#### **Leseni za Udrevu Daraja 'C'**

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliamua kudhibiti kwa karibu zaidi utoaji wa leseni za udrevu za madaraja mbalimbali hususan zile za Daraja 'C' hapa nchini:-

(a) Je, udhibiti huo wa karibu unaendelea kwa muda gani sasa na ni leseni ngapi zimetolewa kwa madrevu katika kipindi hicho na idadi hiyo ni dhidi ya maombi mangapi hususan ya zile za Daraja la 'C'?

(b) Je, ni ajali ngapi za barabarani zimesababishwa na madrevu wasio na leseni au wenye leseni bandia katika kipindi hicho?

(c) Je, kuna viwango gani baina ya zoezi la udhibiti wa utoaji wa leseni na kupanda au kushuka kwa matukio ya ajali barabarani, hususan yale ambayo huripotwiwa kusababishwa na madrevu wenye leseni halali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa umekuwepo udhibiti mkali wa utoaji wa leseni hasa za Daraja 'C' tangu mwaka 2000. Madrevu wa Daraja 'C' ndiyo wanaoruhusiwa kuendesha mabasi ya abiria hasa ya masafa marefu.

Kwa kuzingatia udhibiti huu, ni maombi machache sana ya leseni za Daraja C ambayo hivi sasa yanakubaliwa baada ya mchujo mkali kwa mfano, mwaka 2000 leseni za Daraja 'C' zilizotolewa ni 26 tu, kati ya maombi 5,781, mwaka 2001 leseni za Daraja 'C' zilizotolewa ni 34 kati ya maombi 6,935 na mwaka 2002 zilitolewa leseni za Daraja 'C' 42 kati ya maombi 9,804. Udhibiti huu unaendelea. Wanaokosa leseni za Daraja 'C' hupewa leseni za madaraja mengine ambazo hazihusiki na udreva wa mabasi ya abiria.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 jumla ya ajali 15,490 zilitokea katika mikoa yote Tanzania Bara zikilinganishwa na ajali 13,877 zilizotokea mwaka 2001. Katika ajali za mwaka 2002 ajali 859 zilisababishwa na madreva wasiokuwa na leseni na wengine leseni zao zilikuwa zimeisha muda wake na hii ikiwa ni sawa na asilimia 5.5 ya ajali zote zilizotokea katika kipindi hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupambana na ongezeko la ajali, moja ya mikakati iliyowekwa ni huu wa kudhibiti utoaji wa leseni hasa za Daraja 'C', pia kuanzishwa kwa kozi maalum za madreva wa magari ya abiria katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Katika jitihada hizo imejionyesha kuwa ongezeko la matukio ya ajali kubwa, yaani zile zinazosababisha vifo limeendelea kushuka. Takwimu za mwaka 2001 zinaonyesha kuwa jumla ya ajali kubwa, yaani zile zilizosababisha vifo zilikuwa ni 1,562 zilizotokea ikilinganishwa na ajali za vifo 1,441 zilizotokea mwaka 2000. Hili ni ongezeko la ajali za vifo 121 ambalo ni sawa na asilimia 8.4. Mwaka 2002 ajali mbaya zilizosababisha vifo zilikuwa 1,660 ikilinganisha na ajali kama hizo 1,562 zilizotokea mwaka 2001. Kulikuwa na ongezeko la ajali za vifo 98 sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Kwa hali hii kiwango cha udhibiti wa utoaji wa leseni na mpango wa mafunzo ya madreva umeonyesha kupunguza ongezeko la ajali kubwa kutoka asilimia 8.4 za mwaka 2001 hadi asilimia 6.3 mwaka 2001/2002. Jitihada zinaendelea kufanywa katika utoaji wa mafunzo ya madreva na kutoa leseni kwa uangalifu mkubwa ili kupunguza ongezeko la ajali hapa nchini. (*Makofi*)

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, takwimu alizotoa zinadhihirisha kwamba kuna tatizo kubwa katika zoezi zima la utoaji wa leseni hizi hasa hasa za Daraja 'C' kwa mfano, amesema mwaka 2000 watu 26 tu wamepata leseni, miongoni mwa *applications* zaidi ya 5,000, hivyo mwaka uliofuata wamepata leseni watu 34 kwa *applications* karibu 7,000, watu 42 mwaka 2002 kwa *applications* karibu 10,000:-

(i) Sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana kwamba kuna tatizo la msingi hapo kwa sababu haiwezekani ukawa na *applicants* wengi kiasi hiki halafu zikitolewa leseni kidogo kiasi hiki na bado ukaona ni kawaida; kama tatizo hilo lipo basi naomba anifahamishe analifahamuje yeye Mheshimiwa Naibu Waziri?

(ii) Kulingana na majibu ya msingi ya swali hili inaelekea katika mlolongo mzima wa utoaji wa leseni hizi la kwanza ningependa ifahamike kwamba, udreva ni kazi lakini pia ni biashara moja kubwa sana ambayo pia inahusisha usalama na ufanisi wa vitu vingi tunavyofanya kila siku. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria inawezekana kwenye *chain* ya kutoa leseni kuna mtu ni *stumbling block*. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anaweza kukubali kuangalia uwezekano wa kuhamisha kabisa madaraka ya kutoa hizi kutoka mikononi mwa *Traffic Police* na kupeleka kwenye *Agency*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika sehemu yake ya kwanza ya swali kwamba, liko tatizo kwa nini zinatoka leseni chache kiasi hicho, tatizo lililopo ni kupambana na ajali za barabarani na mchujo huu upo katika leseni za Daraja 'C', ambazo zinahusika na madreva wanaoendesha mabasi. Katika takwimu nilizozitua wale waliokosa wamepewa leseni zingine za kuendesha magari ya nyumbani. Zile ukishamaliza tu masomo katika Chuo na Polisi wakajaribu umefaulu zile zinatolewa bila matatizo. Ugomvi uko kwenye leseni za madreva wa mabasi, hapo nataka lieleweke hivyo. Kwa hiyo, leseni zinatolewa kwa urahisi kwa wale waliofaulu tu, wanaoendesha magari mengine mengine. Kwa mabasi ndipo kuna mkazo mkubwa kwa ajali ya kupunguza ajali. Hao wa leseni Daraja 'C' wamekuwa wachache kwa sababu kwanza tunatazama umri, Daraja 'C' mpaka uwe na umri zaidi ya miaka 21. Daraja 'C' tunatazama vile vile haya magari mengine madogo madogo ya leseni ndogo

umetumia kwa muda gani, isipungue miaka mitatu na uwe na rekodi nzuri na vile vile uende kwenye kozi. Sasa hivi kuna kozi katika Chuo cha Usafirishaji ukitaka kupata leseni ya kuendesha basi. (Makofi)

(b) Kwamba sasa utoaji wa leseni za udreva uhamie katika Wizara nyingine, kusema kweli ni uamuzi wa Serikali, kama Serikali inaona iko haja ya kutoa kazi hii kutoka mikononi mwa Polisi iende katika Idara nyingine ya Serikali, sisi tutakuwa hatuna ugomvi na hilo.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa kuna madreva wengi kwa kipindi kilichopita huko nyuma wamepata leseni za *Class 'C'*; na kwa kuwa kuna utaratibu wa *ku-renew* leseni zao kila baada ya miaka mitatu; je, Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti hizi leseni za zamani ambazo wamekwishapata watu pengine hawastahili? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna ambao walishapata leseni za Daraja 'C' zamani na hao wako katika mafungu mawili, wako wale wanaoendesha magari ya kawaida ya nyumbani na kadhalika, sasa hao muda wao ukifika tunatazama rekodi zao kama ana rekodi nzuri anaweza akapewa tena, kama ana rekodi mbaya ya uendesaji mbaya kwa sababu Idara ya Polisi sasa hivi wanatunza hizi kumbukumbu katika kompyuta, wale wenye rekodi mbaya wakati wa *ku-renew* wanaweza wasipewe, kwa hao wenye magari mengine mengine ya kawaida.

Wale madreva wa mabasi, hao tunaandaa utaratibu, narudia tena kwamba, utafika wakati ambapo wale ambao watakuwa hawajapitia chuoni, hawatapewa leseni na kama anayo atanyang'anywa. Kwa hiyo, napenda kutoa tena wito wale madreva wa mabasi ambao hawajaenda katika Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam, waende sasa. Inatolewa kozi maalum katika Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam ya madreva kama hawa. Wale wenye mabasi ambao matajiri wao wanajua hawajaenda katika chuo hiki tunatoa wito tena waende sasa, kwa sababu wakati utafika tutawanyang'anya leseni hizo wale ambao hawajapitia katika chuo. (Makofi)

Na. 353

#### **Sifa za Mkimbizi kuwa Raia**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo wakimbizi ambao wamekuwa wageni wakazi yaani hawarejei kwao na hawataka kuomba Uraia wa Tanzania mfano wa Ulyankulu na Mishama; na kwa kuwa Tanzania imeingia Mikataba ya Kimataifa ya kukaribisha wakimbizi; je, ni hatua gani zitamfanya mkimbizi wa namna hiyo akose sifa ya kuwa raia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkimbizi katika nchi yoyote duniani, ni raia wa nchi nyingine ambaye amekubalika kupata hifadhi katika nchi hiyo kama walivyo wageni wengine wowote walioingia na kuishi ugenini. Tofauti kubwa iliyopo baina yao ni sababu za kuwepo kwao katika nchi hiyo ikiwemo hapa kwetu Tanzania. Kisheria, mkimbizi hawezi kupata uraia wa nchi yetu mpaka atakapoamua kwa hiari yake kuomba na hatimaye akubaliwe kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995 na kanuni zake za mwaka 1997.

Mkimbizi asiyetaka kurejea kwao na pia hataki kuomba uraia wa Tanzania, ataendelea kuwa chini ya udhibiti wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998. Aidha, mkimbizi huyo atadhibitiwa pia na Sheria ya Uhamiaji Na.7 ya mwaka 1995 na kanuni zake za mwaka 1997 iwapo atakuwa nje ya Kambi au nje ya makazi maalum yaliyotengwa rasmi kama Makambi ya Ukimbizi kwa shughuli za aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni zetu hazimlazimishi mkimbizi au mgeni mwingine yeyote kuomba uraia, bali Serikali huainisha vigezo na taratibu mbalimbali zinazomwezesha mwombaji kuomba uraia wetu na akashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo mkimbizi asiyetaka kurejea kwao na hataki kuomba uraia wa Tanzania, ni wazi kuwa hataweza kupewa uraia wa Tanzania kwa sababu atakuwa hajatimiza kigezo cha kuomba uraia wa nchi yetu. Hivyo, ataendelea kuishi kwa kuhifadhiwa kama mkimbizi au Serikali inaweza kumvua hadhi ya ukimbizi na kumfukuza nchini iwapo atakuwa hana sababu za msingi za kuendelea kuishi hapa nchini kama mkimbizi. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, wakimbizi hawa ambao hawataki kurudi nyumbani kwao ndio hawa wameleta silaha, wamekuwa majambazi, kwa hiyo, nadhani wamekosa sifa ya kukaa Tanzania. Je, Serikali iko tayari kuwafukuza wakimbizi wote ambao wanaleta fujo za namna hii na kuhatarisha amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna wakimbizi ambao wamekaa Tanzania na ni watu wazuri tu, walitokea sehemu za Kaskazini mwa nchi hii, wapo wametulia kama Wamasai na Wajaluo, waliotokea Kusini wapo wametulia kama Wamakonde na Wangoni, haoni wakimbizi waliotoka Magharibi wajifunze tabia za wakimbizi hawa ambao wametokea kuwa Watanzania? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwafukuza wakimbizi wote, hilo haliwezekani kwa sababu ya Sheria za Kimataifa, ambazo sisi kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, tumetia saina katika Mikataba mbalimbali na katika Mikataba hiyo ambayo tumeshasaina inakataza hilo. Lakini katika mazingira fulani fulani, hilo linaweza likafanyika. Kwa mfano, wakimbizi wengi wamekimbia nchi zao kwa sababu ya mapigano, machafuko katika nchi zao. Sasa pale ambapo hali imetulia, wakimbizi wanatakiwa sasa warudi na ndio Sheria ya Kimataifa inavyosema. Kule ambapo hali imetulia, kwa mfano, Burundi hali haijatulia, hatuwezi kuwafukuza kwa sababu tunabanwa na Mkataba. Rwanda hali imetulia na mwaka 2002 tumewarudisha wakimbizi wa Rwanda karibu 28,000. Wapo wengine kiasi cha 1,312 ambao walikataa kurudi.

Tumechunguza sababu zao, tumekuta kati yao, 145 wanazo sababu za msingi. Wengine wameolewa hapa, wameoa na wanataka kuwa raia. Waziri amekubali. Kuna wengine Wanyarwanda 1,167 hawana sababu za msingi. Hawa tayari Wizara yetu imekataa, imeshawavua hadhi ya ukimbizi na sasa hivi wanafukuzwa warudi kwao kwa sababu hali imetulia. *(Makofi)*

La pili, kuhusu Wangoni, Wamakonde, Wamasai na Wajaluo kama Mheshimiwa Profesa Sarungi hapa kuwaita kwamba wote hawa ni wakimbizi warudi kwao, hili halikubaliki. Hawa ni Watanzania wenzetu na Mheshimiwa Selelii, awaombe radhi akina Profesa Sarungi, kwa kuwaita wakimbizi wakati ni Watanzania wenzetu. *(Kicheko/Makofi)*

Na.354

### **Mikopo kwa Wakulima Wadogo**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2002/2003, Waziri wa Fedha alitoa kauli yenye matumaini kwa wananchi kwamba mikopo kwa wakulima wadogo wadogo sasa ipo na inapatikana kupitia Mabenki yetu lakini utaratibu wake bado haeleweki:-

(a) Je, ni lini mpango huu utaanza?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa ufafanuzi zaidi kwa wananchi hasa wakulima wadogo wadogo ili wajiondoe kwenye lindi la umaskini unaowakabili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Thobias Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, nilieleza kwamba, kwa vile uchumi wa Tanzania unategemea sana Sekta ya Kilimo na kwa vile wananchi walio wengi huko Vijijini wanategemea Sekta hii, njia kuu ya kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na ambayo inaweza kusaidia kupunguza umaskini kwa haraka ni kuimarisha Sekta ya Kilimo na kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hiyo ya Bajeti ya 2002/2003, nilieleza wazi kwamba, Sekta ya Kilimo kwa miaka mingi ilikuwa haipatiwi fedha zinazolingana na umuhimu wake, kwanza, kwa sababu fedha hazitoshi, lakini pia kwa sababu uchambuzi wa kina wa kuainisha maeneo muhimu ya kupewa kipaumbele katika kilimo, ulikuwa bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kutokana na Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha na pia Hotuba za Mawaziri wa Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na ya Ushirika na Msoko, ambayo itasomwa leo, kuwa sasa hali ya fedha ni nzuri na mipango ipo ya kuinua kilimo kwa ujumla. Bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004, imeimarisha zaidi mkakati wa kuinua kilimo na kuwezesha wananchi kufanya biashara bila vikwazo, kwa kuruhusiwa kuuza mazao yao kwa taratibu rahisi na zilizo wazi na hivyo kuwapatia mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo toka Mabenki, Serikali imeshachukua hatua ya kuongeza mikopo kwa wakopaji wadogo wadogo. Bajeti ya mwaka 2003/2004 imetenga fedha kwa ajili ya kudhamini mikopo ya Sekta hiyo ya wenye shughuli ndogo ndogo za uzalishaji na kibiashara yaani, *Small and Micro Enterprises* kama nilivyoieleza katika hotuba yangu. Mfuko huu utasimamiwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*). Utaratibu na matumizi ya Mfuko huu yatatangazwa mapema iwezekanavyo. Wananchi wataelimishwa kuwa wanaotakiwa kuomba udhamini huo ni Benki zitakazojiunga na mpango huo hivyo, ni lazima mwombaji awe ameiridhisha Benki husika kuwa wanastahili kukopeshwa kibiashara ili wadhaminiwe na huo Mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wananchi wanahitaji kuhamasishwa ili wazalishe mali zaidi na wawe na utamaduni wa kuweka akiba katika Mabenki ili kujenga uhusiano wa kuweza kukopa. Pia ni muhimu kuwahamasisha wananchi kuanzisha Benki au Mifuko au Vyama vya Kuweka na Kukopa Vijijini na vile vile kujenga tabia ya kurudisha mikopo yote na kwa wakati unaostahili. Kwa njia hii wananchi watajiletea maendeleo yao wenyewe na hivyo kuimarisha shughuli na juhudi zao za kupambana na umaskini.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wetu hawa ni wakulima wadogo wadogo ambao kwa kawaida kipato chao ni duni sana na ikizingatiwa kuwa riba inayotozwa kwenye mikopo hii ni kubwa sana; je, Serikali inaweza kutazama upya huu utaratibu au punguzo la riba ili wakulima hawa wanufaike vizuri na mpango huu wa Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, wakulima wadogo wadogo kipato chao ni duni na kwamba wanahitaji kupewa mikopo yenye masharti nafuu ikiwa ni pamoja na riba ya chini pamoja na masharti mengine ya kurudisha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, riba ni tozo inayotolewa kwa ajili ya kuhudumia mikopo inavyotolewa. Kwa hiyo, Mabenki yanayotoa mikopo ni lazima yatoze riba kwa sababu ya *financial intermediation* yaani gharama za kutoa hiyo mikopo. Lakini suala la riba kama nilivyojibu swali hapa Bungeni kipindi hiki cha Bunge la Bajeti kwamba, Serikali inafanya mipango ya makusudi ambayo itawezesha riba kushuka, inayokopeshwa na Mabenki yetu. Lakini kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, nashawishi wananchi waweze kuanzisha Benki Vijijini na natoa pongezi kwa Wilaya ambazo zimeanzisha *Community Banks* kama Mufindi, Mwanga, Kilimanjaro na Dar es Salaam. *Community Bank* itasaidia sana kupunguza riba. Pia wakulima wa Vijijini waanzishe vyama vya kuweka na kukopa na pia Mifuko mbalimbali. Mifuko hii na Vyama hivi vya Kuweka na Kukopa vinatoza riba ya chini kuliko ambavyo Mabenki ya

kibiashara yanatoza. Nitumie nafasi hii pia kupongeza Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, yanayotoa mikopo ya masharti nafuu kwa wakulima wadogo Wadogo, mojawapo ni *Care Singh* na *CARITAS*.

Na.355

### **Utekelezaji wa Mradi wa TLPM**

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alipofanya ziara hapo tarehe 9 Oktoba, 2001 alitembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi wa *TLMP* hasa kwenye maeneo ya ujenzi/ukarabati wa Minada; na kwa kuwa alipokuwa akikagua ujenzi wa Mnada wa Itigi na Manyoni alijionea jinsi ambavyo ujenzi wa majengo haukidhi haja ya kuwakinga walengwa kwa jua na mvua na kwamba mbao zilizotumika hazitoshelezi kama inavyostahili; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri aliagiza kwamba kazi hiyo ifanyike kikamilifu; na kwa kuwa mpaka sasa mradi huo haujarekebisha; je, Serikali inasema nini juu ya kutokutekelezwa kwa agizo lake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Waziri, alitembelea Vituo vya Itigi na Manyoni katika kipindi hicho cha mwezi wa kumi 2001 na kutoa maagizo ya kukamilisha Vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa utekelezaji wa agizo hilo ulitokana na kucheleweshwa kwa fedha za utekelezaji wa kazi hiyo kutoka kwa Wahisani, yaani Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda kukutaarifu kwamba, fedha za utekelezaji huo zimekwishafika na tayari Wizara yangu kwa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Masoko ya Mifugo nchini, imeshajenga majukwaa ya vyuma ambapo tayari yamezekwa kwenye minada ya Itigi na Manyoni.

Majukwaa haya yanajumuisha paa na sehemu ya kukalia ambayo itakidhi mahitaji ya wanunuzi na wauzaji wa mifugo kwa kukaa na kuingwa na jua au mvua wanapokuwa mnadani. Majukwaa hayo yamekamilika na tayari yanatumiwa na wafanyiabiashara wakiwa mnadani.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Sasa ili kuondoa wasiwasi na kuhakikisha kwamba kweli hii kazi imefanyika kama ilivyotarajiwa; je, Mheshimiwa Naibu Waziri ama Waziri mwenyewe, anaweza akatafuta muda muafaka wa kuweza kuja kukagua hiyo kazi kuona kama imefanyika vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, muda muafaka tutautafuta na tutamwarifu Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kwenda kuangalia, sio Manyoni na Itigi tu, lakini na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge anayamiliki.

Na.356

### **Mradi wa Maji - Mji wa Mbinga**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashari ya Wilaya ya Mbinga ilikuwa na mpango wa kukamilisha Mradi wa Maji Mji wa Mbinga awamu kwa awamu kuanzia mwaka 1995 kwa kutegemea ushuru wa kahawa; na kwa kuwa kwa bahati mbaya sana ushuru wa Kahawa umeshuka kutokana na kushuka kwa uzalishaji na kuanguka kwa bei ya soko na hivyo kuchangia kupunguza mapato ya Halmashauri chanzo cha kushindwa kabisa kukamilisha mradi huu; na kwa kuwa mpaka sasa Halmashauri imetumia Shilingi milioni 115.2 kwa

kununua mabomba na sasa zinahitajika Shilingi bilioni 3.315 ili mradi uweze kukamilika; je, kutokana na hali hiyo Serikali isingefaa kwa sasa ikagharamia mradi huo kwa uwezo wake au kwa kushirikiana na Wafadhili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maji ya Mji wa Mbinga yanatoka kwenye chanzo cha Ndengu kiasi cha lita 864,000 kwa siku. Mahitaji ya maji ya Mji wa Mbinga ni lita 2,592,000 kwa siku. Chanzo hiki cha Ndengu ni cha siku nyingi na kimechakaa.

Kwanza, nachukua nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na wadau wengine wote waliochangia juhudi za kutaka kutatua tatizo la maji katika Mji huo. Pamoja na hali ngumu ya uchumi inayoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na wananchi wake baada ya kushuka kwa uzalishaji na bei ya kahawa, bado naiomba Halmashauri hiyo kuendelea na mpango wake wa kutekeleza mradi huo angalau kwa awamu.

Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi hizo kwa kutafuta fedha ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha Mji wa Mbinga na maeneo mengine hapa nchini unapata maji yanayotosheleza mahitaji yake. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mji wa Mbinga toka uanzishwe mwaka 1964 unakumbana na matatizo makubwa sana ya miundombinu na hasa ikiwemo maji na umeme na kila Wizara inayohusika na matatizo hayo hutoa sababu ya ukosefu wa fedha na hasa kwa Wilaya ya Mbinga tu; je, Mheshimiwa Waziri wa Maji, hawezi akaionea huruma Wilaya ya Mbinga angalau kutoa uwezo wa kutatua tatizo hili moja tu la maji ili wananchi wa Mbinga angalau wakawa na nafuu kidogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyoona chanzo kilichopo sasa hivi kilianzishwa kwa nia hiyo hiyo njema ya kutaka kuwasaidia wananchi wa Mji wa Mbinga tangu kilipoanzishwa. Lakini kukua kwa Mji huo ambapo ni karibu asilimia 4.8 kwa mwaka, kumesababisha chanzo hicho kutokutosheleza na pia matatizo ya kiuchumi ya hapo awali yalisababisha mradi huo kutokuwa katika matunzo na *upgrading* inayohitajika. Lakini naelewa matatizo wanayoyapata wananchi hao, ndiyo maana Serikali inajitahidi sio kwa Mbinga tu, pamoja na sehemu nyingine, ndio maana katika jitihada hizo hivi karibuni tumeingiza Wilaya ya Songea Vijijini ambayo ni jirani ya Wilaya hiyo katika Mradi wa Benki ya Dunia. Kwa hiyo, jitihada hizo hizo zitaendelea ili kuona kwamba, Wilaya zote zenye matatizo yanatatuliwa. *(Makofi)*

Na.357

**Mauaji ya Raia Wasio na Hatia - Palestina na DRC**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE aliluliza:-**

Kwa kuwa Tanzania ni kioo cha uungwana katika Afrika na inajulikana kote Duniani juu ya msimamo wake dhidi ya Ukoloni, Ubaguzi wa rangi na Ukandamizaji wa wanyonge popote duniani; na kwa kuwa historia inaonyesha kwamba Tanzania haikusita kuchukua hatua mbalimbali dhidi ya nchi yoyote Duniani inayomnyanyasa binadamu mnyonge kwa misingi ya rangi, dini, siasa na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini Serikali iko kimya juu ya mauaji makubwa na unyanyasaji usiokuwa wa kifani kwa wananchi wa Palestina unaofanywa na Majeshi ya Israeli?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya mauaji ya watu wengi wasio na hatia yoyote nchini *Congo-DRC* yanayofanywa na Majeshi ya Rwanda na Uganda na kwamba kuna haja gani ya kuendelea kushirikiana na nchi ambazo mikono yao imejaa damu ya mauaji ya Waafrika wenzetu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana na kwa masikitiko makubwa ya unyanyasaji na mauaji yanayoendelea kufanywa na Majeshi ya Israeli dhidi ya Wapalestina, ambayo yamesababisha vifo vya maelfu ya raia wasiokuwa na hatia pamoja na uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Tanzania mara kwa mara imekuwa ikitoa matamko hadharani na kwenye vikao husika kulaani mauaji hayo na vitendo vya kulipiziana kisasi, vinavyopelekea kuuawa kwa raia wasiokuwa na hatia kutoka pande zote mbili na badala yake kurejea kwenye meza ya mazungumzo kama njia pekee ya kuleta ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa msimamo wa Tanzania katika suala hili uko wazi kabisa. Nao ni wa kuunga mkono jitihada za Wapalestina za kudai haki ya kuwa na Taifa lao huru na lenye mipaka inayoeleweka na kutambulika. Katika kutimiza azma hiyo, Tanzania imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kutekelezwa kwa Maazimio mbalimbali ya Umoja wa Mataifa yanayoitaka Israeli kuondoka kwenye ardhi ya Wapalestina. Aidha, Tanzania inaunga mkono malengo ya Mkataba wa Amani wa Oslo wa mwaka 1993, yanayotaka pamoja na mambo mengine, kuundwa kwa Taifa Huru la Wapalestina, sambamba na Taifa Huru la Israeli.

Tanzania itaendelea kulaani vitendo vyovyote vinavyozuia kutimizwa kwa azma hiyo, kwani inamini kuwa mgogoro wa Waisrael na Wapalestina utamalizika pale ambapo litaanzishwa Taifa Huru la Wapalestina.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna matumaini ya kuelekea kwenye lengo hilo baada ya Mpango wa Kuleta Amani unaotambulika kwa jina la *Road Map* kati ya Wapalestina na Israel, uliotayarishwa na kutangazwa na Mataifa makubwa na kukubaliwa na pande zote mbili, ingawa Israel bado inaonesha kuwa na mashaka nao kwa maneno na vitendo, kwa kuendelea na mashambulizi ya kuwahi yaani *pre-emptive strikes* ambayo yanapofanywa, huchochea mashambulizi ya kulipiza kisasi kutoka kwa upande wa Wanamgambo wa Palestina.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaunga mkono Mpango huo wa *Road Map* na kuzisihi pande zote mbili kuutekeleza kikamilifu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa mgogoro wa Wapalestina na Israel, Tanzania imekuwa ikilaani vikali mauaji ya raia wasiokuwa na hatia, yanayofanywa na pande zinazopigana ndani ya *DRC* bila ya kujali yanafanywa na nani au kwa uungwaji mkono na nani. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania itaendelea kufanya hivyo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono utekelezaji wa makubaliano ya Mikataba ya kuleta amani na utulivu ndani ya *DRC*.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imefurahishwa kwa kuundwa kwa Serikali ya Mpito nchini *DRC* pamoja na kuwepo kwa hali ya utulivu na usalama Mjini Bunia, Mashariki ya Kongo. Aidha, Tanzania inalaani vitendo vya kutumia nguvu, hali mbaya ya usalama na mauaji ya raia wasiokuwa na hatia katika Jimbo la Kivu na Wilayani Ituri.

Tunatoa wito kwa Wanamgambo wa Kihema na Kilendu kuacha mapigano na kuheshimu Mikataba walivyotiliana saina mara mbili Mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kurudia wito alioutoa Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa Umoja wa Mataifa, wa kuongeza ukubwa wa Jeshi la kulinda amani na kupanua madaraka yake ili yawe madaraka ya kuleta amani pia, badala ya kulinda amani tu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la Nyongeza. Namshukuru vile vile Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali hili kabla ya kusoma Sera ya Mambo ya Nje tuliyogawiwa juzi. Sasa kwa kuwa Dira ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ni kukuza na kujenga mahusiano ya uchumi kwa maslahi ya nchi yetu; je, kuna sababu gani za msingi kwa Serikali ya Tanzania kutokufungua uhusiano wa Ubalozi na Israel ambayo huko nyuma tulikuwa tukifanya biashara nzuri sana na tulifaidika sana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Mambo ya Nje anatoa hotuba yake ya Bajeti hapa Bungeni juzi tu, alielezea umuhimu wa nchi yetu kukuza diplomasia hiyo ya kiuchumi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema na ndio kielelezo muhimu katika Sera Mpya ya Mambo ya Nje kama ilivyogawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, (baadhi ya vitabu vilivyogawiwa hapa).

Mheshimiwa Spika, juu ya kukuza au kuanzisha uhusiano na Israel, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alisema hapa kwamba, nchi yetu ina mahusiano ya kidiplomasia na nchi kama 150 ikiwemo Israel. Tuna uhusiano nao wa kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, suala la ufunguaji wa Ubalozi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyosema hapa, inategemea sana na uwezo wa kiuchumi wa nchi yetu wa kuweza kufungua Ubalozi katika nchi fulani na alitangaza hapa kwamba, hadi sasa tuna Balozi kama 28 na pia alitoka azma ya nchi yetu ya kuendelea kufungua taratibu, kulingana na uwezo wa kiuchumi na kulingana na maslahi yetu sehemu hadi sehemu. *(Makofi)*

Na.358

### **Kilimo cha Umwagiliaji Mikoani**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu iliunda Kikosi cha Askari wa Miavuli kwa lengo kuu la kuwahakikishia Watanzania kuwa na uhakika wa kuendelea kuishi maisha ya uhakika; na kwa kuwa uhai unatokana na uhakika wa chakula cha kutosha kwa wakati wote na kwa watu wote, ikizingatiwa kwamba kilimo cha Tanzania ni cha kubahatisha kwa vile kinategemea mvua ambayo haina uhakika wa kunyesha:-

(a) Je, ni Mikoa mingapi imeanzisha miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani?

(b) Je, nini uwiano wa uzalishaji wa mazao ya kilimo kati ya kilimo cha jadi cha kutegemea mvua na kilimo cha kisasa cha umwagiliaji maji hapa nchini?

(c) Je, ikitokea Tanzania ikakosa mvua kwa miaka miwili mfululizo hali ambayo siombe itokee, Serikali ina mikakati ipi ya kukabili hali hiyo kwa njia ya kujitegemea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kwanza kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kilimo cha aina zote hutegemea mvua kama njia ya kupata maji yanayotumiwa na mimea. Kama mvua zikikosekana kwa kipindi kirefu, vyanzo vya maji vitakauka au kuwa na upungufu wa maji ambao utafanya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani nacho kipungue au kishindikane kwa kukosa maji.

Pili, katika nchi nyingi duniani ukiondoa nchi zilizoko kwenye majangwa, sehemu kubwa ya kilimo hutegemea mvua na kilimo cha umwagiliaji hutumika kuongeza uhakika wa mazao na kuwezesha kilimo kuendelea wakati kunapokuwa hakuna mvua.

Tatu, kilimo cha umwagiliaji maji kimekuwepo duniani kwa miaka mingi tangu enzi za ustaarabu wa Masopotamia na Mapharaoh wa Misri. Usasa unaweza kuwepo kwenye mbinu zinazotumiwa, sio kwenye dhana yenyewe.

Baada ya maelezo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ngwatura, kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka 1995/1996 na 2002/2003, Mikoa 19 ya Tanzania Bara iliendeleza Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani kwa kuanzisha miradi mipya 93 yenye eneo la jumla ya hekta 29,673 na kukarabati skimu 12 za zamani zenye jumla ya hekta 3,936 zilizoharibika. Aidha, katika mwaka wa 2003/2004, ukiondoa Mkoa wa Dar es Salaam, Mikoa mingine yote itatekeleza miradi 65 ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani kwa kutumia fedha za Serikali, Wahisani mbalimbali, Mfuko wa Pamoja wa Msaada wa Chakula kati ya Tanzania na Japan, Halmashauri za Wilaya na vyanzo vingine vya fedha.

(b) Kati ya hekta milioni kumi zinazolimwa kila mwaka nchini, ni hekta 200,985 tu zinazomwagiliwa maji. Asilimia 98 ya mazao yanayolimwa yanategema mvua.

(c) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kama kutatokea ukame wa muda mrefu hata kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kitashindikana kwa sababu vyanzo vya maji ambavyo vinategemea kunyesha kwa mvua navyo vitaathirika. Pamoja na ukweli huo, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ya kupambana na ukame unaoweza kutokea:-

- Kama ambavyo tumeeleza hapa Bungeni mara nyingi, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia kwenye Shirika lake la Ushirikiano wa Kimatifa, *JICA*, inaandaa Mpango kamambe wa umwagiliaji maji mashambani.

- Kuanzia mwaka huu na kwa ushirikiano wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo tutajenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwenye Mikoa saba ya Tanzania Bara.

- Serikali inahimiza matumizi ya maji ya maziwa na mkazo mkubwa unawekwa katika kutumia maji ya Ziwa Victoria, mito na maji ya ardhini. Aidha, Serikali itaendelea kuwahimiza wananchi kulima mazao yanayostahimili mazingira yao kama muhogo, mtama, uwele, viazi vitamu na jamii ya maharage kwa maeneo ya ukame.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa wakulima wa Mbinga ni hodari sana katika kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili; na kwa kuwa wanatumia mifereji kumwagilia kahawa, vile vile maji haya yanatumika katika kumenyea kahawa; na kwa kuwa tatizo kubwa ni kukosekana kwa maji safi na salama; je, Waziri atakuwa tayari kutumia fedha za *STABEX* ili kuwaletea wakulima wa Mbinga maji safi na salama ili wapate bei nzuri ya kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli napenda kuwapongeza sana wakulima wa Mbinga kwa uhodari wao katika kilimo cha umwagiliaji maji. Vile vile kilimo cha ngoro ni maarufu nacho. Hongera sana.

Pamoja na hayo ningependa kusema kauli ya jana aliyotoa Mheshimiwa Waziri, ilisema wazi wazi kama fedha hizi za kuboresha shughuli za kilimo zitaanzia huko huko. Kwa hiyo, napenda kutoa wito

kwa Mheshimiwa Ngwatura, kushirikiana na Halmashauri yake ya Mbinga, kuingiza mipango hiyo, wakati ukiwa muafaka fedha zitatolewa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamemalizika. Kuna tangazo moja tu la kikao kwa leo, nayo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Kamati ikutane saa 5 asubuhi chumba namba 54 katika vyumba vya Kamati. Mwisho, wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Selelii, ametania kwamba, kuna makabila ambayo ni wakimbizi hapa Tanzania. Ni suala zito, ingekuwa ni mtu mmoja mmoja nafuu. Mheshimiwa Naibu Waziri, alimwambia aombe radhi, lakini hakufanya hivyo.

Nielekeze Mheshimiwa Spika, sijui nifanye nini? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mwanzoni hata mimi nilichukulia maneno ya Mheshimiwa Selelii kwamba, ni utani. Lakini Kanuni inakataza kutumia maneno ya kuudhi wengine. Sasa madhali kuna Mheshimiwa Kone ameuadhika, sasa nakuagiza Mheshimiwa Selelii, uombe radhi. (*Kicheko*)

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, akiangalia *Hansard*, mimi nimesema kwamba, Watanzania ambao walikuwa wakimbizi waliotoka Kaskazini kama Wajaluo na Wamasai na wengine waliotoka Kusini kama Wayao, Wamakonde na Wangoni, zamani. Historia inasema kweli walitoka kule. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Umemwudhi Mbunge mmojawapo, omba radhi, *Sergeant-At-Arms* jiandae kama anafanya ubishi. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Kwa kuwa nimemwudhi Mheshimiwa Kone, namwomba radhi. (*Kicheko/Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 Wizara ya Ushirika na Masoko

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, inayohusu Wizara ya Ushirika na Masoko na kwa kuzingatia Taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka 2003/2004. Pamoja na Hotuba hii, nawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Sekta ya Uzalishaji Mali katika kipindi cha 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, iliyojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 2 Juni, 2003 na kuyapitisha kwa kauli moja. Ushauri uliitolewa na Kamati utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Kamati imewahi kukutana na viongozi wa Wizara kupata maelezo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara na Mashirika ya umma yaliyoko chini yake. Aidha, tarehe 30 Mei, 2003 Kamati ilishiriki katika Warsha ya mashauriano juu ya Sera Mpya ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002, Maandalizi ya Sheria Mpya ya Vyama vya Ushirika na mfumo wa kutumia stakabadhi za mazao katika maghala kama dhamana ya mikopo kwa wakulima. Wizara ilifaidika sana na ushauri uliitolewa na Kamati katika Warsha hiyo na itauzingatia.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake za kusimamia na kuendeleza amani, utulivu

na uchumi wa nchi yetu. Chini ya uongozi wake madhubuti, Tanzania inahesabika katika kundi la nchi chache za kuigwa Barani Afrika, zenye sera safi na endelevu za kukuza uchumi, demokrasia na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wasemaji waliotangulia, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliohinda katika uchaguzi mdogo uliofanyika Mei, 2003 na michango yao ya kusisimua, ambayo Bunge lako Tukufu limekwisha shuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, kwa Hotuba yake nzuri ya Bajeti ambayo imefafanua masuala mengi ya Ushirika na Masoko. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, walionitangulia kwa Hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii. Napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya Ushirika na Masoko wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo na Chakula na Mawaziri wengine, walipowasilisha Hotuba zao, ikiwa ni pamoja na hali ya Ushirika na Masoko na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha, kufufua na kuendeleza ushirika na masoko nchini.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, Dakta Ladislaus Komba, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Profesa Suleiman Chambo, Mkuu wa Chuo cha Ushirika Moshi, Bwana Severine Mosha, Mkurugenzi Mkuu COASCO, Viongozi wa Bodi za Mazao na wadau wote wa Ushirika na Masoko, kwa ushirikiano na ushauri wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ushirika na Masoko tokea iundwe Novemba, 2000 imetimiza umri wa takriban miaka miwili na nusu. Dhumuni moja kubwa la kuundwa kwa Wizara hii ilikuwa ni kukeleza azma ya Serikali ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini. Hii ilitokana na ukweli kuwa pamoja na kutambua umuhimu wa ushirika kama njia mojawapo muhimu ya kuondoa umaskini, hali ya vyama vingi vya ushirika ilikuwa mbaya sana, iliyogubikwa na matatizo mengi sugu. Matatizo hayo sugu ni pamoja na ukosefu wa mitaji, uongozi mbovu, ubadhirifu, hujuma na wizi, muundo duni wa ushirika, kukosa uhai wa kiuchumi na elimu duni ya ushirika. Hali hiyo ilisababisha kwa kiasi kikubwa umma wa Watanzania kupoteza imani iliyokuwepo juu ya ushirika. Hayo ndiyo mazingira ambayo Wizara iliyakuta ilipoundwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kifupi, kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya ushirika, uongozi uliokabidhiwa kazi ya kuiongoza Wizara hii mpya na nyeti ilibidi utumie kila aina ya ujasiri, uzoefu na maarifa kupambana na matatizo sugu niliyoyataja. Licha ya ugumu wa kazi hiyo, tayari matunda ya juhudi hizo yameanza kuonekana kama nitakavyoelezea baadaye. Lakini kwa kifupi matokeo ya juhudi hizo ni kuwa imani iliyopotea kuhusu uwezo wa ushirika imeanza kurudi na zinaonekana juhudi za wazi za wananchi na wanachama wenyewe za kuanzisha upya ushirika pale ulipozorota au kuuimarisha pale ulipolegalega.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Vyama vya Ushirika wa aina mbalimbali imeongezeka kutoka vyama 4,862 vilivyokuwepo Mei, 2002 hadi kufikia vyama 4,903 Mei, 2003. Katika kipindi hiki, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Uvuvi imeongezeka kutoka, vyama 74 vilivyokuwepo Mei, 2002 hadi vyama 86 Mei, 2003 sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Hii inaonesha kuwa wananchi, hususan wazalishaji wadogo na wa kati, wameitikia wito wa kufufua na kuimarisha ushirika kwa kuanzisha Vyama vya Ushirika ili wapate mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies - SACCOS*), vimekuwa na mvuto mkubwa kwa wananchi sehemu mbalimbali. Idadi ya vyama hivi imeongezeka kutoka vyama 1,048 Mei, 2002 hadi kufikia vyama 1,236 (778 mijini na 458 vijijini) Mei, 2003. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 18. Aidha, idadi ya wanachama iliongezeka kutoka 149,890 Mei, 2002 hadi 157,774 Mei, 2003, sawa na ongezeko la asilimia 5. Hisa na amana za wanachama zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 18.8 Mei, 2002 na kufikia shilingi bilioni 20.9 Mei, 2003, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Ongezeko la vyama hivi ni ishara njema kwa maana ya kujenga mitaji imara



ndani ya Ushirika. Wananchi wameanzisha vyama hivi katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, utalii, elimu na biashara.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vimeanza kujizatiti kubadili mfumo wa uendeshaji ili viweze kutoa huduma za kifedha kwa wananchi ambao hawapati huduma hizo vijijini na mijini kulingana na mahitaji yao. Jitihada zilizofanywa ni pamoja na ujenzi wa Ofisi zenye kuvutia wateja, upatikanaji wa vitendea kazi na kuimarisha usalama wa fedha za wanachama. Hivi sasa Vyama vya Ushirika 50 katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Dodoma, Iringa na Dar es Salaam, vimebadilisha mfumo wa uendeshaji na kuboresha utoaji huduma. Vyama hivi ni sawa na asilimia nne ya *SACCOS* zilizopo nchini. Pia, kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali kama vile Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (*SCCULT*), Benki ya *CRDB* na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya *FISEDA* na *DID*, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vimeanza kuimarisha huduma zao pamoja na kutoa bidhaa mbalimbali za kifedha ili kukidhi mahitaji ya wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Vyama vya Ushirika bado haujakidhi mahitaji yote ya wanachama. Hata hivyo, wanachama kwa kushirikiana na Serikali, Asasi zisizo za Serikali na Asasi nyingine za maendeleo, wameendelea kutatua matatizo yanayokwamisha shughuli za Ushirika ili kuufanya uweze kuwahudumia vizuri zaidi. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wanachama ili waweze kuvitawala na kuviendesha vyama vyao kulingana na matakwa yao. Kutokana na elimu hiyo wanachama wameweza kuwaondoa Viongozi na Watendaji wabovu na kuwaweka wapya na waadilifu. Mifano mizuri ni *SHIRECU*, *KDCU*, *KCU*, *ACU* na *RUCU*. Mabadiliko haya ya Uongozi, pamoja na uimarishaji wa mitaji ya Vyama vya Ushirika, umeviwezesha Vyama Vikuu kadhaa na baadhi ya Vyama vya Msingi kutoa malipo ya pili na ya tatu, kwa wanachama kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Kwa mfano, *KCU* baada ya malipo ya awali ya shilingi 90 kwa kilo kwa Kahawa ya maganda, ililipa malipo ya pili ya shilingi 25 kwa kilo. Aidha, kwa kahawa hai (*Organic Coffee*), baada ya malipo ya awali ya shilingi 400 kwa kilo, wakulima walilipwa malipo ya pili ya shilingi 100 kwa kilo. Aidha, *KDCU* baada ya malipo ya awali ya shilingi 60 kwa kilo kwa kahawa ya robusta ilitoa malipo ya nyongeza ya shilingi 90 kwa kilo. Hali kadhalika *VUASU* na Vyama vya Msingi 31 katika Mkoa wa Kilimanjaro, vililipa malipo ya pili ya shilingi 150 kwa kilo baada ya malipo ya awali ya shilingi 450 kwa kilo. Wizara itaendelea kuhimiza utaratibu huu ili Vyama vingine vya Ushirika navyo vilipe malipo ya pili na ya tatu kila inapowezekana. Waliofaidika na nyongeza hizi zote ni wale tu waliouza kahawa yao kupitia kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameendelea kuunganisha nguvu zao kwa lengo la kuanzisha na kuimarisha vyama vitakavyowapatia huduma muhimu kama ilivyokuwa hapo awali. Matokeo yameanza kuonekana ambapo baadhi ya Vyama vya Ushirika, Mkoani Kagera (*KCU*) na Mtwara vimeanza kutoa huduma ya pembejeo kwa wanachama wao, baada ya huduma hiyo kusitishwa kwa muda mrefu. Katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa mitaji, Benki ya Ushirika ya Wakulima wa Mkoa wa Kagera ilianza kutoa mikopo kwa wananchi mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika Moshi kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika Ushirika. Wanaonufaika na elimu na mafunzo ya chuo ni pamoja na Maafisa Ushirika, Watendaji, Viongozi, Wanachama wa Vyama vya Ushirika na wadau wengine ndani na nje ya nchi. Elimu na mafunzo hayo hutolewa katika ngazi mbalimbali ambayo ni pamoja na kozi ya Cheti, Stashahada ya Juu na Stashahada ya Uzamili. Aidha, utafiti pamoja na ushauri juu ya maendeleo ya Ushirika na mafunzo hutolewa chuoni na kwa kupitia matawi yake 16 yaliyopo katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Mara.

Mheshimiwa Spika, msukumo wa mafunzo hivi sasa ni elimu ya ushirika shirikishi inayolenga kuwawezesha wanaushirika na jamii kuleta mabadiliko katika utendaji wa shughuli zao. Mafunzo hayo yatawezesha wanachama wa Vyama vya Ushirika kumiliki, kupanga na kusimamia vyama vyao ikiwa ni pamoja na kuweka uongozi unaofaa na kuondoa ule usiofaa inapobidi. Kwa upande wa huduma za ushauri na elimu kwa wanachama, chuo kwa kushirikiana na Wizara, kimeendelea kuwaandaa Maofisa Ushirika wa Halmashauri za Wilaya ili waweze kutoa huduma za maboresho ya Ushirika ili uongozwe na wanachama

wenyewe. Pia, kwa kupitia matawi ya chuo yaliyoko mikoani chuo kimeendelea kutoa elimu ya ushirika shirikishi kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika katika maeneo yaliyochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kukiongezea uwezo wake kitaaluma, Chuo vile vile kimejishughulisha na mipango ya kubadili hadhi ili kiwe Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Maandalizi ya zoezi hili linalohusisha pia Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Wizara ya Fedha na wadau wengine yamefikia katika hatua ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, hali ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika imeanza kuimarika baada ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kuendesha Programu Maalum ya kuondoa viporo vya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika. Idadi ya vyama visivyokaguliwa imepungua kutoka vyama 3,111 kati ya vyama 4,862 vilivyokuwepo mwezi Mei, 2002 hadi vyama 2,353 mwezi Mei, 2003. Kati ya Vyama vya Ushirika 4,903 vilivyopo, vyama 2,551 vimekaguliwa hesabu za mwaka 2001/2002, sawa na asilimia 52 ya vyama vilivyopo nchini ikilinganishwa na asilimia 36 ya vyama vilivyokaguliwa hesabu za mwaka 2000/2001 ilipofika mwezi Mei 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari mambo yafuatayo yanaeleza umuhimu wa ushirika nchini mwetu:-

(i) Vyama vya Ushirika ni asasi za kiuchumi na kijamii, zisizo za Kiserikali zilizokuwepo nchini Tanzania kwa miaka mingi kuliko asasi nyingine za kiuchumi na kijamii. Vyama vya Ushirika vimekuwepo nchini kwa miaka 72 hadi leo. Kwa kuwepo kwa miaka mingi hivi, Vyama vya Ushirika vimekuwa na uzoefu mkubwa wa kutatua matatizo ya kiuchumi, kisera, kisiasa na matatizo mengine ya kijamii.

(ii) Vyama vya Ushirika ndiyo asasi zilizosaidia kuleta uchumi wa fedha maeneo ya vijijini. Katika shughuli za ununuzi wa mazao, Vyama vya Ushirika vimeweza kuwafikishia wananchi wa kawaida fedha nyingi katika maeneo yao, hata yale ambayo hayafikiki kirahisi.

(iii) Kwenye upande wa asasi za fedha, mfumo wa Vyama vya Ushirika wa akiba na mikopo umedhihirisha kuwa ni endelevu na vinaweza kuanzishwa na wazalishaji na wafanya biashara wadogo wadogo na kutoa huduma za kibenki pale pale vilipo.

(iv) Ushirika ni chimbuko la uongozi wa kidemokrasia na Utawala Bora. Ushirika umejengwa kwenye misingi na kanuni ambazo zimekuwepo kwa miaka 159 hadi leo na kujaribiwa katika mifumo yote ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa mantiki hiyo, Viongozi wengi wa Tanzania walijifunza mbinu za Uongozi huo kupitia Ushirika, hususan katika nyanja za siasa na uchumi.

(v) Ingawa hivi sasa kuna wanachama takriban 600,000 kwenye Vyama vya Ushirika, huduma zake zinawagusa maskini wapatao milioni kumi. Kwa hiyo, tunapozungumzia Ushirika, tunazungumza namna ya kuwafanya Watanzania walio wengi kuondokana na umaskini.

(vi) Ushirika kama dhana ya kuunganisha nguvu za wanyonge ni mchakato wa kujenga nguvu za pamoja ili kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kama vyombo vya kuunganisha nguvu za wanachama, Vyama vya Ushirika vinaweza kudorora au kulegalega na hata kufa lakini moyo wa ushirika (*The Spirit of Cooperative Enterprise*) hautakufa.

Mheshimiwa Spika, kilio cha wananchi walio wengi kwa sasa ni ukosefu wa masoko mazuri na ya uhakika ya kile wanachozalisha. Hii inatokana na ukweli kuwa hadi sasa nchi yetu iliweka mkazo mkubwa zaidi katika kukuza uzalishaji bila kujali sana masoko ya kile tunachozalisha, hususan katika mazao yasiyo na biashara. Lakini mara kwa mara pale ziada inayozalishwa inapokosa soko matokeo yake ni kuwa mzalishaji anakuwa amepata hasara kwa vile gharama za uzalishaji hazawezi kufidiwa. Aidha, mzalishaji hukata tamaa kuzalisha katika misimu inayofuata.

Kwa kiasi kikubwa, sekta binafsi imekuwa ikishiriki katika shughuli za ununuzi na uuzaji wa mazao ndani na nje ya nchi. Vyama vya Ushirika vinavyojishughulisha na kununua na kuuza mazao vimekuwa vikiongezewa uwezo wa kufanya shughuli hizo ili kuweza kuhimili na kumudu mikiki mikiki ya uchumi wa soko huru. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa soko la ushindani katika mazao mengi yanayolimwa hapa nchini, ushindani uliopo hivi sasa haujaweza kuboresha maslahi ya wazalishaji wengi kutokana na ukweli kwamba, ushindani huo haujawa huru na wa haki. Moja ya matokeo ya kutokuwa na ushindani wa haki ni wafanyabiashara kutozingatia ubora na madaraja ya mazao wanayonunua kutoka kwa wakulima. Aidha, wakulima wamekuwa wakipatiwa bei ndogo kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, kiasi kikubwa cha mazao makuu yanayozalishwa nchini huuzwa yakiwa ghafi. Wazalishaji wa mazao haya hawana uwezo mkubwa wa kupatana bei katika soko. Hali hii inafanya bei ya mazao haya kuwa chini ikilinganishwa na bei ya mazao yaliyosindikwa. Kwa upande wa mazao yasiyo asilia, viwango vya chini vya ubora, kutozingatia madaraja na uzalishaji wa msimu wa mazao haya ni kati ya sababu zinazofanya wazalishaji wasiweze kupata bei nzuri hata kama kiasi kinachozalishwa ni kikubwa (mfano, machungwa na tangawizi). Hivyo, kwa hivi sasa ni muhimu sana kuendelea kuhamasisha uzalishaji unaozingatia mahitaji ya masoko ya mazao ikiwemo ubora, madaraja na upatikanaji wa uhakika. Aidha, sekta binafsi inahamasishwa kuwa na mipango ya kusindika mazao ili kuongeza thamani yake, kwa mfano, korosho, mbegu za mafuta, mihogo na kadhhalika.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003, hali ya masoko ya baadhi ya mazao ya biashara imekuwa ya kuridhisha kidogo kutokana na ongezeko dogo la bei katika soko la dunia. Hata hivyo, bei kwa mkulima zimeendelea kuathiriwa kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa masoko ya ndani. Uduni wa miundombinu na kuwepo kwa mlolongo wa gharama zisizo za lazima katika kutumia baadhi ya miundombinu ni sababu kubwa za kuwepo kwa gharama kubwa za uendeshaji wa masoko ya ndani na nje. Kwa mfano, ukiritimba na gharama kubwa za matumizi ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kupata fursa ya kuuza bidhaa katika Soko la Amerika kwa mujibu wa *African Growth and Opportunity Act (AGOA)*, Soko la Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Soko la Upendeleo kwa nchi maskini nchini Japan, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo za Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Pamoja na kuwepo kwa fursa hizi, nchi yetu bado haijatumia kikamilifu fursa hiyo kutokana na kukosa bidhaa zinazokidhi viwango vya ubora wa mahitaji ya masoko hayo. Tanzania ina nafasi kubwa ya kukuza soko la mazao ya kilimo katika masoko niliyoyataja endapo sekta binafsi zitawezeshwa kuzalisha na kuuza bidhaa zenye viwango vya ubora unaohitajika katika masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa mazao makuu ya biashara katika msimu wa 2002/2003, ulifanyika bila matatizo makubwa isipokuwa ununuzi wa zao la pareto ambao ulikumbwa na tatizo kubwa la ukosefu wa soko. Kati ya tani 3,000 za pareto iliyozalishwa msimu wa 2002/2003, ni tani 1,100 tu ambazo zilinunuliwa. Aidha, uzalishaji wa sumu kali ya pareto (*Crude Extract*) msimu wa 2002/2003, ulikuwa kilo 37,420 ikilinganishwa na kilo 53,459 msimu wa 2001/2002. Mauzo ya sumu hiyo ilipungua kutoka kilo 30,705 msimu wa 2001/2002 na kufikia kilo 14,819 katika msimu wa 2002/2003 ikiwa ni anguko la asilimia 51.73. Katika kukabiliana na tatizo la soko la pareto, Serikali imetoa dhamana kwa Benki ya *CRDB* ili iweze kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.48 kwa Vyama vya Ushirika vitakavyonunua maua ya pareto yaliyopo kwa wakulima na pareto ya msimu wa 2003/2004. Zoezi la kutathmini uwezo wa Vyama vya Ushirika katika kununua zao hilo umefanywa na kubaini kuwa Vyama vya Ushirika vya msingi 16 vinavyoweza kupatiwa mikopo katika msimu huu. Vyama hivyo vipo katika Wilaya za Mbeya Vijijini (2), Makete (9), Njombe (1), Ludewa (2) na Mafinga (2). Utaratibu wa kuviwezesha vyama hivyo kupata mikopo toka Benki ya *CRDB* umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yaliyojitokeza kwa zao la pareto, kumekuwa na ongezeko la ununuzi kwa mazao ya kahawa, pamba mbegu, korosho, chai, tumbaku ya moshi na mkonge. Ununuzi wa zao la kahawa uliongezeka kutoka tani 37,000 msimu wa 2001/2002 na kufikia tani 49,427 msimu wa 2002/2003 ikiwa ni ongezeko la asilimia 33.6. Katika kipindi hicho, ununuzi wa pamba mbegu uliongezeka kutoka tani 148,142 na kufikia tani 188,690 ikiwa ni ongezeko la asilimia 27, korosho kutoka tani 67, 369 hadi tani 90,000 sawa na ongezeko la asilimia 33.6, chai kutoka tani 24,732 hadi tani 28,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.3 na tumbaku ya moshi kutoka tani 1,799 hadi tani 4,812 ikiwa ni ongezeko la

asilimia 167.5. Ununuzi wa zao la mkonge uliongezeka kidogo kutoka tani 23,502 na kufikia tani 23,641 ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.06. Aidha, ununuzi wa tumbaku ya mvuke ulipungua kutoka tani 25,901 zilizonunuliwa msimu wa 2001/2002 na kufikia tani 23,134 sawa na anguko la asilimia 10.7. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003 wastani wa bei ya mkulima kwa mazao ya korosho, pamba, kahawa na tumbaku ya mvuke na moshi iliongezeka kwa viwango tofauti. Bei ya kahawa aina ya robusta iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 40 kwa kilo msimu wa 2001/2002 na kufikia wastani wa shilingi 135 kwa kilo ikiwa ni ongezeko la asilimia 237.5. Katika kipindi hicho hicho, bei ya kahawa aina ya arabica katika Mkoa wa Kilimanjaro iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 500 kwa kilo hadi kufikia shilingi 733 kwa kilo, sawa na ongezeko la asilimia 46.6. Aidha, katika kipindi hicho, wastani wa bei ya korosho ghafi kwa kilo iliongezeka kutoka shilingi 300 hadi shilingi 360 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20. Wastani wa bei ya pamba mbegu iliongezeka kutoka shilingi 175 hadi shilingi 180 sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Bei ya tumbaku ya mvuke iliongezeka kutoka wastani wa shilingi 543 hadi shilingi 570 sawa na ongezeko la asilimia 4.9 na tumbaku ya moshi kutoka wastani wa shilingi 518 hadi shilingi 550 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6. Bei ya mkulima kwa zao la chai haikubadilika na iliendelea kubakia wastani wa shilingi 80 kwa kilo. Wastani wa bei ya kahawa aina ya arabica iliyozalishwa katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya na Iringa iliendelea kubakia kuwa shilingi 300 kwa kilo wakati ile inayo zalishwa katika Mkoa wa Arusha iliendelea kubaki na wastani wa shilingi 500 kwa kilo katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bei kwa mazao ya korosho, kahawa ya robusta na tumbaku ya mvuke lilitokana na kuimarika kwa bei ya mazao hayo katika Soko la Dunia. Wastani wa bei ya kuuzia nje korosho ghafi iliongezeka kutoka wastani wa dola za Marekani 0.54 msimu wa 2001/2002 na kufikia wastani wa dola za Marekani 0.58 kwa kilo msimu wa 2002/2003. Wastani wa bei ya kuuzia nje kahawa aina ya *mild arabica* iliongezeka kutoka dola za Marekani 0.98 msimu wa 2001/2002 na kufikia dola za Marekani 1.11 kwa kilo katika msimu wa 2002/2003 sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Katika kipindi hicho, bei ya kahawa aina ya *robusta* iliongezeka kutoka wastani wa dola za Marekani 0.33 na kufikia wastani wa dola za Marekani 0.52 kwa kilo. Wastani wa bei ya tumbaku ya mvuke iliongezeka kutoka dola za Marekani 1.40 na kufikia dola za Marekani 2.18 kwa kilo. Wastani wa bei ya kuuzia nje tumbaku ya moshi katika kipindi hicho ilishuka kutoka dola za Marekani 1.86 hadi dola za Marekani 1.78 kwa kilo. Bei ya chai katika soko la dunia katika vipindi hivyo haikubadilika na iliendelea kubakia kuwa wastani wa dola za Marekani 1.22 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka yanakadiriwa kuwa wastani wa tani 340,000. Katika msimu wa 2002/2003, tani 190,120 za sukari zilizalishwa hapa nchini ikilinganishwa na tani 163,994 zilizo zalishwa msimu wa 2001/2002. Hadi kufikia Aprili, 2003, jumla ya tani 155,900 za sukari iliyo zalishwa na viwanda hapa nchini ilikuwa imeuzwa katika soko la ndani na nje. Mauzo ya sukari chini ya Mkataba wa *Everything But Arms (EBA)* katika Soko la Ulaya msimu wa 2002/2003 yalikuwa tani 22,700 na kuliingizia Taifa pato la dola za Marekani milioni 12.2 ikilinganishwa na tani 22,150 za sukari zilizo uzwa msimu wa 2001/2002 chini ya utaratibu wa *ACP/EU Sugar Protocol*.

Mheshimiwa Spika, ununuzi na uuzaji wa mazao makuu ya chakula kama vile mahindi, mchele, ngano na maharage, ulifanyika bila matatizo makubwa ingawa biashara ya mazao haya iliendelea kukabiliwa na matatizo yatokanayo na hali duni ya barabara za vijijini, magulio au vituo vya kuuzia na kununulia na upungufu wa vinu au viwanda vidogo vya kusindika mazao haya. Hali hii husababisha gharama kubwa za kusafirisha mazao kutoka maeneo ya uzalishaji na pia kuwanyima wazalishaji na wafanyabiashara fursa ya kuhifadhi mazao hayo ili kuyauza wakati bei inapokuwa nzuri. Vile vile, wafanyabiashara wadogo wa mazao ya chakula wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa mitaji ya kufanyia biashara zao. Kwa sasa tatizo hili limepata ufumbuzi baada ya Serikali kuanzisha utaratibu wa kutoa dhamana kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia *Credit Agency for the Informal Sector*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu wa chakula katika nchi jirani za Malawi, Zambia, Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, katika msimu wa 2002/2003, wafanyabiashara, hususan wa zao la mahindi waliweza kupata soko katika nchi hizo. Wafanyabiashara hao walinunua mahindi kutoka Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Dodoma na kuyauza katika soko hilo kufuatia hatua

ya Serikali kuruhusu uuzaji wa mahindi katika nchi jirani. Takwimu kutokoa Idara ya Forodha zinaonyesha kuwa, mauzo ya mahindi kwenda nchi za *SADC* yaliongezeka kutoka tani 8,018 mwaka 2001 na kufikia tani 135,885 mwaka 2002. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 95 ya mauzo yote ya mahindi nchi za nje kwa mwaka 2002. Katika mwaka uliotangulia wa 2001, mauzo ya mahindi kwenda nchi za *SADC* yalikuwa ni asilimia 32 tu ya mauzo yote ya mahindi nje ya nchi. Mauzo ya mahindi kwenda nchi za *SADC* yalilingizia Taifa jumla ya dola za Marekani milioni 1.10 mwaka wa 2001 na dola za Marekani milioni 22.70 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, mazao ya mboga mboga, maua, matunda na viungo, wazalishaji wa mazao ya mboga mboga na matunda hutegemea kwa kiasi kikubwa soko la ndani kutokana na sehemu kubwa ya wazalishaji wa mazao hayo kutokidhi mahitaji ya Masoko ya Kimataifa. Wazalishaji wachache wa mboga mboga, maua na viungo, wamefanikiwa kupata soko katika nchi za Ulaya baada ya kuzalisha mazao yenye kukidhi mahitaji ya masoko hayo. Mfano wa wazalishaji hao ni Kampuni za *Gomba Estate Limited* na *Serengeti Fresh Limited* zilizoko Arusha ambazo huzalisha na kuuza mboga mboga nchini Uingereza na nchi nyingine za Ulaya, wazalishaji wa maua ni *Kiliflora Limited*, *Tengeru Flowers Limited* na *La Fleur d'Afrique Limited*, wazalishaji wa viungo ni *Tanzania Zanzibar Organic Producers (TAZOP)* na *Zanzibar Organic Producers (ZANOP)*. Makampuni haya yameiwezesha Tanzania kupata jumla ya nishani nne za dhahabu, moja ya fedha na mbili za shaba katika maonesho ya mboga mboga, maua, matunda na viungo yanayoendelea hivi sasa Mjini Rostock, Ujerumani. Napenda kuchukua fursa hii kuyapongeza kwa dhati makampuni haya. Vile vile napenda kuyashukuru maduka makubwa kama *SHOPRITE* na baadhi ya Hoteli za Kitalii, ambao wameendelea kununua na kuuza matunda, mboga mboga na bidhaa za mifugo zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kueleza katika Hotuba yangu nilipowasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2002/2003, Sekta ya Mifugo na mazao yake bado inategemewa kwa kiasi kikubwa soko la ndani kutokana na mifugo yetu pamoja na mazao yake kutokidhi viwango vya Kimataifa. Aidha, kuwepo kwa magonjwa ya mifugo katika ukanda wetu kunazuia usafirishaji na uuzaji wa mifugo na bidhaa zake katika Masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku, kwa ajili ya soko la ndani uliongezeka kwa asilimia 2.6 ikilinganishwa na msimu wa 2001/2002. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya soko la ndani uliongezeka kutoka lita milioni 900 na kufikia lita milioni 980. Aidha, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai milioni 650 na kufikia milioni 790 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21.5.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo msimu wa 2002/2003, uliongezeka kwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na idadi ya ngozi zilizokusanywa msimu wa 2001/2002. Mauzo ya ngozi nje ya nchi katika kipindi hicho yaliongezeka kwa asilimia 17. Mauzo haya yalilingizia Taifa kiasi cha shilingi bilioni 4.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.0 zilizopatikana msimu wa 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara yangu ilipanga kutekeleza majukumu yaliyolenga kuimarisha na kuendeleza huduma muhimu za ushirika na masoko kwa lengo la kuiwezesha jamii kushiriki na kumiliki shughuli za kiuchumi kupitia nyanja za ushirika na masoko. Mafanikio ya utekelezaji yalipatikana katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, kwenye eneo la sera, sheria na mipango, Wizara ilifanya kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha zoezi la kutafsiri Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002 katika lugha ya Kiswahili. Nakala za sera zinasambazwa kwa wadau ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge;

(ii) Kwa kushirikiana na wadau wengine, Wizara imeandaa rasimu ya mkakati wa kutekeleza Sera ya Ushirika ya mwaka 2002. Rasimu inaboreshwa na utayarishaji utakamilika Novemba, 2003. Aidha, kwa kushirikiana na wadau, Wizara imeanza kutayarisha programu ya kurekebisha mfumo wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika nchini (*Cooperative Reform Programme*). Lengo la programu kuwa na Vyama

vya Ushirika endelevu na vyenye uhai wa kiuchumi vinavyokidhi mahitaji ya wanachama. Madhumuni makuu ya programu hii ni:-

- Kujasirisha wanachama kumiliki, kuviendesha vyama vyao na kudhibiti viongozi na watendaji.
- Kuwezesha Vyama vya Ushirika viendeshe katika misingi ya biashara na viweze kuhimili ushindani katika soko huru.
- Kuwa na Vyama vya Ushirika vinavyoendesha kwa ufanisi.
- Kuweka uhasiano na mgawanyo sahihi wa kazi kati ya Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika ambapo Vyama vya Msingi ni wanachama.

(iii) Wizara imekamilisha maandalizi ya awali ya kuandaa Sera ya Maendeleo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Development Policy*). Madhumuni ya Sera hii ni kutoa miongozo ya kusimamia shughuli za uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Rasimu ya Sera hiyo inatarajiwa kukamilika Desemba, 2003;

(iv) Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 yamekamilika na Serikali imepitisha Waraka wa Baraza la Mawaziri uliopendekeza kutunga Sheria Mpya ya Vyama vya Ushirika (*The Cooperative Societies Act 2003*) mwezi Mei, 2003. Muswada wa Sheria mpya umeandaliwa na utasomwa mara ya kwanza Bungeni katika Bunge hili la Bajeti la 2003 na kusomwa mara ya pili Bungeni mwezi Novemba, 2003. Kupitishwa kwa Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika ya 2003 kutaweka mhimili wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002. Sheria hii itakapitishwa na kipengele cha maadili ya uongozi (*Code of Conduct for Cooperative Management*) kuanza kutekelezwa, itawezesha vyama kuchagua na kuajiri viongozi na watendaji kazi waadilifu na kuondoa viongozi na watendaji wabovu. Hivyo, Sheria itatoa fursa kwa Vyama vya Ushirika kuongozwa na viongozi wenye uwezo na maadili yanayostahili ili viwezed kuimarika na kuwapatia wanachama huduma zitakazokidhi mahitaji yao;

(v) Ili kuwezesha wakulima wadogo na wafanyabiashara kupata mikopo kwa kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala (*Warehouse Receipt System*), kama dhamana, Wizara inaandaa utaratibu wa kisheria wa kutumia mfumo huo. Mfumo huu umeonyesha mafanikio katika maeneo uliofanyiwa majaribio na mradi wa kuendeleza na kuboresha biashara ya pamba na kahawa unaofadhiliwa na Mfuko Maalum wa Mazao (*Common Fund for Commodities*). Majaribio ya mfumo huu yamefanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma na Mbeya kwa zao la kahawa na Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Kagera kwa zao la pamba. Katika mikoa hii wakulima katika vikundi, Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu, wamepata mikopo kutoka Benki za CRDB, KCB na EXIM. Kwa upande wa zao la pamba, mikopo ilitolewa na Benki ya CRDB kwa Vyama Vikuu vya Ushirika vya SHIRECU, Nyanza na Biharamulo. Lengo ni kutumia mfumo huu kwa mazao yote; na

(vi) Kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula na Maji na Mifugo kukamilisha Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*), ikiwa ni pamoja na mwongozo wa kuandaa mipango ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya. Halmashauri zimetumia mwongozo huu katika kuandaa mipango shirikishi ya kilimo, mifugo na ushirika, ambayo baadhi ya mipango hii itanza kutekelezwa katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004. Uimarishaji wa baadhi ya Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), utafanywa kupitia mipango hiyo. Fedha za mipango hiyo zimetengwa chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika, katika masuala yanayohusu maendeleo ya Ushirika Wizara imefanya yafuatayo:-

(i) Wizara imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kujiunga pamoja na kuanzisha Vyama vya Ushirika kama njia bora ya kuondokana na umaskini. Katika kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo kwa mwaka wa 2002/2003, jumla ya SACCOS 188 zimeanzishwa na kufanya idadi ya SACCOS nchini kufikia 1,236. Idadi ya wanachama wa SACCOS iliongezeka kutoka 149,890 mwezi Mei 2002 na kufikia 157,774 mwezi Mei 2003. Jumla ya hisa ni

shilingi bilioni 8.8, Amana (*Deposits*) shilingi bilioni 12.1 na mikopo iliyotolewa kwa wanachama ni shilingi bilioni 19.3. Hii inaashiria kukua kwa uwezo wa wananchi katika kujipatia mitaji na mahitaji mengine kwa njia ya kujitegemea. La maana zaidi kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba pamoja na ufinyu wa kipato chao;

(ii) Katika kuratibu mchakato wa uundaji wa Benki ya Ushirika ya Taifa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, imeandaa Hadidu za Rejea za Mshauri Mwelekezi, atakayefanya upembuzi yakinifu wa kuanzisha Benki ya Ushirika Kitaifa kulingana na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991 (*Banking and Financial Institution Act - BFIA*);

(iii) Katika mwaka wa 2002/2003, Serikali ilitenga shilingi bilioni 6.5 chini ya utaratibu wa Mfuko wa Mauzo ya Mazao Nje (*ECGS*) kwa ajili ya kutoa dhamana kwa Benki za Biashara ili ziweze kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kununulia mazao. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa dhamana ya shilingi bilioni 4.7 kwa Benki ya *CRDB*, ambayo iliidhinisha mikopo ya shilingi bilioni 11.86 kwa Vyama vya Ushirika ambavyo vilikusanya na kuuza mazao ya pamba na kahawa. Vyama Vikuu vya Ushirika vya *MBOCU, KNCU, KDCU, ISAYULA, KCU, SHIRECU, NYANZA, ACU* na *BCU* na Vyama vya Msingi vya Maindindo, Mahenge, Luwaita, Kimuli na Pilikano vya Mkoa wa Ruvuma, viliweza kupata mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 8.87 kutoka Benki hiyo ikiwa ni sawa na asilimia 74.79 ya fedha zilizoidhinishwa. Vyama hivi vilikadiriwa kununua jumla ya tani 41,000 za kahawa na tani 42,500 za pamba mbegu. Hadi kufikia mwisho wa msimu wa 2002/2003, vyama hivi vilikuwa vimekusanya tani 41,000 za kahawa na tani 5,336 za pamba mbegu (marobota 9,979). Pia, Vyama hivi vimerejesha mikopo ya shilingi bilioni 8.5 sawa na asilimia 95.6 ya mikopo iliyotolewa na Benki ya *CRDB*. Aidha, Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (*Kilimanjaro Cooperative Bank*) ilitoa mikopo ya shilingi milioni 802.5 kwa *VUASU* Mkoani Kilimanjaro ambavyo viliweza kukusanya tani 1,674 za kahawa. Vyama hivyo vimerejesha shilingi milioni 736.8 sawa na asilimia 92 ya mikopo iliyotolewa. Kwa mwenendo huu ni wazi kuwa Vyama vya Ushirika hivi saa vinakopesheka;

(iv) Katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Ushirika katika Halmashauri za Wilaya, Wizara ilinunua na kusambaza jumla ya pikipiki nane kwa Maafisa Ushirika katika Wilaya za Arumeru, Songea Vijijini, Kyela, Dodoma Vijijini, Sengerema, Bariadi, Urambo na Mtwara Vijijini. Vile vile, Mkoa na Wilaya zilipelekwa shilingi 96,500,000 ili kuimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, utoaji wa taarifa, uhamasishaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika;

(v) Katika kuimarisha uhasibu na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Wizara imeboresha miongozi mbalimbali iliyopo hususan, miongozi ya Uhasibu (*Accounting Manuals*), Fedha (*Financial Regulations*), Utawala (*Staff Regulations and Schemes of Service*), uandaaji wa makisio na miongozi ya ukaguzi kwa ajili ya kutumika katika Vyama vya Ushirika. Aidha, rasimu ya mwongozo wa ukaguzi (*Audit Manual*) wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), umekwishakamilika na utawasilishwa katika Bodi ya Wakurugenzi kwa hatua zaidi;

(vi) Wizara kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na taasisi nyingine za dola, iliendelea kufuatilia kesi zinazohusu wizi na ubadhirifu wa mali za Vyama vya Ushirika ili kuhakikisha kuwa kesi hizo zinaamuliwa kwa haki na wakati. Ufuatiliaji uliohusisha mashtaka 218 ulifanyika katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mara, Mwanza, Kagera, Arusha na Kilimanjaro. Kati ya mashtaka 218 yaliyofuatiliwa, kesi 118 zimetolewa maamuzi na kuchukuliwa hatua. Kati ya kesi 118, kesi 24 watuhumiwa walifungwa au kutozwa faini. Kesi 100 zilizobaki ziko Mahakamani na nyingine ziko katika hatua ya upelelezi. Ili kuboresha hali hii katika Sheria Mpya ya Vyama vya Ushirika kutakuwa na kifungu kipya kitachowapa uwezo Maafisa Malum kuendesha kesi za Vyama vya Ushirika Mahakamani. Pia kipengele cha *surcharge* kilichokuwepo katika Sheria ya Ushirika ya mwaka 1991, kimefanyiwa marekebisho ili kupunguza urasimu katika utekelezaji wake. Aidha, katika Sheria Mpya kutakuwa na utaratibu utakaozingatia maadili ya uongozi na utendaji katika Vyama vya Ushirika (*Code of Conduct for Cooperative Management*), ambao utahusu Maafisa au Watendaji watakaosababisha hasara kutakiwa kufidia hasara hizo. Aidha, kwa kutumia elimu ya ushirika shirikishi, wanachama watajasirishwa ili waweze kuwachukulia hatua Viongozi na Watendaji wabovu;

(vii) Katika kutatua migogoro ndani ya Vyama vya Ushirika, Wizara imefanya uchunguzi katika Vyama vya Ushirika vya *KYECU, RUCU, CHUTCU, MICU, SAMCU, NCU, RIVACU, IFACU, SHIRECU*, Posta na Simu na *Apex* ya Tumbaku kwa vyama vyenye migogoro ya kawaida. Vile vile uchunguzi umefanyika kwenye vyama vyenye migogoro ya mashamba vya Nshara, Uduru Makoa, Machame, Wari, Foo, Nronga, Masama Mula, Shakyero, Nkwansira, Lemira Mroma, Marukeni, Kyuu Isuki na Loliondo. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwaondoa viongozi wasiofaa na kutoa ushauri kwa wanachama ili wachukue hatua zinazostahili; na

(viii) Ili kupunguza viporo vya ukaguzi (*Audit Backlog*) wa Vyama vya Ushirika, Wizara ilitoa shilingi milioni 368 kwa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), ambazo ziliwezesha shirika kununua magari matano, Kompyuta 10 na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuimarisha shughuli za ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Juhudi hizi zililiwezesha shirika kukagua jumla ya vyama 2,551 kati ya vyama 4,903 vilivyopo nchini. Pamoja na kushughulikia ukaguzi na ununuzi wa vitendea kazi vilivyotajwa, Shirika la *COASCO* limepitia Sheria yake ya mwaka 1982 na kupendekeza marekebnisho ili kuwezesha muundo wake na utekelezaji wa majukumu yake vikidhi mahitaji ya wakati. Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika vyombo vinavyohusika ili hatimaye Muswada wa Marekebisho ya Sheria uwasilishwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuendeleza sekta ya masoko na kuboresha biashara ya mazao, Wizara iliendelea na juhudi zifuatazo za kuwezesha upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na uanzishaji wa Kituo cha Kuendeleza Masoko (*Marketing Development Centre*). Wizara imechambua rasimu ya mradi iliyotayarishwa na mshauri mwelekezi na utaratibu wa kuanzisha kituo hicho unaendelea. Aidha, Wizara imefanya mawasiliano na Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*), ambalo limeonyesha nia ya kushirikiana na Wizara katika kuanzisha kituo hicho kwa lengo la kukifanya kuwa kiungo muhimu cha biashara chini ya mpango wa *AGOA* ambacho kitaunganishwa katika mtandao (*network*) wa vituo vikuu vya biashara (*Trade Hubs*) vya Nairobi, Kenya, Gaborone na Bostwana;

(ii) Katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za masoko kwa wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara, Wizara imeendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za mwenendo wa wastani wa bei ya jumla kwa mazao makuu ya chakula na mifugo katika mnada wa Pugu kupitia vyombo vya habari husuan magazeti na Redio. Taarifa hizi hutolewa kupitia *Radio Tanzania* mara tatu kwa wiki (Jumanne, Alhamisi na Jumamosi) saa 12.00 asubuhi. Aidha, wataalam wapatao 55 wanaohusika na ukusanyaji wa takwimu na taarifa za masoko ya mazao katika Wilaya na Miji mikuu ya mikoa walipatiwa mafunzo;

(iii) Ili kukabiliana na tatizo la kupungua kwa pato la mkulima kunakosababishwa na kushuka kwa bei ya mazao katika soko la dunia, Wizara ilifanya tafiti za kubaini gharama za kuuza na kununua mazao (*Marketing Costs*), kwa mazao ya pamba, kahawa, tumbaku, pareto, nyama ya ng'ombe na kuku. Lengo la tafiti hizo lilikuwa ni kutoa mapendekezo ya kuondoa au kupunguza gharama zisizokuwa za lazima na hivyo kumwongezea mkulima kipato. Wizara itatumia matokeo ya tafiti hizo kuvishauri Vyama vya Ushirika na wafanyabiashara, kupunguza gharama za uendeshaji kwa lengo la kumwongezea mkulima mapato;

(iv) Kuanzia msimu wa 2002/2003, Serikali imeweka msukumo wa pekee katika kukuza soko la mazao yasiyo ya asilia hususan, mboga mboga, matunda, maua na viungo, kwa kuhamasisha wazalishaji na wafanyabiashara wa mazao hayo kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa yanayofanyika katika Mji wa Rostock nchini Ujerumani kuanzia mwezi Aprili hadi Oktoba, 2003. Aidha, Wizara imeweza kuwaunganisha wakulima wadogo wadogo wa mboga mboga na matunda na wakulima na wafanyabiashara ambao tayari wanauza bidhaa hizo katika masoko ya Ulaya. Ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara, wadau katika sekta hii kutoka Tanzania na Ujerumani watakuwa na mkutano wa kibiashara mwezi Septemba, 2003 Mjini Rostock, Ujerumani. Katika juhudi nyingine za kukuza soko la mazao ya kilimo na mifugo ndani na nje ya nchi, Wizara ilihamasisha wazalishaji na wauzaji wa mazao ya kilimo kutangaza bidhaa zao kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa ya Nane Nane yaliyofanyika



Mjini Morogoro mwezi Agosti, 2002. Katika maonesho hayo, Wizara ilionesha sampuli za bidhaa zenye viwango mbalimbali zinazohitajika katika masoko ya ndani na nje;

(v) Ili kujipenyeza katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara ilishiriki kukamilisha maandalizi ya Sera na mkakati wa kilimo na maendeleo vijijini kwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Lengo la mkakati huo ni kuimarisha upatikanaji na uhakika wa chakula na kujenga misingi endelevu ya kilimo na hivyo kuboresha maisha ya wananchi wa Jumuiya. Rasimu ya Sera na mkakati huo imekamilika. Aidha, Wizara inashiriki katika maandalizi yanayoendelea ya Itifaki ya Biashara (*Trade Protocol*) yenye lengo la kuanzisha muungano wa ushuru wa Forodha kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(vi) Wizara ilishiriki katika vikao mbalimbali vya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), vilivyojadili makubaliano ya biashara. Makubaliano hayo yameanza kuzaa matunda ikiwa ni pamoja na kuwezesha wazalishaji wa zao la mahindi kupata soko katika nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo msimu wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kujiimarisha na hivyo kuweza kuhimili ushindani katika mazingira ya uchumi wa soko huru, Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Ushirika Moshi, imeendelea kutekeleza Programu ya Elimu Shirikishi kwa kutoa mafunzo ya *Training of Trainers*. Hadi kufikia Juni, 2003, jumla ya Maafisa Ushirika 190 wamepata mafunzo, kati ya hao 2 wa Wizara, 20 wa mikoani na 168 ni wa Wilaya. Aidha, Serikali imetoa udhamini kwa wanafunzi 83 kati ya 351 wanaosoma katika Chuo cha Ushirika Moshi katika mwaka 2002/2003. Kati ya hao wanafunzi 40 wanasomea stashahada ya juu mwaka wa kwanza, 23 stashahada ya juu mwaka wa pili, 10 stashahada ya juu mwaka wa tatu na 10 stashahada ya uzamili.

Vile vile watumishi wa Wizara wa kada mbalimbali walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuongeza ujuzi na kuleta ufanisi kazini. Hadi kufikia Juni, 2003 watumishi 19 wa Wizara wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi. Watumishi wengine watano wanaendelea na masomo ya muda mrefu ya shahada ya uzamili katika Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Dar es Salaam. Mtumishi mmoja yuko nchini China kwa masomo ya shahada ya uzamili katika biashara. Pia semina kuhusu namna ya kujikinga na ukimwi na kuishi kwa matumaini ziliendeshwa na Wizara ikishirikiana na watumishi wa Wizara ya Afya - Dodoma kwa watumishi wote. Pamoja na hayo Wizara kwa kushirikiana na Maafisa kutoka Tasisi ya Kuzuia Rushwa, waliendesha Semina kuhusu kuzuia rushwa sehemu za kazi kwa wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya watumishi mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

- Jumla ya watumishi 90 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo wakiwemo maafisa ushirika 86 na watumishi wengine 4.

- Watumishi 29 waliopendekezwa kuthibitishwa kazini wamethibitishwa na mamlaka husika.

- Kibali cha ajira kujaza nafasi 10 zilizo wazi kutoka Idara Kuu ya Utumishi kimepatikana. Utaratibu wa ajira unaendelea.

- Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) uliandaliwa na umezinduliwa Novemba, 2002.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza majukumu makuu ya msingi, Wizara vile vile imetekeleza majukumu mengine yafuatayo:-

- (i) Wizara imeendelea na maandalizi ya mpango wa kukibadilisha Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (*SUA*). Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mapendekezo hayo umeandaliwa kwa hatua zaidi;

(ii) Ili kuainisha thamani ya Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Manonga ili kuwawezesha wanachama kununua hisa zaidi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, walifanya uthamini wa kiwanda hicho Desemba, 2002. Mthaminihaji alibaini kuwa thamani ya kiwanda ni shilingi bilioni 2.884. Tarifa ya uthamini huo iliwasilishwa na kujadiliwa kwenye kikao cha Halmashauri ya Chama cha Ushirika cha Igembensabo, Kampuni ya Rajani na Uongozi wa Mkoa wa Tabora. Katika kikao hicho ilikubalika kwamba, kiwanda kiuzwe kwa shilingi bilioni 1.7. Uongozi wa Igembensabo unafanya jitihada za kuona kama kiwanda kinaweza kufanya kazi na hivyo kukinunua; na

(iii) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Wizara, Dodoma. Ukarabati wa majengo manne ya Ofisi umekamilika na ujenzi wa jengo litakalokuwa na Ofisi mpya za nyongeza, ukumbi wa maonyesho, mikutano na maktaba unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 kuhusu kuendeleza ushirikiano kati ya Wizara na Idara zisizo za Muungano, Wizara ya Ushirika ya Masoko ilifanya mikutano na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ifuatavyo:-

(i) Mkutano na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika kuhusu maendeleo ya Ushirika, ambapo masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu katika uandaaji wa sera na maendeleo ya Ushirika kwa ujumla. Vile vile mikutano hiyo imewezesha kufikia muafaka kati ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*TFC*) na Vyama Vikuu vya Ushirika vitano vya Zanzibar kuhusu utaratibu wa kugawa mali ya iliyokuwa Washirika; na

(ii) Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii Zanzibar, imehusishwa kikamilifu katika mikutano mbalimbali ya maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika Maonyesho ya Kimataifa ya Mboga Mboga, matunda, maua na viungo yanayofanyika katika Mji wa Rostock, Ujerumani kuanzia Aprili hadi Oktoba, 2003. Zanzibar ilishiriki mwezi Juni katika maonyesho ya viungo. Aidha, Waziri wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii Zanzibar, walishiriki katika maonyesho hayo Septemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara imesimamia na kushiriki katika utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa kuendeleza na kuboresha biashara ya pamba na kahawa (*Coffee and Cotton Marketing Development and Trade Promotion Project*) unaofadhiliwa na Mfuko Maalum wa Mazao (*CFC*), ambao ulitekeleza shughuli zifuatazo:-

- Kuimarisha mnada wa kahawa wa Moshi kwa kuanzisha matumizi ya *Electronic Auction Machine*. Lengo la kuanzisha matumizi ya mashine hii ni kuongeza ushindani katika ununuzi wa zao kwa kuondoa uwezekano wa wanunuzi kuunda magenge (*cartels*) ya kununua kahawa yao wenyewe wanapoipeleka mnadani. Tangu utaratibu wa kutumia *Electronic Auction Machine* uanze mwezi Oktoba, 2002 kumekuwapo na ushindani na uwazi zaidi katika ununuzi wa kahawa.

- Mradi umewezesha ununuzi wa mashine ya kisasa (*High Volume Instrument*) ya kudhibiti ubora wa pamba nyuzi.

- Kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za mazao kwenye maghala kutumika kama dhamana ya kupata mikopo, hususan kwa wakulima wadogo kama nilivyoeleza hapo awali.

(ii) Mradi wa kuendeleza masoko ya mazao katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa na utekelezaji wake unasimamiwa na mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzanika (MVIWATA). Kazi zifuatazo zimefanyika katika mwaka 2002/2003:-

- Uhamasishaji na mafunzo kwa walengwa (viongozi na wakulima) kuhusu mradi.

- Maeneo yatakayojengwa masoko yameainishwa na michoro imetayarishwa.

- Mkandarasi Mshauri (*Consulting Engineer*) wa kusimamia, kushauri na kujenga barabara na masoko amepatikana. Ujenzi wa masoko na barabara umeanza Julai, 2003.

- Mafunzo kwa Mameneja wa Masoko na wasaidizi wao yamefanyika katika Chuo cha Ushirika Moshi.

(iii) Programu ya kuendeleza Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing System Development Programme*), Programu hii inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ilizinduliwa mwezi Novemba, 2002. Lengo la programu ni kuwezesha wakulima wadogo wadogo kuongeza uzalishaji na kupanua wigo wa mazao. Aidha, programu hii inalenga kuongeza idadi ya wafanyabiashara wa ngazi ya kati ambao wataweza kufanya biashara na wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo vijijini. Programu hii ambayo inafadhiliwa na *IFAD, ADF (African Development Fund)* na Serikali ya Ireland, itagharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 37.92. Programu hii itatekezwa kwa kipindi cha miaka saba katika Wilaya 36 za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma.

Shughuli muhimu zitakazotekezwa chini ya programu hii ni pamoja na:-

- Kuwezesha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Policy*).

- Kujasirisha wazalishaji na kuwaunganisha na masoko (*Producer Empowerment and Market Linkages*).

- Kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wazalishaji na wafanya biashara wa mazao vijijini (*Financial Market Support Services*).

- Kuimarisha miundombinu ya masoko (*Rural Marketing Infrastructure*).

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula na Maji na Maendeleo ya Mifugo zimeandaa mapitio ya matumizi ya fedha za umma (*Public Expenditure Review*), kwa mwaka wa 2002/2003. Maelezo ya *PER* ni muhimu katika kutayarisha mwongozo wa Bajeti na kuandaa mpango wa muda wa kati wa matumizi ya Serikali (*Medium Term Expenditure Framework*), kwa mwaka wa 2003/2004 - 2005/2006. Aidha, Sheria Mpya ya Fedha na Ununuzi Na.3 ya mwaka 2001 inafuatwa katika kuimarisha udhibiti wa ununuzi wa vifaa vyote vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Ushirika na Masoko ilitengewa jumla ya shilingi 7,094,712,200 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 5,897,524,600 zilikuwa za matumizi ya kawaida (Mishahara na matumizi mengine) na shilingi 1,197,187,600 zilikuwa za matumizi ya maendeleo. Aidha, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara iliongezewa fedha jumla ya shilingi 367,014,478 kwa ajili ya mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara (shilingi 101,014,478), Maonyesho ya Kimataifa ya mboga mboga, maua, matunda na viungo yanayofanyika Mjini Rostock, Ujerumani (shilingi 250,000,000) na fedha za shughuli za kupambana na rushwa (shilingi 16,000,000). Hivyo, kufanya jumla ya fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa kwa Wizara kuwa shilingi 6,242,642,934.

Hadi tarehe 30 Juni, 2003 matumizi ya fedha yalikuwa kama ifuatavyo: Shilingi 6,055,701,765.32 fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 97 ya fedha zilizotolewa zilikuwa zimetumika na Shilingi 986,130,920 fedha za matumizi ya maendeleo, zote za kigeni, sawa na asilimia 82.4 ya fedha zilizotengwa zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea na juhudi za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika na Masoko kwa kuzingatia mabadiliko ya Sera za kijumla za uchumi pamoja na Sera ya Maendeleo ya Ushirika. Aidha, mpango wa kazi umezingatia mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha kuhusu utayarishaji wa mpango wa muda wa kati na mfumo wa matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 - 2005/2006 (*Medium Term Expenditure*

*Framework*) na muundo na majukumu ya Wizara ya Ushirika na Masoko. Kazi zitakazotekelezwa zimeainishwa chini ya maeneo yafuatayo:-

Katika mwaka wa 2003/2004, katika eneo la sera, sheria na mipango, Wizara itafanya kazi zifuatazo:-

- Kukamilisha maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002.

- Kuandaa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Marketing Policy*) na mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo.

- Kukamilisha Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 2003 (*The Cooperative Societies Act 2003*), pamoja na Kanuni na Taratibu za utekelezaji. Aidha, semina za kuwaelimisha wadau kuhusu sheria mpya zitaandaliwa.

- Kukamilisha Programu ya kurekebisha mfumo wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika nchini (*Cooperative Reform Programme*).

- Kukamilisha mpango wa kupandisha hadhi Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*Moshi University College of Cooperatives and Business Studies*).

- Kuendelea na maandalizi ya kisheria ya kutumia mfumo wa stakabadhi za mazao kwenye maghala (*Warehouse Receipt System*) kama dhamana ya kupata mikopo.

- Kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kukamilisha Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme*).

- Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya *COASCO* ya mwaka 1982 pamoja na kuendelea na hatua za kuimarisha shirika (*Capacity Building*) kwa kuliongezea wataalam wanaofaa na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini inafikiwa, Wizara inafanya mambo makuu yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuendelea na kuhamasisha wananchi kuunda Vyama vya Ushirika vya Msingi katika sekta mbalimbali na kuimarisha Vikundi/Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia mahitaji ya walengwa kama vile wakulima, wafugaji, wavuvi na vikundi vya wanawake na vijana vya uzalishaji mali.

- Kuendelea kuvikutanisha Vyama vya Ushirika na Benki za Biashara ili kuviwezesha kupata mikopo kwa ajili ya kununulia mazao ya wakulima kwa utaratibu wa dhamana ya mfuko wa mauzo ya mazao nje ya nchi (*Export Credit Guarantee Scheme*). Kama ambavyo Waziri wa Fedha katika Hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 alivyosema, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 13.1 kwa ajili ya Mfuko huo. Ili kuhakikisha kuwa Serikali haipati hasara, Wizara itaendelea kusimamia matumizi ya mikopo hiyo na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inarejeshwa kwa wakopeshaji.

- Kwa kushirikiana na wadau wa Ushirika, kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa (*National Cooperative Bank*).

- Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za dola kuendelea na kufuatilia kesi zinazohusu wizi na ubadhirifu wa mali za ushirika ili kuhakikisha zinaamuliwa kwa haki na kwa wakati. Aidha, kutokana na ongezeko la kasi la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), Wizara itaimarisha Kitengo cha Ukaguzi na Usimamizi wa Shughuli za *SACCOS* ili kudhibiti wizi unaoweza kujitokeza.

- Kwa kutumia Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Usimamizi (COASCO), kuendelea na utekelezaji wa Programu Maalum ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Lengo la programu hii ni kuondoa viporo vya ukaguzi na kuhakikisha kuwa ukaguzi wa vyama unafanywa kwa wakati. Katika mwaka wa 2003/2004, COASCO watakamilisha viporo vya ukaguzi wa hesabu za 2001/2002 za vyama 2,352 na kukamilisha asilimia 50 ya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2002/2003. Aidha, Shirika litaandaa taarifa ya uhai wa Vyama vya Ushirika kwa madhumuni ya kujua hali ya uhai wa Vyama vya Ushirika kiuchumi na kubaini vipi vinastahili kuimarishwa, kuunganishwa au kufutwa. Zoezi hili litatuwezesha kutekeleza programu ya kurekebisha mfumo wa Vyama vya Ushirika.

- Kuendelea kutoa miongozo ya uendeshaji ili kusaidia kuboresha utendaji wa Vyama vya Ushirika, hususan Vyama vya Ushirika vya Msingi.

- Kwa kutumia Chuo cha Ushirika Moshi, kuendelea utekelezaji wa programu ya elimu ya ushirika shirikishi kwa waraghibishi na wanaushirika. Elimu na mafunzo kwa wanaushirika yatatilia mkazo nyanja zifuatazo: Maudhui, kanuni na utawala wa Vyama vya Ushirika, stadi za biashara, uzalishaji na huduma bora, ujasirimali biashara, ujenzi wa asasi za kujiletea maendeleo na ujasirishi wa wanachama katika kudhibiti na kutekeleza misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea mfumo wa masoko na kuongeza ufanisi wake, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuimarisha na kuendelea mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao ili kuboresha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za masoko. Aidha, *directorate* ya wanunuzi wa mazao itaandaliwa.

- Kuendelea na juhudi za kuanzisha Kituo cha Kuendeleza Masoko (*Marketing Development Centre*).

- Kuendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa mbalimbali za masoko kwa walengwa. Lengo ni kuongeza wigo wa taarifa za mazao yanayotangazwa katika vyombo vya habari na pia kutoa matangazo hayo katika vyombo vingine vya habari kama vile Radio Binafsi na Vituo vya Televisheni.

- Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za masoko kwa lengo la kuainisha vyanzo vya matatizo mbalimbali ya masoko ya mazao na kutoa mapendekezo yanayoweza kuondoa matatizo hayo.

- Kuendelea kuhamasisha wazalishaji na wanunuzi wa mazao kutangaza bidhaa zao kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonyesho ya Kitaifa na Kimataifa.

- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuandaa mikakati ya kukuza soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi na kuwathibitisha kazini watumishi wanaostahili pamoja na kuajiri watumishi wapya ili kuziba nafasi zilizo wazi. Vile vile Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea mapambano dhidi ya rushwa, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi wake ili kuwawezesha kupiga vita vitendo vyote vya rushwa. Sambamba na vita hiyo, kampeni dhidi ya janga hatari la UKIMWI zitaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ifuatayo:-

(i) Mradi wa kuendelea na kuboresha biashara ya pamba na kahawa, unatekelezwa kwa fedha za msaadakatoka Mfuko Malum wa Mazao (*Common Fund for Commodities*), pamoja na fedha za hapa. Katika mwaka wa 2003/2004, kazi zifuatazo zitatekelezwa chini ya mradi huu:-

- Kukamilisha taratibu za kisheria za kuwezesha matumizi ya stakabadhi za mazao yaliyopo ghalani kama dhamana ya mikopo kutoka katika vyombo vya fedha kwa wakulima wadogo na wanunuzi wa mazao.

- Kuendelea na uhamasishaji na mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa stakabadhi za mazao yaliyopo ghalani kutumika kama dhamana ya mikopo.

- Kuendeleza juhudi za kuimarisha ubora wa mazao ya kahawa na pamba.

(ii) Mradi wa kuendeleza masoko ya mazao katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini unatekelezwa katika Wilaya za Kongwa na Morogoro Vijijini, kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Ufaransa na unaratibiwa na mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania. Katika mwaka wa 2003/2004, kazi zifuatazo zimepangwa kufanyika:-

- Kuanza ujenzi wa soko la mazao katika Mji Mdogo wa Kibaigwa na magulio ya mazao katika Vijiji vya Tandai, Tawa na Nyandira katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.

- Kuboresha barabara katika vijiji hivyo.

- Kujenga kituo cha mafunzo ya vikundi vya wakulima katika Mji Mdogo wa Kibaigwa, Vijiji vya Mgeta, Tawa na Kinole.

- Kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima na wafanya biashara juu ya utunzaji wa miundombinu itakayoendelezwa.

Uzoefu utakaopatikana kutokana na masoko haya, utaiwezesha Serikali kujenga Vituo vya Masoko (*Commodity Exchange Centres*) vya Kanda vitakavyotumika kama minada mikuu ya mazao.

(iii) Programu ya kuendeleza mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo. Wizara itaendelea kutekeleza programu hii ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ili kutathmini mwenendo wa matumizi ya fedha za Serikali, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula na Maji na Maendeleo ya Mifugo, kuandaa mapitio ya matumizi ya fedha za umma (*Public Expenditure Review*), kwa mwaka wa 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa mstari wa mbele katika juhudi za kufufua, kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini. Jitihada zake zimehamasisha wanachama wa Vyama vya Ushirika kuleta mageuzi katika vyama vyao na hivyo kurejesha imani kwa wananchi kwa ujumla kuhusu uwezo wa Ushirika katika vita dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara yangu katika juhudi za kuendeleza Ushirika na Masoko. Kwanza, napenda kuzishukuru nchi za Japan, Norway, Ufaransa, Uholanzi, Canada na Marekani. Vile vile, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zikiwemo Benki ya Dunia, *International Cooperative Alliance, ILO, ICO, IFAD, CFC, UNOPS, UNCTAD* na *ADB*. Pamoja na shukrani hizo napenda kuwaomba waendeleo kutusaidia kwani bado tunahitaji sana misaada yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Viongozi na Wanachama wote wa Vyama vya Ushirika nchini na vikundi vya uzalishaji na utoaji wa huduma mbalimbali kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya kwa pamoja katika kuimarisha na kuendeleza Ushirika ili kufanikisha malengo yao. Vile vile, tunawashukuru wadau wote wengine wanaoshughulika na biashara ya mazao ya kilimo na mifugo na bidhaa nyingine ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Shilingi 6,831,540,900.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 395,747,000.00 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya hizo shilingi 169,300,000.00 ni fedha za hapa nchini na shilingi 226,447,000.00 ni za kigeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ushirika na Masoko katika kipindi cha mwaka 2002/2003 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya mwaka 2002/2003 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 81(1) Toleo la 2003, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, ilikutana Mjini Dar es Salaam tarehe 2 Juni, 2003 kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko. Katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilizingatia maeneo muhimu yafuatayo:-

- (i) Dira, malengo na madhumuni ya Wizara.
- (ii) Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali kwa mwaka 2002/2003.
- (iii) Mapato na Matumizi ya fedha katika kipindi cha 2002/2003.
- (iv) Mafanikio na matatizo ya utekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2002/2003.
- (v) Kazi zilizopangwa kufanyika kwa kipindi cha mwaka 2003/2004.
- (vi) Maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Dira ya Wizara ya Ushirika na Masoko ni kuwa Mwezesaji wa Maendeleo ya Vyama vya Ushirika endelevu vinavyodhibitiwa na wanachama wake na mfumo wa soko wenye ufanisi. Aidha, kutunga Sera, Sheria na taratibu za usimamizi pamoja na kutoa huduma bora za Ushirika na Masoko kwa Vyama vya Ushirika, wazalishaji, wafanyabiashara wadogo wadogo na wengine ili kuwawezesha kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi kwa jitihada za mtu mmoja mmoja, vikundi au kupitia Vyama vyao vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pili, Kamati yangu iliridhika na Dira fasaha ya Wizara inayoendana na mazingira halisi ya uchumi na mfumo wa Ushirika unaohitajika ili kujibu mahitaji ya mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kamati ilielezwa kuwa majukumu ya Wizara ya Ushirika na Masoko ni pamoja na:-

- (i) Kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya Sekta ya Ushirika na Masoko nchini.

(ii) Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo pamoja na uundaji wa vyombo vya fedha vya wanachama wenyewe ili kuimarisha uwezo wa ndani wa mitaji ya Vyama vya Ushirika.

(iii) Kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali ili kupanua wigo wa Ushirika.

(iv) Kusaidia Vyama vya Ushirika kupata mitaji endelevu ikiwa ni pamoja na kusaidia kuvikutanisha vyombo vya fedha na inapobidi kuvidhamini kwa ajili ya kupata mikopo na kuviwezesha vyama kukidhi haja za wanachama wake.

(v) Kuimarisha utafiti, ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taarifa muhimu za Ushirika na Masoko.

(vi) Kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa na mazao ndani na nje ya Tanzania na katika nchi inazoshirikiana nazo katika Jumuiya ya Nchi za Afrika ya Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), ili kuimarisha masoko ya mazao.

(vii) Kuwezesha na kuhamasisha ukuaji wa masoko ya mazao na bidhaa ndani na nje ya nchi.

(viii) Kuandaa na kuratibu mafunzo ya Ushirika na Masoko kwa wataalam wa Wizara, Watendaji na Viongozi wa Vyama vya Ushirika, wanachama na jamii.

Mheshimiwa Spika, nne, Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati yaliyotolewa mwezi Juni, 2002. Katika kujadili Bajeti ya Fungu 24, Wizara ya Ushirika na Masoko iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali ilitoa maoni na ushauri ambao ulihitaji kutolewa taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni yaliyotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali ulihusu maeneo yafuatayo:-

(i) Malipo ya malimbikizo ya madeni ambayo wakulima wamekuwa wakividai Vyama vya Ushirika kama mkakati wa kuendeleza na kufufua Ushirika nchini.

(ii) Ahadi ya Wizara ya kusaidia kulimaliza tatizo la madai ya Vyama Vikuu vya Ushirika vya Nyanza na *KNCU* na Bodi za Mazao husika katika mwaka wa fedha 2002/2003.

(iii) Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika vilivyopo na juhudi za kuanzisha Vyama vipya vya Ushirika na kufufua vile ambavyo vinasuasua.

(iv) Uhamasishaji na utoaji elimu kwa wananchi kuhusu uanzishaji wa Vyama vya Ushirika kwenye maeneo ambayo Ushirika haupo kabisa kwa kutumia programu mbalimbali hususan Chuo cha Ushirika Moshi.

(v) Kusaidia kutatua tatizo sugu la baadhi ya wanaushirika kuhodhi uanachama na uongozi katika Vyama vya Ushirika.

(vi) Serikali kuangalia uwezekano wa kuyachukua madeni yaliyofikia shilingi bilioni 22 yaliyolimbikizwa na Vyama vya Ushirika kwa Mabenki ya Biashara.

(vii) Kuanza kutumika kwa Sera Mpya ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ilipitishwa na Serikali Aprili, 2002.

(viii) Serikali kuzihakikishia Bajeti za kutosha na vitendea kazi vyote Bodi za Mazao pamoja na kupitia upya (*review*), Sheria zilizoanzisha Bodi hizi ili kuzipatia nguvu na uwezo wa Kisheria wa kujipatia vyanzo vingine vya mapato.



(ix) Kuchukua juhudi za makusudi kusindika bidhaa ambazo tunauza nchi za nje ili kuziongezea thamani.

(x) Wizara kuhakikisha kuwa msimu wa ununuzi wa mazao unafunguliwa mapema ili kuepuka tatizo sugu la ulanguzi.

(xi) Uanzishaji wa magulio na vituo maalum vya ununuzi wa mazao (*Market Centres*) kama njia ya kukabiliana na hatimaye kutokomeza kabisa tatizo sugu la ulanguzi na ubabaishaji wa wanunuzi binafsi.

(xii) Uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa wakulima wa pamba juu ya umuhimu wa kuzingatia Kanuni ya Msingi ya kutenga pamba kwenye madaraja.

(xiii) Serikali ichukue hatua zinazostahili ili kunusuru kushuka kwa ubora wa zao la kahawa kutokana na ununuzi usiozingatia madaraja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Wizara ya Ushirika na Masoko na Serikali kwa ujumla, kwa hatua ambazo zimechukuliwa katika kutekeleza maoni na ushauri wote uliotolewa na Kamati (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara iliweza kukusanya mapato (maduhuli) ya kiasi cha Sh. 9,052,834/=, mapato hayo yalitokana na ada za zabuni na uandikishaji wa Vyama vya Ushirika. Aidha, matarajio ya kipindi cha mwaka 2003/2004 ni kukusanya Sh. 6,820,900/= kutoka kwenye ada za zabuni na uandikishaji wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 29 Mei, 2003 Wizara ilikuwa imetumia shilingi 4,578,041,938/= kati ya shilingi 6,147,524,600/= ilizotengewa sawa na asilimia 78.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara imepanga kutekeleza baadhi ya kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002.

(ii) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya mazao ya kilimo (*Agricultural Marketing Policy*).

(iii) Kuendelea na maandalizi ya programu ya kurekebisha uendeshaji wa Ushirika (*Cooperative Reform Programme*).

(iv) Kukamilisha Muswada wa Sheria wa Vyama vya Ushirika 2003 (*The Cooperative Societies Act, 2003*).

(v) Kukamilisha Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme*), kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

(vi) Kuratibu maandalizi ya kuanzisha Benki ya Ushirika ya Taifa.

(vii) Kuhamasisha wananchi kuunda Vyama vya Ushirika vya Msingi vinavyohusu sekta mbalimbali.

(viii) Kuendelea na uanzishaji wa Kituo cha Kuendeleza Masoko (*Marketing Development Centre*).

(ix) Kuendelea kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za Ushirika na Masoko na kuwaarifu walengwa.

(x) Kuendelea kufanya utafiti wa gharama za kununua na kuuza (*Marketing Costs*) ili kupendekeza njia za kupunguza gharama zisizo za lazima na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizipitia kazi hizo moja moja na kuridhika kuwa zimeelekezwa katika kujenga Vyama vya Ushirika endelevu, shirikishi na vinavyolenga kuleta ufanisi na tija. Hata hivyo, Kamati ilishauri Wizara kuendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wadau ili wachukue nafasi stabili katika mchakato na mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kubuni mpango wa kuanzisha Benki ya Ushirika itakayohudumia na kutoa mikopo kwa riba nafuu pamoja na kuviunganisha Vyama vya Fedha vya Ushirika. Kwa mantiki hiyo, Kamati inashauri Wizara kuchukua juhudi za makusudi kukamilisha uanzishaji wa chombo hiki haraka ili kitekeleze majukumu yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

Vyama vya Ushirika ni nyenzo muhimu katika juhudi zinazoendelea hivi sasa za kupambana na umaskini. Hata hivyo, bado maeneo na Mikoa kadhaa nchini haijahasishwa na kupewa elimu juu ya umuhimu wa Vyama vya Ushirika. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kufanya juhudi zaidi kuhamasisha wananchi kwenye maeneo hayo ili waanzishe Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa kuzingatia mazingira na mahitaji yao.

Uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi na vikundi vya Ushirika vinavyoongezeka kwa kasi, sharti uende sambamba na uimarishaji wa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), ili liweze kuvihudumia ipasavyo. Pamoja na juhudi za Serikali za kuongeza Bajeti kwa Shirika hilo, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuliimarisha zaidi ili liweze kuhimili kazi kubwa na wingi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika hasa ukizingatia ukubwa wa nchi yetu kijiografia. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa Sheria ya kuanzisha *COASCO* (Sheria Na. 15 ya 1982) iangaliwe upya, ili muundo wake na majukumu yake vikidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa fursa ya *AGOA*, miaka mitatu iliyopita, nchi yetu bado haijanufaika ipasavyo na fursa hiyo iliyotuwezeshwa kupenyeza bidhaa zetu kwenye Soko la Marekani kwa nafuu mkubwa. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kutekeleza azma yake ya kuanzisha Kituo cha Kuendeleza Masoko (*MDC*), ili kiweze kuwa kiungo muhimu cha *Trade Hubs*, ambazo zipo katika Mpango wa *AGOA*. Kamati inaamini kuwa kukamilika kwa kituo hiki itakuwa ni kichocheo kikubwa kwa nchi yetu kunufaika ipasavyo na Mpango wa *AGOA*.

Idara za Ushirika zina nafasi ya pekee katika kuhakikisha ustawi na maendeleo ya Vyama vya Ushirika kwa kuwa zinafanya kazi na kushirikiana kwa karibu zaidi na wananchi katika Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Pamoja na umuhimu huo, bado Idara hizo zinakabiliwa na tatizo la upungufu wa wataalam na vitendea kazi muhimu hususan vyombo vya usafiri. Aidha, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Mikoa na Wilaya walipelekewa jumla ya Sh. 46,500,000/=, kiasi ambacho ni kidogo sana. Hivyo, Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa Idara za Ushirika kwa kuzipatia wataalam, fedha na nyenzo zinazokidhi mahitaji halisi ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi George C. Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko na Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa ushirikiano na namna walivyowasilisha Bajeti hii ya Wizara kwa ufasaha. Aidha, nawapongeza Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dr. Ladislaus Komba, kwa ushirikiano na maandalizi mazuri ya mpango wa Bajeti. Kwa mara nyingine tena, namshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa ushirikiano na umakini wao wakati wa kujadili na kuchambua Bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo, Kamati kwa ujumla imekubaliana na mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na kuyapitisha

kama yalivyowasilishwa na Wizara bila mabadiliko yoyote. Kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara chini ya Fungu 24 ni kama ifuatavyo: Matumizi ya Kawaida Sh.6,831,540,900/=, Matumizi ya Maendeleo Sh. 3,407,045,339/=, Jumla Sh. 10,238,586,236/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, wasemaji wanne wa mwanzo katika hoja hii ni Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa Stephen M. Kazi, wajiandae.

**MHE. AISHA P. MAGINA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5)(b)(c) cha Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ninapenda kutoa pole kwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Balozzi George C. Kahama na Mheshimiwa Janet B. Kahama, kwa kufiwa na mtoto wao hivi karibuni huko Afrika ya Kusini na kuzikwa Jijini Dar es Salaam. Mwenyezi Mungu, awape moyo wa subira. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliohinda uchaguzi mdogo uliofanyika mapema Mei, 2003.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepitia katika majaribio mengi katika kutekeleza Sera za Chama Tawala, jambo ambalo limechangia sana kuua nguvu za uchumi wa wananchi. Mifano iliyo hai ni kwa kutoheshimu hata Azimio la Arusha lililosema wazi kuwa “njia kuu za uchumi zitamilikiwa na umma kwa kupitia Mashirika ya Umma na kwa kupitia Vyama vyao vya Ushirika”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwa kufilisiwa Vyama vya Ushirika, Benki ya Ushirika na mali za wanaushirika kinyume na Azimio la kuanzisha Sheria ya Jumuiya ya Muungano wa Vyama vya Ushirika ambavyo havitokani na Vyama vyenyewe vya Msingi, hivyo uwakilishi ukawa wa kisiasa zaidi kuliko Vyama vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo na kutokana na ushindani wa kibiashara na kwa Serikali kuondoa upendeleo maalum kwa Vyama vya Ushirika, vimekuwa dhaifu na kukosa nguvu za kiuchumi. Ni kutokana na makosa hayo, kwa kuwa Serikali imekuwa ikirudisha mali za wahujumu uchumi na kadhalika. Serikali irudishe mali ilizofilisi Vyama vya Ushirika hasa Benki ya Ushirika kutokana na mapato yatokanayo na kuuzwa Mashirika ya Umma kama NBC. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ushirika ni chombo muhimu sana katika kuiwezesha nchi kuondokana na suala la umaskini kwani Ushirika wa kweli hauna madaraja ya wanachama, unaendeshwa kwa misingi ya usawa kwa wanachama hasa katika kutoa mawazo, kutoa kauli na kufikia maamuzi kuhusu utendaji, utekelezaji, uendeshaji, tathmini na kwa lengo la kugawana maslahi kwa haki kulingana na mchango wa kila mwanachama. Mwanachama anakuwa na uhuru wa kujiunga, kuendesha shughuli zake kwa demokrasia na kutambua kuwa Ushirika huu ni mali ya Washirika na siyo mali ya Viongozi wa Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatana na hayo hapo juu, katika Ushirika wa Tanzania mambo hayo hayafuatwi na ndiyo maana Ushirika ama umekufa au uliobaki uko mahututi ni kwa sababu zifuatazo:-

- Ushirika haukuundwa na wanachama wenyewe wala wanachama hawana kauli na ndiyo maana viongozi wanafanya watakavyo. *(Makofi)*

- Kuna watu waliunda Ushirika wa kiukoo, hili siyo la uongo *SHIRECU* ni mfano halisi na Mheshimiwa Waziri anajua japo sasa ukoo wa *U-SHIRECU* umeondolewa. Tunaipongeza sana Serikali kwa hilo. (*Makofi*)

- Hata hao ambao wanajiita ni Wanaushirika, tulitegemea kuuza mazao yao kwenye Vyama vya Ushirika. Ukweli ni kwamba, hawauzi mazao yao hapo badala yake wanauza kwa watu binafsi na wakati mwingine hata Wenyeviti wa Vyama vya Ushirika wanafanya biashara inayofanana na Ushirika wanaouongoza na hivyo kuwa washindani. Siyo jambo la ajabu kuona Mwenyekiti wa Ushirika ananunua pamba, anachambua kwa kutumia Viwanda vya Ushirika na kuuza nje. Kwa sura hii Vyama vya Ushirika vitakufa. (*Makofi*)

- Kuhusu tatizo la Wanachama wa Vyama vya Ushirika kuwa wachache wakati wakulima ni wengi katika maeneo ambapo vyama hivyo vipo, ni kwa sababu ya wale waliopo wanaogopa kuingiza wanachama wengi ambao wanawaona kuwa tishio kwa ukiritimba na ulaji wao hivyo wanaogopa demokrasia itawatoa katika madaraka. (*Makofi*)

- Maafisa Ushirika wa Wilaya na Mikoa huwa wanashiriki kwenye Vikao vya Halmashauri ya Vyama vya Ushirika na kwa jinsi hiyo hujipatia posho ambazo huwaziba masikio na macho hivyo wasione matatizo kwenye vyama hivyo na ndiyo maana matatizo hayatatuliwi mwanzo yanapojitokeza hadi hapo kelele za wananchi zitakapomfikia Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri, ndiyo tatizo litatuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la msingi hapa ni kwamba, Vyama vya Ushirika vinafikia hali mbaya kama vile Mabwana Ushirika (*Co-operative Officers*) hawapo. Hapa lingekuwa jambo la busara kwa Serikali kuwashughulikia Maafisa hao ambao wamekuwa washiriki Wakuu kwa kuua Vyama vya Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

- Uundwaji wa Vyama vya Ushirika uwe rahisi na wa uwazi, wananchi waanzishe Ushirika wao kuanzia ngazi za msingi, ngazi za kati hadi kufikia Ushirika Mkuu. Kwani Ushirika wa sasa unaanzia juu kwenda chini, Ushirika wa kweli unaanzia chini kwenda juu. (*Makofi*)

- Vyama hivyo viundwe kwa misingi ya kiushirika (*Co-operative Principles*) na siyo kwa misingi ya kisiasa. Kwani vyama vilivyopo bado vina mtazamo wa kizamani kwamba, Chama cha Ushirika ni sehemu ya Chama cha Siasa. (*Makofi*)

- Vyama vya Ushirika viwe na uhuru wa kupanga bei ya kiushindani na wanunuzi binafsi.

- Kwa kuwa vyama vingi vina viwanda vya kusindika na kuchambua mazao kama pamba visiuze mazao yakiwa ghafi, hii inasaidia bei ya mazao kupanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ushirika Moshi kila mwaka kimekuwa ni hadithi kwamba, Wizara inaandaa na kuratibu chuo hicho kiwe Chuo Kikuu. Kambi ya Upinzani haina pingamizi kwa chuo hicho kubadili majukumu yake. Hofu yetu ni kwamba, chuo hicho kilikuwa kinatoa Elimu ya Ushirika kwa wanaushirika kuanzia *Primary Societies* hadi kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika. Jukumu hilo liliwafanya wanachama wengi na Viongozi wa Ushirika kuufahamu Ushirika na shughuli zake, ikiwa ni pamoja na kuendeleza demokrasia ya Kiushirika. Kubadili majukumu ya chuo hicho na kuwa Chuo Kikuu, Serikali imejiandaa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya awali ya Ushirika yaliyokuwa yakitolewa na chuo yatafanywa na nani? Kwani hatujaona katika Bajeti ya Wizara kuwa Vyuu vidogo vidogo vya Ushirika vimepangiwa kuchukua majukumu hayo na pia kama kuna mpango wowote wa kuvipanua vyuu hivyo kama vile Kizumbi ambayo ni *Branch of the Moshi Co-operative College*, ili kuchukua nafasi ya *Moshi Co-operative College* itakapokuwa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, Vyama vingi vya Ushirika vimeshindwa kufunga vitabu kwa muda unaotakiwa, hii inatokana na uwezo mdogo wa Viongozi wa Vyama hivyo wakati mwingine ni kwa kuhofia ubadhirifu kufahamika kama vitabu hivyo vitaandikwa na kufungwa. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa kila Chama cha Ushirika kiwe na programu ya kusomesha wataalam katika nyanja za Uhasibu, Utawala na *Marketing*. Bila ya kuwa na wataalam vyama vitakuwa havifungi vitabu. Pili, Vyama vya Ushirika vinaweza kuajiri Wahasibu binafsi kwa malipo ili waandike na kufunga vitabu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyama vingi vya Ushirika na Vyama vya Msingi kwa sehemu kubwa havikukaguliwa kutokana na Wakaguzi kuwa wachache. Kambi ya Upinzani inaona tatizo hili litakwisha kwa sababu tunaamini kuwa, Vyama vya Ushirika ni Vyama vya Wanaushirika wenyewe na hivyo wana ruhusa ya kuteua Wakaguzi Binafsi (*Private Auditors*). Tuachane na utaratibu wa sasa ambapo Mkaguzi wa Vyama vya Ushirika ni *COASCO* peke yake. *COASCO* haina *capacity* kifedha na Wakaguzi hawatoshi na Vyama vya Ushirika ni vingi. Hivyo, kuendelea na *COASCO* kama Mkaguzi pekee wa Vyama vya Ushirika ni kutowatendea haki Wanaushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muundo wa Vyama vya Ushirika, kuna kitu kinaitwa *Apex*. *Apex* ipo kwenye Ushirika wa mazao yote. *Apex* imeanzishwa kwa nguvu za Serikali, Serikali ilitunga Sheria na hata jina lenyewe likatajwa na Sheria hiyo badala ya Wanaushirika kutoka chini kupanda juu na kuanzisha *Apex* hiyo pamoja na kutaja jina. *Apex* imeshindwa katika majukumu yake pamoja na shughuli za kiutendaji wa kila siku. Kambi ya Upinzani inaona *Apex* ya aina hii ni mzigo kwa wakulima na Wanaushirika. Kambi ya Upinzani inadhani kama Serikali inataka kufufua na kuimarisha Ushirika, Serikali ilete Muswada wa kurekebisha Sheria iliyoanzisha *Apex* na kuruhusu Wanaushirika waanzishe *Apex* yao kwa mfumo wanaotaka wenyewe kwa kufuatana na kanuni na taratibu za kiushirika (*Co-operative Principles*) na masharti watakayokubaliana wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kudhihirisha kwamba Vyama vya Ushirika vimekufa, ni ushahidi wa maghala yaliyojengwa kwa ajili ya kuhifadhi mazao kiushirika, kwa sasa yanatumika na Serikali za Vijiji kwa kuhifadhi mahabusu badala ya kuhifadhi mazao na sehemu nyingine yamekuwa ni sehemu ya kupikia pombe haramu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

- Vyama vinavyoundwa kwa sasa vikabidhiwe maghala hayo bila masharti yoyote. *(Makofi)*
- Kama haiwezekani Serikali iyauze maghala hayo na fedha itakayopatikana inunue matrekta ya Kijiji ambayo yatasaidia uzalishaji wa mazao kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ushirika ndiyo njia pekee ya kufuta umaskini katika ngazi ya Kijiji hata mpaka Taifa. Ushirika wa sasa umeongeza umaskini kwa wananchi badala ya kufuta umaskini. Wanaushirika kwa sasa hawapati manufaa yanayotokana na Ushirika kama vile mgao unaotokana na faida (*dividends*). Pia mali za Ushirika ambazo zingetakiwa ziwanaufaishe Wanaushirika wote zinawanufaisha wajanja wachache na wengine kubakia watazamaji tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza sheria iwekwe bayana kumuwezesha au kumlinda mwanaushirika kuanzia wa chini mpaka wa juu ili afaidike na mapato ya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani katika hotuba yake ya mwaka 2001/2002, ilikuwa imetoa mapendekezo kuwa Wizara hii ivunjwe iunganishwe na Wizara ya Kilimo na Chakula kama ilivyokuwa zamani kwa sababu kuu zifuatazo:-

- (i) Fedha nyingi zinatumiwa kuhudumia Wizara badala ya kuendeleza Ushirika. *(Makofi)*
- (ii) Kwa kufanya hivi tunapunguza ukubwa wa Serikali ambao siyo wa lazima. *(Makofi)*
- (iii) Wizara imeshindwa kujenga imani kwa Wanaushirika. Kwa mfano, Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikitoa kauli kwamba, wale waliofilisi Ushirika watachukuliwa hatua hata kufilisiwa mali zao. Serikali haijamkamata hata mmoja wala kumfilisi yeyote. *(Makofi)*

(iv) Kwa kuwa kauli hizi zimetolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali akiwemo Waziri Mkuu katika hotuba zake lakini hakuna linalotekelezwa, hii ni kuonyesha kushindwa kwa Serikali kusimamia Ushirika. Kwa hiyo, Serikali iwajibike kwa watu waliopoteza fedha au kudhulumiwa mali zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano walionipa katika kuandaa hotuba hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge na wewe Mheshimiwa Spika kwa kunisikiliza, ahsanteni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba iliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kumpa pole Mheshimiwa Balozi Sir George Kahama, kwa msiba mkubwa wa kupoteza mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 wakati nachangia hapa nilikuwa nimeahidi kwamba, kama zisingechukuliwa hatua zozote kushughulikia waliosababisha ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika basi ningekuja na hoja ya kuunda Tume ya kuchunguza waliopewa majukumu hayo ni kwa nini wanashindwa kufanya kazi yao. Lakini hapa katikati nikafanikiwa kuibana Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Serikali ikaeleza hatua mbalimbali na leo hii katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa mara ya kwanza imetoa *paragraph* nzima ikielezea jitihada mbalimbali ambazo Serikali inachukua kushughulikia waliosababisha ubadhirifu. Kwa kweli ninafarajika kwa sababu sikuona popote pale ambapo sasa Serikali inasema si kazi ya Serikali na Vyombo vya Dola, neno hilo halimo kabisa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kama lingekuwepo basi ningengea tofauti na ninavyoongea sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, sina nia ya kugombana na Serikali katika hili kwa sababu sasa inaonekana wameamua kulifanyia kazi. Orodha imetolewa hapa inaonyesha kesi ambazo zimeshafikishwa Mahakamani, waliofungwa, upelelezi unaendelea, labda nitoe tahadhari kwamba, mwaka ujao tusielezwe tena kwamba upelelezi bado unaendelea kwa sababu upelelezi ukiwa *indefinite* inakuwa haina maana yoyote. Napenda niseme hapa kwamba, wahusika wanaweza kunywa soda kidogo na kuendelea kuwa na uhakika na kazi zao wala simuombi tena Rais, kuwaondoa katika kazi zao na badala yake sasa niwaombe wafanye kazi yao na kama walivyoeleza na Bajeti ya mwaka kesho nitakuja na orodha hii, niuweke hapa, niangalie kuanzia leo mpaka wakati huo ni kazi ipi itakuwa imetendeka.

Mheshimiwa Spika, leo hii asubuhi wakulima wa kahawa Tanzania wameamka hawawezi kunywa chai nzuri kama ambavyo wangependa wanywe, baadhi ya watoto walitakiwa kwenda shule lakini hawawezi kwa sababu hakuna karo, lakini vile vile watoto wao wanaumwa wangependa waende hospitali lakini hawawezi kufanya hivyo kwa sababu pato la kahawa limeshuka kwa zaidi ya asilimia 60, ikimaanisha bei ya kahawa anayopata sasa hivi ni robo ya bei aliyoipata miaka 40 iliyopita, hili ni jambo la hatari kabisa na huyu ndiye mkulima wa kahawa tunayemtetea. Lakini baya zaidi hata fedha ya *STABEX* aliyotegemea kwamba walau itakuja imsaidie kupunguza matatizo hayo na yenyewe jana Serikali imetoa maelezo ya kina kwamba, mkulima hawezi kupatiwa. Sasa ni matatizo makubwa hao ndio wakulima tunaowawakilisha na hali yenyewe ndio hiyo. (Makofi)

Tunaweza kukaa sana hapa Bungeni tunagombana na Sir George, Serikali na huyu, kumbe tunaogombana nao ni maskini wenzetu na wao hawana la kufanya. Sasa hili ni tatizo kama hatujui tatizo liko wapi tutapiga kelele sana, tutashikana mashati hapa, tutawekana msalabani lakini kumbe mhusika hayupo hapa yupo sehemu nyingine kabisa amepumzika. Nilikuwa najaribu kuliangalia hili nikajuliza tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tunayo makampuni kama matano duniani yanayofanya biashara ya kahawa na makampuni haya ni *Kraft, Nestle, Protector and Gamble, Sara Lee* na Kampuni kubwa ya Kijerumani inayoitwa *Tchibo*. Makampuni haya biashara yake kwa mwaka ni zaidi ya trilioni 55 lakini fedha inayokwenda kwa wakulima wa kahawa duniani kote ni trilioni 8 tu. Kwa hiyo, tunachosema

ni kwamba, kuna makampuni machache duniani yanayonufaika na biashara ya kahawa wakati yenyewe yanapata trilioni 55, wakulima wa kahawa wote duniani wanapata trilioni 8 kwa fedha za Kitanzania. Lakini makampuni hayo matano tu wakati mkulima wa kahawa anapata asilimia 2 tu ya bei ya kahawa duniani, yenyewe yanatengeneza faida kubwa ya zaidi ya asilimia 30 ya *profit margin* na faida za namna hii kiuchumi zingeweza kupatikana mbinguni sio duniani lakini makampuni haya yanatengeneza faida hiyo duniani.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo tu mwaka 1980 mkulima wa kahawa akitaka kununua jembe alihitajika auze kilo nne, mwaka 1990 mkulima wa kahawa alihitajika auze kilo 7 ili aweze kununua jembe la mkono, mwaka 2000 hali ikawa mbaya zaidi alihitajika auze kilo 8 aweze kupata jembe la mkono na mwaka 2001 alihitajika auze kilo 10 za kahawa safi kununua jembe la mkono, hali hii ni ya hatari kabisa. Ndio maana nasema hapa kuendelea kugombana na Serikali, Sir George na nini, ni kupoteza muda bure maana wote hawa ni maskini wenzetu na kwa kweli wamejikuta kwenye dunia ya utandawazi ambapo wanashindwa wafanye nini.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kama Wabunge, hatuwezi kuishia hapo lazima tujiulize tunaweza kufanya nini. Kuna faraja kidogo kwamba, Bunge la Ulaya lilitoa tamko kwamba, mkulima wa kahawa ana matatizo makubwa na inafaa asaidiwe. Vile vile Bunge la Spain nalo likatoa tamko rasmi kwamba, kwa kweli mkulima wa kahawa wa nchi maskini amepata matatizo makubwa anatakiwa asaidiwe. Hata Wamarekani ambao tungefirikia hawajui matatizo hayo *US Congress* na *Senate* wakatoa tamko rasmi kwamba, kwa kweli mkulima wa kahawa amepata matatizo makubwa anatakiwa asaidiwe.

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo ni kwamba sisi hapa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao tunawawakilisha wakulima hawa hatujatoa tamko la kusema mkulima sasa yuko katika matatizo makubwa na inafaa asaidiwe. Sasa hiyo ni changamoto kwetu sijui tunaweza tukalifanyaje? Lakini napenda kusema ingekuwa bora tutoe tamko ili kuonyesha nguvu za kisiasa na utashi wa kisiasa kwamba, wakulima wetu wako katika matatizo makubwa na tungependa wasaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana tumeona maelezo ya Serikali kuhusu *STABEX*, ukitazama maelezo yote yale yanakwambia jambo moja tu la msingi kwamba, uwezo wetu wa kujenga hoja ni mdogo ndio maana unaenda kule unaeleza wanasema lakini sasa mbona ninyi hamjui wakulima waliozalisha kahawa na kwa sababu hujajiandaa vizuri basi unasema ni kweli sijui mkulima aliyezalisha kahawa unakaa chini unarudi hapa kuja kutoa ufafanuzi kwenye Bunge, tatizo ni ule udhaifu wa kujenga hoja.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo kubwa kuliko hilo, tatizo ni kwamba, nchi maskini moja moja haina uwezo wa kwenda *European Union* na ikajenga hoja ikaeleweka, ni ngumu sana. Utaenda Tanzania utaeleza mambo yako tu, kwanza ukifika pale Amsterdam, kama hujawahi kufika kule kwanza utapotolea pale kwenye uwanja wa ndege, hatua ya kwanza ya kushindwa kufikisha sawasawa hoja ulizokwenda nazo. Ukifika kwenye jengo lile kubwa unapanda kwenye *lift*, unapigiwa muziki na unawekewa wasichana wazuri wanakunywesha *whisky*, tayari umesahau kabisa kwamba umeenda kujenga hoja, sasa hilo ni tatizo la kimsingi kabisa. Wanafanya mambo haya sio kwa bahati mbaya ni kwa makusudi kabisa kwamba, hawa wakifika hapa basi watafuata tutakayotaka sisi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna tatizo sio la Serikali yetu tu, sio sisi Watanzania tu, nchi zote maskini inabidi ziungane ili kujenga hoja. Tukiendelea kusema sijui Waziri wa Fedha alienda kule akaongea nao, Waziri wa Fedha hawezi kujenga hoja hii lazima kuwepo ushirikiano wa pamoja. Ukisema na Mheshimiwa Keenja alienda sijui akafanya nini hii haiwezi kusaidia lazima tulitazame hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nilishukuru Shirika la *OXFAM* kwa sababu limefanya kazi kubwa ya kujaribu kutetea nchi maskini. Lakini napenda niseme ni vizuri tukatoa tamko na tukajaribu kujielekeza kwenye mambo mbalimbali ambayo ni ya kimsingi. Tueleze matatizo ambayo yanatukabili lakini vile vile tuziambie nchi tajiri hizi ziondokane na tabia ya kutoa ruzuku kwa sababu nchi maskini zinapata hasara ya trilioni bilioni moja kila siku kwa sababu ruzuku ambazo nchi zilizoendelea zinatoa katika nchi zao. Lakini vile vile bado kuna kodi, ukitaka kuingia kwenye Soko la Ulaya kuna kodi ya zaidi ya asilimia 10 katika kahawa, tuwaambie waondoe kodi za namna hiyo. Vile vile haya makampuni makubwa ambayo mimi nayaita Vibaka Uchumi, yaache tabia ya kunyonya nchi maskini na kuendelea kutengeneza faida kubwa

huku mkulima wa kahawa akiendelea kupata matatizo siku hadi siku. Vile vile tuwaambie *IMF* na *World Bank* wao siku zote walikuwa wanatushauri na sisi tunasema sasa tuko katika janga hili wanatushauri nini ili kuweza kumsaidia mkulima wa kahawa? Nimezisikia hoja ambazo Serikali imetoa hapa kuhusu *STABEX*, kwa kweli hoja zote hazina uzito wowote lakini kama nilivyosema, kuendelea kugombana hapa ni kupoteza muda tujaribu kuangalia tumekosea wapi ili mbele ya safari tuweze kujisahihisha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika Sheria Mpya ya Kahawa, tulianza mfuko wa ku-*stabilize* bei ya kahawa. Sasa wakati umefika tuanze kutenga fedha kwa ajili ya kuweka katika mfuko huo na tuweke mikakati ya kuwezesha mfuko huo kuanza kufanya kazi ili tuachane na mawazo ya kugombana kuhusu *STABEX*, fedha ambayo siyo yetu na badala yake tuwe na utaratibu wetu sisi wenyewe wa kuwa tuna-*stabilize* bei za mazao yetu. Tukiweza kulitekeleza hilo tutaondokana na ugomvi mwingine ambao kwa kweli baada ya kujifikiria sana nikagundua kwamba, hapa huenda tunagombana tu na kupoteza muda kwa vitu ambavyo kusema kweli tungeweza kuviepuka kama tungeweza kufikiria tufanye nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ili nitoe mchango wangu kwa Wizara hii ya Ushirika na Masoko. Pia napenda niipongeze Wizara hii ya Ushirika na Masoko, tangu ianze imeonyesha ubora wa kazi zake hadi kufikia sasa. Ukisoma hotuba ya mwaka huu wa 2003/2004 ukilinganisha na ya mwaka 2002/2003, unaweza kuona yapo mabadiliko makubwa, ufanisi mkubwa, kwa kweli siwezi kuwa mchoyo wa kuwapongeza kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tunashauriwa kusoma Ripoti ya Kamati iliyoungwa kutazama kwa nini Ushirika ulikuwa unadorora, tungeweza kujua kwa nini Serikali iliamua kuunda Wizara hii. Kama Wizara hii ilikuwa kama Kitengo kwenye Wizara nyingine tukawa na matatizo leo tena tunasema Wizara hii ivunjwe, basi hii ni bahati mbaya sana. Kwa kweli wanaojua Ushirika wanaona kwamba, kuundwa kwa Wizara hii ni ukombozi wa Ushirika katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kupongeza, nadhani watu watasema huyu bwana amesimama kupongeza tu, kwa kweli najaribu kutazama mambo yaliyokuwepo na hali ilivyo sasa hivi. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kubuni utaratibu huu wa kuanzisha *Export Guarantee Scheme*. Vyama vingi vya Ushirika vilikuwa vimekwama lakini kutokana na utaratibu huu sasa hivi Vyama vinaaminika, vinakopesheka na taarifa tuliyoipata ni kwamba, Vyama vyote vilivyokopeshwa fedha ya kununua mazao vimerudisha fedha hizo, hili sio jambo dogo ni kubwa sana kwa sababu mamilioni yalikuwa yanapotea lakini leo vyama vyote vimerudisha, hili ni jambo kubwa na ni maendeleo makubwa. Tunaomba Idara ya Ushirika na *COASCO*, kufuatilia mambo mengine ya mikopo na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesikia kwamba, Wizara inajaribu kuleta Bungeni Marekebisho ya Sheria na hii itasaidia sana. Juzi tulikuwa tunazungumza habari ya vikundi vya akina mama vya akiba na mikopo, pengine sheria hii itaanza kutambua vikundi vidogo vidogo vya akina mama, vijana, wazee ili kuvilea na hatimaye kuimarisha Ushirika katika nchi hii. Bila kufanya hivyo, vikundi vidogo vidogo vya akina mama, wazee, vijana vya kuweka na kukopa ambavyo havitambuliwi kisheria, sheria hiyo kama italetwa ikiwa na mabadiliko ya aina hii tunaweza kuongeza Ushirika katika nchi yetu na kuboresha zaidi hali za wananchi wetu.

Ninaomba niseme kwamba, pamoja na mafanikio yote yanayoonekana, lakini naona Serikali imesinzia mahali pamoja. Naomba sasa Serikali iviwezeshe Vyama vya Ushirika kushika uchumi wa nchi hii sio tu katika sekta ya mazao. Kwa mfano, katika zoezi linaloendelea sasa hivi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, sijaona Vyama vya Ushirika vimechukua umiliki au hisa kwenye makampuni ambayo yalikuwa ya Serikali. Kwa hiyo, kwa makusudi kabisa, Serikali ichukue jukumu la kuviwezesha kimtaji ili viweze kuendesha mashirika makubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile ili tuweze kuendeleza Ushirika lazima Serikali ichukue jukumu kubwa zaidi katika kutoa elimu ya Ushirika. Aidha, Naibu Waziri wa Serikali za Mitaa, namwona hapa,



achukulie kwamba, Ushirika katika Serikali za Mitaa ni eneo mojawapo ambalo linaweza kuboresha maisha ya wananchi. Kwa hiyo, kwa makusudi kabisa, Serikali za Mitaa ziwe zinatenga fedha kwa ajili mafunzo ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuendelea. Bila Serikali za Mitaa kuchukua jukumu hili, Ushirika hautakwenda mbali kwa sababu Sekta ya Ushirika iko chini ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakipongeza Chuo cha Ushirika Moshi kwa hatua iliyofikiwa. Tulipewa taarifa hapa nadhani Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu na Mheshimiwa Dr. Ng'wandu kwamba, mipango ya kukifanya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Shirikishi cha Chuo Kikuu cha Sokoine imefikia mahali pazuri. Kwa hiyo, naupongeza sana Uongozi wa Chuo cha Ushirika Moshi kwa kazi waliyoifanya. Hayo sio mambo madogo, *University* haiwezi kuwa *University* kwa siku moja, kuna utaratibu mwingi, kuna Kamati nyingi, mtazamo wa fedha na kadhalika. Kwa hiyo, hatua hiyo mliyofikia tunaipongeza ingawa wenzetu wa Kambi ya Upinzani hapa hawaoni hilo, lakini hii ni bahati mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya, sasa hivi wameanza ku-*recruit* Maafisa Ushirika katika Wilaya zetu. Kwa mfano, Wilaya ya Ludewa nilikuwa na Afisa Ushirika mmoja tu lakini sasa hivi tumepata wawili na nadhani tutapata na wa tatu. Kwa hiyo, hiyo peke yake tunakupongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina ombi lakini ni gumu, pengine Wizara ijaribu, naomba ikiwezekana tuna vijana wengi waliopata *Advanced Diplomacy* katika Chuo cha Ushirika, lakini walipata *retrenchment* waombewe kibali cha kuajiriwa. Wapo vijana wamesoma vizuri, wana elimu ya kutosha na walikuwa wanafanya kazi vizuri, lakini kwa sababu ya kupunguza tu walikuwa hawana kasoro. Pawepo na kibali maalum kumwomba Rais kwamba, tunaomba watu hawa badala ya kuwa *reinstated* wawe *re-employed*, hii inawezekana. Mara nyingi Serikali badala ya kuwarudisha wanaajiriwa upya, sasa hivi wanapata tabu sana anaambiwa wewe ume-*retire*, ka-*retire* mtu ana miaka 25? Kwa hiyo, tunaomba badala ya kuwa *reinstated* wawe *re-employed freely* na Halmashauri zijulishwe kwamba, hao watu hawana makosa yoyote walipunguzwa tu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza, nimeona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia habari ya *Code of Conduct* ya *Cooperative Management*. Hili ni moja katika matatizo yaliyokuwa yanasababisha Vyama vya Ushirika viweze kuanguka kwa sababu tulikuwa tunachukua watu kiholela tu. Lakini kwa sababu sasa kutakuwa na hii *Code Of Conduct*, tutajua kwamba, mtu huyu ana sifa zipi ili kuweza kusaidia kuendesha Vyama na vile vile watumishi wawe na utaalum wa namna gani, sifa zipi na kadhalika. Kwa hiyo, hilo nalo nawapongeza. Pamoja na hayo, nafikiri bado Idara ya Ushirika inahitaji kuimarishwa zaidi kwanza idadi ya watumishi, sifa zao, mafunzo, vyombo vya usafiri na kadhalika na vile vile wangeweza kupewa *OC*. Sisi wengine tumewahi kufanya kazi hizi, unaweza kuwa hufanyi kazi kwa sababu huwezi kufika kijijini, huwezi kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imetolewa hapa kwamba, Maafisa Ushirika wasifike kwenye mikutano, looh, hii ni hatari Afisa Ushirika asifike kwenye mikutano tena itakuwaje? Anatakiwa afike kwenye mikutano kwa sababu anatakiwa atoe ripoti, anatakiwa ahojiwe, sasa leo asifike huko afike nani sasa? Haiwezekani kwa sababu anatoa ushauri unaohusika na sheria na *accounts* na uendeshaji na kadhalika, kwa hiyo, lazima afike huko mradi tu tukiwa na Afisa Ushirika waaminifu, waliosoma vizuri na wenye utaalum. Kwa hiyo, nashauri wawezeshwe hawa kwenda vijijini kufanya kazi zao, vinginevyo tuingoja *COASCO* ifike itakuta mahesabu yako shaghalabaghala, hawa wanaandaa *accounts and management* kuwa nzuri. Kwa hiyo, wawezeshwe kuweza kufika huko vijijini ambako wananchi wako.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu masoko. Palikuwa na agizo hapa nadhani ni zuri, pamoja na sera ya soko huria, lakini tulikubaliana kwamba, hawa wanunuzi binafsi wa mazao tukutane nao kwenye mnada bado wengine wanazengeazengea huko vijijini, ndio wanaotuharibia ubora wa mazao yetu. Kahawa inakuwa ya ovyo kwa sababu ya wafanyabiashara kwenda kugombea huko kwenye uzalishaji, wao wangoje kwenye mnada. Kwa hiyo, hili nalo likisisitizwa linaweza kuleta mambo mazuri tu. Nafikiri Vyama vya Ushirika vingebuni utaratibu wa kupunguza muda wa malipo toka kahawa inunuliwe inaweza kununuliwa mwezi Oktoba anakuja kupata hela zake baada ya miezi tisa au sita kwa hiyo muda wa kungojea malipo unakatisha tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha katika ushindani wa dunia ya leo linalofanya soko la mazao yetu liende chini nadhani tumeshagundua kwamba ni ubora wa mazao yenyewe. Nafikiri kwa sababu hatuna vinu vya kukoboa mazao katika *center* fulani ili wakulima wapeleke kukoboa kahawa katika *center* hiyo, nasikia wenzetu Kenya kule wana vinu katika maeneo kadha wa kadha ili kuinua na ubora wa mazao. Tatizo sasa ni Wizara ya Nishati hakuna umeme ni tatizo kwenye Wilaya, hakuna umeme je, huko vijijini? Pia kutokuwepo kwa wataalam nalo ni tatizo kwa hiyo bei ya kahawa inazidi kwenda chini. Pia ughali wa pembejeo nalo ni tatizo, usafiri wa kusafirisha mazao, nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza sana mlipotoa hoja ya kuanzisha Benki ya Ushirika, huo ndio ukombozi kwa kweli wa kuwezesha Vyama vya Ushirika. Hoja ya kudai mambo yaliyopita nayo tuyaache sasa hivi Wabunge wote tutazame mbele kusaidia namna gani tunaweza kufufua Vyama vya Ushirika kuliko kulaumu. Hakuna ukombozi mwingine kwa mkulima unaoweza kusaidia Vyama vya Ushirika ni Wabunge sisi tukihasabiana hapa ukiuliza nani yuko kwenye Chama cha Ushirika huko kwake hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ushirika na Masoko. Nianze kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Sir George Kahama, pamoja na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kifo cha mtoto wao mpendwa, tumwombe Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amin*.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kuleta taarifa hii katika Ukumbi huu wa Bunge ikiwa na sura nzuri namna hii, nawapongeza sana. Nitaendelea kutoa pongezi kwa sababu ni kitu ambacho kinaonekana na ni vema tu ukasema ukweli ulivyo, niendeleo kumpongeza Waziri kwa azma ya Serikali ambayo imekuwa ikisisitizwa katika Bunge hili kuhamishia Makao Makuu yawe Dodoma, yeye kwa asilimia 100 ameteketeza, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yeye amelitaja kwa kifupi sana katika ukurasa wa 40 lakini nadhani ni nafasi yetu sisi Wabunge kupita katika Wizara yake na kujionea wenyewe kwa sababu kazi iliyofanyika pale ni ya kihistoria. Pesa tulizoziruhusu mwaka 2002 kama ni kufanya kazi basi Mheshimiwa Sir George Kahama, kwa kweli pesa hizo ulizitumia zilivyo badala ya kununua magari ya *luxury* umeona uweke msingi kwa ajili ya vizazi vijavyo, nakupongeza sana. Wizara hii ni mpya, ina umri wa miaka miwili na nusu kama alivyoeleza Waziri na kazi iliyopewa ilikuwa ni ngumu sana, kufufua Ushirika ni kazi ngumu, hali iliyokuwa nayo Ushirika ilikuwa mbaya, wizi, ubadhiriifu na kila aina ya vurugu. Nina imani kubwa kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri bila kuleta sheria mpya hapa Bungeni, kazi ingeendelea kuwa ngumu kwake.

Lakini basi nimshukuru sana kwa kuleta sheria hiyo mpya hapa Bungeni na kwa bahati nzuri tumeisoma kwa mara ya kwanza, tutakwenda nayo ili mwezi Novemba, 2003 tuje kuweza kuchangia mawazo yetu. Nina imani kubwa kabisa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yenu mtapata nafasi ya kuweza kuijadili na wananchi na wanaohusika kwa ujumla na baadaye itakuwa na *impact* nzuri ya kuweza kuwa sheria ambayo itakuwa na mlolongo mrefu wa kuweza kudumu bila kufanyiwa marekebisha kwa sababu itakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kujadiliwa na kutolewa ushauri mahali panapowezekana, tutaleta picha ya umma katika Bunge hili ili tuweze kurekebisha ambapo tunaweza kurekebisha. Lakini kwa sababu mimi sheria hii nimeanza kuipitia mengi yamegusa katika utaratibu ambao nadhani ni wa wanaushirika, imegusa mengi mazuri sana. Kwa kweli hili halitakuwa na matatizo makubwa.

Kwa hiyo, ninakupongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuliona hilo ili sheria zetu ziwe zinasomwa kwa Mara ya Kwanza, halafu twende nazo, tuzipeleke kwa wahusika ili baadaye tutakapokuja hapa tunakuja na mawazo. Kwa hiyo, utungaji wetu wa sheria utakuwa katika picha ambayo kwa kweli tutakuwa tunatunga sheria ambayo inagusa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Ushirika ulivyo kwa sasa. Kwanza, niendeleo kuipongeza Wizara, kweli imevisaidia sana Vyama vya Ushirika kupata mikopo katika mabenki.

Wamezungumzia hili katika ukurasa wa 26 kwamba kumekuwa na msaada huu ambao kweli Wizara imeshughulikia vizuri sana. Lakini niseme kwamba bado kuna matatizo ambayo ni magumu kwa Vyama vya Ushirika. Si rahisi kupata faida. Matatizo yenyewe ni kule kuupata mkopo kunakuwa na *facilities fee* ambayo ni *one percent* ya mkopo. Kwa hiyo, hilo ni tatizo na hiyo pesa imekwenda mapema kabla hata hujachukua mkopo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili ni kuhusu riba. Tunaipongeza Serikali angalau riba imeshuka kidogo kutoka kwenye asilimia 21 sasa hivi ipo kwenye asilimia 15, japo bado ni kubwa. Kwa hiyo, ushindani unakuwa ni mgumu zaidi. Asilimia 15 bado kuna zile gharama za kupewa mkopo, bado kuna hawa wasimamizi wa mkopo, dola 2,500 kwa mwezi mara miezi ambayo utakaa na hayo mazao kabla hujayauza ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mfano, ukiangalia katika Wilaya ya Biharamulo wanatozwa shilingi 2,500/= *Collateral Manager*, ni tatizo kubwa bado wanakwambia kwamba lete nusu ya mazao katika ghala halafu baadaye tukuandikie *Certificate* ndiyo ukapewe tena. Sasa mkopo unakuwa na masharti magumu. Kwa hiyo, Wizara iangalie kuona kwamba bado kuna tatizo kubwa la mtaji kwenye Vyama vya Ushirika. Mabenki bado yanafanya biashara katika njia ya kuweza kunyanyasa Vyama vya Ushirika.

Kwa hiyo, Serikali ifanye makusudi mazima kabisa ya kuona jinsi gani ifufue ushirika katika suala la mtaji, ndiyo itakuwa jambo muhimu zaidi la kuweza kukomboa wanaushirika wetu. Tusipoangalia suala la mitaji bado tutazidi kuimba katika utaratibu ambao utatuweka katika hali moja ambayo ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, athari zake kutokana na masharti mazito hayo kwanza hawatafikia lile lengo. Umekisia kununua kilo milioni 50 za pamba, hali halisi unakuwa na milioni kumi tayari umeshakula hasara kubwa sana. Kurudisha mkopo matokeo yake unauza assets za wanaushirika kitu ambacho sasa unazidi kuudidimiza ushirika katika utaratibu huo. Kwa hiyo, tuzidi tu kuiomba Serikali ibadilishe utaratibu huo na kuona kwamba inaingia namna gani hasa kwa makusudi mazima.

Sasa nigusie suala la ajira ya watumishi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, alikuwa anajibu swali Bungeni hapa akasema kuna mpango wa kuajiri watumishi 400, lakini katika hotuba hii sijaona. Tatizo kubwa sana la watumishi katika Vyama vya Ushirika au katika Halmashauri zetu bado ni kubwa mno. Utakuta baadhi ya Wilaya ni Maafisa wawili au mmoja. Sasa wawili au mmoja atafanya kazi gani?

Kwa hiyo, Ofisi ya Rais, Utumishi, ione uwezekano wa kutoa vibali ili angalau waweze kuajiriwa watendaji wa kutosha ili tuweze kuendana na suala la kufufua Ushirika katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la ajira ni muhimu mno na naomba sana Serikali ijaribu kulitilia maanani. Waajiri Maafisa Ushirika wa kutosha na bado pawepo na nafasi ya Wizara kufuatilia mpaka angalau kwenye maeneo ya Wilaya. Sasa hivi utakuta Maafisa Ushirika ndiyo wanaofanya kazi za kukusanya kodi badala ya kufufua Ushirika. Anapangiwa na Mkurugenzi kazi nyingine ambazo hawezi kuzikataa. Sasa pawepo basi na nafasi ya Waziri au Wizara yenyewe kuwafuatilia mpaka angalau huko walipo ili waweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Pia naomba nigusie suala la kuvunjwa kwa Vyama vya Ushirika mwaka 1976. Serikali nadhani inalifahamu vizuri hilo na kweli Vyama vya ushirika vilivunjwa na mali za Vyama vya Ushirika zilichukuliwa katika hali ambayo kwa kweli haikuwa ya mazungumzo. Ilifika mahali unaambiwa wewe ondoka Meneja na Halmashauri yako sasa tunaweka huyu mtu mwingine analinda hii mali mpaka kuja kurudisha mwaka 1984. Sasa huo muda wa mpito mali nyingi za wanaushirika zilipotea.

Sasa Wizara inatakiwa ifuatilie kuona kwamba ni mali zipi ambazo bado zimesalia kwenye Mashirika mbalimbali ambayo wanaushirika walikuwa wameweka hisa zao. Mfano, halisi ni kwenye Kiwanda cha *MWATEX* ambacho kimeshauzwa au kubinafsishwa sikumbuki sawa sawa. Sasa kulikuwa na hisa vya Vyama vya Ushirika, ziko wapi na zina hali gani?

Mheshimiwa Spika, kuna *Pamba Engineering* pale Mwanza imeshauzwa, sifahamu sasa hivi Vyama vya Ushirika vya Buha, *SIRECU* ya Singida, *Nyanza Cooperative Union*, *SHIRECU* na *MARACU* walikuwa na hisa kwenye hiyo kampuni. Sasa hilo nalo sielewi kwamba wamefikia wapi. Lakini kubwa zaidi ni kwenye Benki ya *CRDB* iliyopo sasa hivi. Vyama vya Ushirika vilikuwa na pesa zake, nina imani mpaka sasa hivi bado kuna pesa hapo. Sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Waziri kuweza kufuatilia na kuona kwamba hizo pesa zilizopo hapo ziweze kupatikana na ndiyo zisaidie ikiwezekana kuanzisha Benki ya Ushirika ambayo wanaushirika wanaitegemea kwa asilimia kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nigusie suala la *Stabex*. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, wakati anajibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, alitamka kwamba zao la pamba si muhimu kwa hiyo, halihusiki katika suala la *Stabex*. Kwa kweli sisi walima pamba raha ilituishia na nilichukua jukumu la kuweza kufuatilia na kuona kwamba ni kweli au vipi. Kwa bahati nzuri, kwanza nimpongeze Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa kauli yake ya Serikali ambayo ilinipa picha nzuri baada ya kutamka kwamba hata zao la Pamba linashughulikiwa, limo na lenyewe lina pesa zake. Nampongeza sana Waziri kwa taarifa yake hiyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba katika kufuatilia kufuatilia kwangu zile pesa za *Stabex* ya Pamba ni kweli zilishafika Mwanza na wadau huenda walikaa. Sasa sijui wadau ni wapi ambao walikaa. Kazi iliyofanyika imefanyika katika eneo la Chuo cha Utafiti Ukiriguru. Chuo cha Ukiriguru kipo katika Wilaya yangu ya Misungwi, ukarabati uliofanyika pale umeonekana kwa kweli ni hali ya kutia matumaini lakini kwa sababu hatukuelezwa unalalamika. Kwa hiyo, kitu kama hicho ni vema basi Wabunge na Madiwani wa maeneo fulani wahusishwe ili waweze kuelewa pesa za wananchi wao zimetumika vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi hilo naona limekwenda vizuri lakini kwa sababu Wabunge hawakuelimishwa ndiyo maana wanalalamika. Pesa za Pamba zilikuwa ni kidogo, zimefanya kazi ikiwemo kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Chuo cha Utafiti cha Ukiriguru. Kwa hiyo, maelezo kama hayo kama yatatolewa hapa mara kwa mara inakuwa ni nafuu kwetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niipongeze Serikali kwa kuweza kufuatilia kesi mbalimbali za Vyama vya Ushirika kama alivyosema Dr. Diodorus Kamala, ni kweli amefuatilia sasa hivi angalau watu wanachukuliwa hatua na kufufua kesi zingine ambazo zilikuwa katika hali mbaya. Maana tumekuwa na historia Vyama vya Ushirika vingi kesi zake hazishindi matokeo yake ni kutupiliwa mbali na baadaye huyu aliyewaibia anawaomba tena mumfidie. Kitu ambacho kwa kweli wanaushirika kimekuwa kikiwakosesha raha.

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo sana Chuo chetu cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu. Wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, ni shahidi na ni Mwenyekiti wetu wa Bodi hiyo ya Chuo cha Ushirika. Nina imani kubwa na wewe kwamba kukwama kufikia kuwa Chuo Kikuu kuna kitu ambacho kilikuwa nadhani hakijakamilika nina imani kabisa kwamba kwa umahiri wako kitakuja kikiwa kimekamilika na baadaye kitaweza kupita kwa asilimia kubwa na kuwa Chuo Kikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo basi niunge mkono kwa asilimia mia moja kabisa ili Waziri wetu wa Ushirika na Masoko, aweze kutumia pesa hizo kwa maendeleo ya Wanaushirika nchini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Ushirika na Masoko. Kwanza ningependa nimpe pole Waziri, Mheshimiwa *Sir* George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa tatizo lililowapata la kupoteza kijana wao. Kwa kweli tunamwomba sana kwa Mungu ili kijana huyu roho yake iwekwe mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pili, ni lazima niseme wazi kwamba hotuba ya Waziri imekuwa wazi, imeandaliwa vizuri na imenipa picha ya kuona kwamba kuna bidii kubwa inafanyika ya kuona namna gani tuweke ushirika wetu katika ngazi ya ufanisi mzuri ili tufaidike na hii dhima nzima ya ushirika ambayo watu wengine duniani wanaifaidika nayo. Sisi Tanzania tukiwa mmoja wa hao waliopo katika dunia hii

nasi tuweze kufaidika kwa sababu katika kiwango tulichonacho sisi ni wazi kwamba ushirika ndiyo njia mojawapo ambayo tunaweza kuunganisha fedha zetu ndogo, tukapata mtaji wa kutosha kufanyia kazi ambayo inaweza ikatuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika hilo ni lazima nimshukuru sasa Waziri mwenyewe kwa kuwasilisha hotuba hii vizuri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wote na watendaji wote katika Wizara. Nina imani wameshiriki kwa karibu kabisa katika kuandaa hotuba hii ya Wizara ya Ushirika na Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja ambacho kinajitokeza wazi na ningependa niwape pongezi na sifa Wizara ya Ushirika na Masoko ni ubunifu wa hili wazo la ku-*guarantee*, kuwawezesha wanaushirika waweze kupata fedha kwa ajili ya kushughulikia hasa ununuzi wa mazao katika maeneo yao. Hili wazo lilianza mwaka 2001. Lilianza kwa mazungumzo ya ndani na Waziri na mimi nilishiriki kwa ajili ya kuwaomba watu wa zao la Pamba kwamba Ushirika hautaweza kabisa kununua Pamba ingawaje wananchi wapo tayari kuuzia pamba yao katika ushirika. Basi katika haya tukajaribu kuzungumza pia na Waziri wa Fedha, ndipo likaanza hili jambo la kuweka dhamana yaani Serikali kuwadhamini washirika, wanunuzi hawa ili kwamba waweze kushiriki vizuri katika mazao mbalimbali likiwemo Korosho, Pamba, Kahawa na mengine mengi yaliyowekewa hiyo dhamana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba za mwaka huu za Mawaziri nimeona jambo hili limekwenda mbele zaidi, hata Wizara ya Kilimo na Chakula, imetumia mtindo huu. Kwa hiyo, hii ni sifa kwa Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa kweli nawapa pongezi sana kwa ubunifu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimoja ambacho katika hotuba ya Waziri pamoja na kwamba mimi ni mmoja katika Kamati hii ambayo imejadili Wizara hii, lakini kimoja ambacho kinaonekana wazi na nilikiona hata wakati ule tunazungumzia suala hili la Wizara ni suala la kuweka idara maalum kwa sababu ndiyo tatizo letu kubwa hapa Tanzania kuhusiana na masoko ya kuuza bidhaa zetu kokote kule. Sasa katika taratibu za Wizara kuna kitengo maalum kama ilivyoeleza hotuba hapa waziwazi kwamba hiki kitengo kinashughulikia masuala ya masoko tu na juhudi zake zimeanza kuonekana, taarifa zimetolewa wazi hapa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu mimi ningesema tu kwamba umeniridhisha na ningependa nitamke wazi kwenye Bunge lako Tukufu bila kuogopa kwamba ni utaratibu ambao ningependa ukomae na idara hii ikomazwe zaidi ili iweze kufanya kazi zake za manufaa kwa Watanzania wote na mimi mwenyewe kama mkulima wa pamba nifaidike na matokeo ya shughuli za Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina machache ambayo nataka kuyakazia, kuyakazia kwa maana ya kwamba kuyaweka yafahamike zaidi ndani ya Wizara na Wizara ione itayafanyiaje kazi mambo haya. Kwa kweli kiasi cha fedha ambacho Wizara imeomba nakiona ni kidogo kwa kazi ambazo hasa kwa Wizara kama hii ambayo ni ya msingi na ni kubwa kiasi hiki, ambayo inatugusa Watanzania wote, kwa sababu kila eneo kuna ushirika. Ushirika hasa ndiyo lugha, ndiyo hasa msimamo na ndiyo hasa njia pekee ya kutukomboza sisi Watanzania wenye uwezo mdogo. Sasa katika pesa hizo mambo ambayo nataka kuwaomba wayakazie kwa karibu, sijui lakini wataona wenyewe huko au mwaka kesho waone watafanyaje ili waeleze Serikali iweze kuwaongezea kidogo mgao ili waweze kutekeleza mambo ya msingi kama haya.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kwamba pamoja na mipango hasa kwa zao la pamba si kweli kwamba bohari hizi ambazo zipo katika maeneo yetu ya mazao zinatumiwa kwa kupikiwa gongo. Bohari hizi kwa utaratibu wa sasa ndiko mahali ambapo wanunuzi wote wanakutania. Zinatumiwa vizuri sana kwenye eneo la zao la pamba. Sasa sijui kule kwingine sijaangalia na kutafiti kwa karibu lakini kwa wakulima wa Pamba kwenye bohari au magodauni yaliyokuwa mali ya Vyama vya Ushirika ambavyo bado vipo mpaka sasa, havijapotea sana, ndiko mahali ambapo kwenye huu utaratibu wa masoko wanakutania pale wote kununua na kuuza Pamba. Wanunuzi wanakusanyika pale ili kwamba anayeza awaone wanunuzi pale, wakatane nao pale.

Sasa hizi bohari labda tu kitu ambacho kingeweza kuelezwa hapa na kueleweka ni kwamba ziboreshwe zaidi ili kwamba taratibu hizi na ununuzi mzima wa zao la Pamba na mazao mengine zifanyikie hapo. Kwa maana kwamba hawa wanunuzi wasiende kuwafuata wakulima mmoja mmoja pembeni kule,

pawe ndiyo mahali pao pa kukutania na kuweza kuuza Pamba, Kahawa, Korosho au Tumbaku kwa uwazi na kwa masoko ambayo yanaweza yakakidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ningetaka kukikazia ni kuiomba Wizara isimamie kwa ukaribu sana suala la ukaguzi kwa sababu mimi naona ndiyo lilikuwa moja ya matatizo makubwa ambayo yamesababisha kukwama kwa ushirika. Ukaguzi usimamiwe kwa karibu sana na Wizara, Idara ya COASCO nafahamu ina matatizo ndiyo maana nimezungumzia suala la pesa kama kuna uwezekano Wizara iongeze pesa COASCO ili kusibaki Vyama ambavyo havijakaguliwa hata kimoja na ukaguzi uweze kufanyika mara tatu au nne kwenye msimu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo njia pekee ya kuweka macho yetu kwenye shughuli hizi nzima za ushirika ili kama kuna ubadhirifu, kuna mpango ambao unafanywa kinyume na watumishi katika maeneo hayo basi ufahamike mara moja na mapema kuliko kusubiri miaka miwili au mitatu hamjamwona huyu mtu. Hii ndiyo inasababisha hata kesi zingine zinakuwa ngumu kupeleleza. Unakuta ushahidi mwingine umepotea, huyu mtu aliyeiba naye ameandaa mambo yake.

Kwa hiyo, ukaguzi kama majukumu ya Wizara yanavyosema sasa jukumu la kusimamia kwa ukaribu mwenendo wa Vyama vya Ushirika ningeshauri kwa nguvu zangu zote kwamba ukaguzi ufanywe vizuri na wa kutosha kwenye msimu mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa niombe Wizara iangalie kwa karibu ni suala la utafiti. Kuna maamuzi mengi tunayafanya maamuzi ambayo yanatuhusu wakati mwingine hata kujaribu labda kutoa maoni au kutaka kubadili utaratibu mzima wa chombo cha Ushirika haya maamuzi nimegundua mengi yanafikiwa bila takwimu na taarifa ya kutosha.

Kwa hiyo, hapakuwa na utafiti wa kutosha kwenye kutufikisha kwenye maamuzi yale. Kwa mfano, maamuzi yaliyofanywa na Serikali mwaka 1968, mwaka 1976 na mwaka 1984 kuhusiana na Vyama vya Ushirika nina mashaka kama yalikuwa na utafiti wa kutosha. Kwa sababu ukifuatilia haya sasa ndiyo unakuta yamezorotesha ushirika na kuufikisha hapo ulipofikia, jambo ambalo naliona siyo zuri.

Sasa Wizara hii imekabidhiwa jukumu hili zima, ningeomba na niombe kwa karibu kama majukumu yake yanavyoeleza lazima isimamie utafiti na ifanye utafiti wa kutosha. Kama kuna jambo linatakiwa kufanyiwa maamuzi basi liwe limekamilika na limetafitiwa vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, ningeomba Wizara ibaki kwenye majukumu yake tu isiende nje ya hapo. Kwa mfano, Ushirika wowote ule lazima wanaouunda wakubaliane kwanza, wapeane masharti mazuri ya Ushirika, pawe na hisa na kura moja, pawe na utaratibu mzima wa kulipa ada, kwa hiyo, ushirika wa msingi hata kama ni wa Chama cha Ushirika basi unakuwa ni mali ya watu waliouunda. Serikali inabakia pale kuweka mazingira mazuri, kusimamia na kuwasaidia hawa. Si vizuri kwa Serikali kuingia kufanya maamuzi ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, hilo jambo mimi naiomba sana Serikali na Wizara ili iangalie kwa makini na kwa ukaribu, ikae mbali kujiingiza kwenye maamuzi ya Vyama vya Ushirika la sivyoo wanachama watakuwa waoga. Wataona kwamba kumbe Chama chetu tunapokiunda siyo chetu Serikali ndiyo yenye madaraka. Kwa hiyo, wanashindwa kufanya mambo yao na maamuzi yao wao kwa sababu ya Serikali kuingia kwenye utaratibu mzima huu. Kwa hiyo, hili naiomba Wizara isimamie na ikubali kabisa kama maoni yalivyotoka na mapendekezo na hali kamili ya majukumu ya Wizara ibaki ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kikubwa na cha mwisho ambacho ningeomba niombe Wizara ikifanye kwa makini ni elimu ya ushirika kwa njia zozote zile. Kuna hii inayojitokeza kwa njia ya redio, lakini vipeperushi, maandishi mbalimbali, taarifa mbalimbali zipeleke kwa wanaushirika ili waelewe wajue kwamba hapa ndipo kwenye Ushirika.

Sisi tunaweza kufanya A, B, C, na D, Serikali kama ina cha kufanya ndani ya ushirika ni kimoja, mbili, tatu, vijulikane. Kwa sababu elimu hii sasa inatakiwa tena tuirudie, tulikuwa tumeshaikamilisha miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1960 na 1970 tulikuwa na Ushirika wenye nguvu hapa, watu walikuwa wamepata mwamko mzuri na wa kutosha. Kwa hiyo, sasa inabidi turudi nyuma tena kufanya jukumu hili na kazi hii kwa karibu na kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mambo haya nimeona niyasema au niyarudie tu makusudi ili kukazia ili Wizara yetu iweze kufanya kazi zake na tuweze tena kuwa na ushirika wenye nguvu ambao unafahamika na unatambulika kiulimwengu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na maoni ambayo yametolewa na Kamati kwa kweli nakubaliana kabisa na suala la Benki. Suala ambalo ni moja ya matatizo makubwa ambayo sasa yangukuwa yameshatatuliwa.

Pia suala la utaratibu mzima wa kuanzisha Vyama vya Ushirika kama nilivyosema na mambo mengine mengi kuhusiana na usimamizi huu katika Vyama vya Ushirika yazingatiwe kwa karibu kwani yatatusaidia sana kutatua hili tatizo na kurudisha ushirika wetu ili uwe na nguvu na wa kusikika kama ulivyokuwa katika miaka ya sitini na sabini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana. Pia namshukuru Waziri wa Ushirika na Masoko, nimwombe tu awe na bidii asirudi nyuma. Kwa kweli picha inaanza kuonekana kwamba tunakwenda wapi.

Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi kuhubiri Ushirika katika maeneo yetu hasa watu wa maeneo ya kilimo cha Pamba, Kahawa, Tumbaku na Korosho, tusirudi nyuma tumsaidie Waziri kwa sababu tukishafanya hilo Ushirika ukisimama tu hali itakuwa tofauti na tatizo letu la umaskini tutakuwa tumelifanyia kazi kwa karibu na kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja na niitakie Wizara ya Ushirika na Masoko, mema kwa mwaka wa 2003/04. *(Makofi)*

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada ambazo anazifanya kuweza kusaidia kufufua Ushirika ambao sasa hivi ulikuwa unatetereka katika hali mbaya zaidi. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara mbalimbali katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Ushirika na Masoko, imeanza hivi karibuni inawezekana kwa kweli ikafanya vizuri au ikafanya makosa madogo madogo. Kwangu mimi naona suala la Ushirika ndicho chombo pekee ambacho kinaweza kusaidia na kuchangia kumwinua mwananchi wa kawaida mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya hali ya wakati huu tunachanganya mambo mawili. Ushirika baada ya sheria hii ya soko huru kuingia hapa nchini basi ushirika umekuwa ukirudi nyuma. Hali yake imekuwa duni sana na hii nafasi inachukuliwa na makampuni binafsi ambayo yana mamlaka makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muundo wa Vyama vya Ushirika ni chombo cha pamoja ambacho kinasaidia nguvu kwa pamoja na kila jambo ambalo linatakiwa kutendwa lazima kuwe na mkutano wa kuweza kuamua kitu ambacho kinatakiwa kifanyike, hicho ambacho kimefanya ushirika uweze kuzorota katika pambano hili la ushirika na soko huru.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo nataka niliseme Wizara hii inakwenda pole pole mno. Inakwenda pole pole mno kwa sababu kulikuwa na mambo ya kufanya haraka ili kuweza kuyafanyia kazi katika kipindi hiki cha 2000 hadi 2005.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumechelewa mno hata hii sheria inayokuja itakuwa imechukua nafasi ya miaka miwili tu kuifanyia kazi, kwa sababu kama italetwa mwezi Oktoba, Novemba, halafu ije ipitishwe nadhani mwaka utakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Spika, mpaka ije kuanza kufanya kazi inachukua miaka miwili, uchaguzi unaingia na suala la uchaguzi likiingia mambo ya Ushirika kama yameshavurugika itakuwa ni *political issue* kwa maeneo fulani fulani kama vile Shinyanga, Mwanza na Mara ambako suala la Ushirika ni muhimu sana. Kwa hiyo, tunapokwenda pole pole inatupeleka pabaya.

Mimi nilikuwa naomba kwamba Serikali iweke umuhimu wa pekee wa kuweza kuharakisha mambo ambayo ni muhimu yafanyiwe kazi mapema ili jambo liweze kutendeka vizuri. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali kwa suala hili imelichelewesha, lakini ifanye jitihada ya kuweza kulifanyia kazi vizuri na mapema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie tena kwa upande wa Ushirika ni suala la ukaguzi. Kama mambo yanavyokwenda sasa hivi Vyama vya Msingi, Vyama Vikuu vya Ushirika vinatakiwa viwe vinakaguliwa mara kwa mara na sheria ya Ushirika inasema lazima ukaguzi hufanyike mara moja kwa mwaka. Lakini bahati mbaya tena wataalam wa Vyama vya Ushirika hasa hawa *Co-operative Inspectors* sasa hivi ni wachache mno. Unachukua mtu mmoja akakague Vyama vya Ushirika 40 vya Msingi kwa mwaka, mara nyingi huyo mtu atalipua hawezi kufanyakazi vizuri kwa sababu ni Vyama Vingi vya Ushirika ambavyo vinatakiwa vifanyiwe ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, wakaguzi hawana elimu ya kutosha, tatizo ambalo Serikali ingejipa muda wa kuweza kuwapeleka hawa wanaoendesha Ushirika ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa kwenye mafunzo ambapo wangeweza wakahimili ushindani uliopo wa sasa wa Ushirika na soko huria. Vinginevyo watakuwa wanaimba tu au tutakuwa tunasema tu Ushirika, lakini hakuna lolote litakalotendeka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa nafasi ya ukaguzi iweze kuichukulia hatua inayostahili. Kwa wale ambao wanafanya wizi, udokozi, wachukuliwe hatua kali. Kwa sababu sasa hivi wananchi na wakulima kwa ujumla wamekata tamaa, mali zao zinachukuliwa hivi hivi na wale viongozi ambao wanaendesha Ushirika wala hawachukuliwi hatua yoyote. Sasa inakuwa ni vigumu kurudisha imani hiyo kwa wanaushirika kama wanaona hali hiyo wala haichukuliwi hatua yoyote. Kwa hiyo, naishauri Serikali jukumu la kuimarisha ukaguzi ni muhimu sana na mara inapoonekana kwamba kuna kasoro basi sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa nizungumzie suala la masoko ya mazao. Kuhusu masoko tumekuwa na tatizo, mkulima kama anafanya jitihada za nguvu kwa kutumia jembe lake au nguvu yake hatma yake anakuja kupata kiasi kidogo sana kuliko kiasi alichotumia inamkatisha tamaa. Kuhusu hili kwa sababu Wizara yenyewe ndiyo yenye jukumu la kuangalia masoko ifanye jitihada na kuangalia masoko kwa mazao ambayo yanatokana na nguvu za mkulima huyu mdogo mdogo kama kweli yanaleta faida au kama ni hasara jukumu la kuchukua hatua haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi soko la dunia linaendelea kila mwezi na tuna mitandao tu ya kuangalia. Kwa sababu soko la dunia liko sehemu moja tu siyo kwamba lipo katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, ni kiasi cha kuangalia kwamba soko kwa zao fulani bei yake ni kiasi gani na kuona, basi taarifa zitolewe kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, suala la Pamba mwaka huu tumeingia msimu wa 2003/2004 hatujatangaziwa na baadaye kutangaza kwamba bei ya kuanzia ni shilingi 225/=, walioanza kununua Pamba walianza na shilingi 255/= na wengine wamefikia mpaka shilingi 300/= na wengine shilingi 350/=. Sasa inamtia wasiwasi mkulima anajaribu kuangalia sasa Serikali inatamka nini? Serikali imetamka bei ya chini sana, wale wanunuzi wameenda juu mpaka shilingi 350/=.



Kwa hiyo, hapa kuna maana ya kwamba Serikali labda inashirikiana na wale wanaonunua mazao yao, kiasi kwamba inawezekana wanapunja au kuna mambo ambayo yanafanyika bila kuwasaidia wakulima. Suala hili kwa kweli lazima liangaliwe, kwa sababu Serikali ina ngazi zote za kuangalia mtandao wa masoko kwa mazao ya mkulima, lazima iangalie mapema na kutoa tahadhari. Inawezekana iwe inatolewa taarifa ya kila mwezi kwa sababu soko linaweza likabadilika, basi wananchi wataarifiwe kwamba kuna hali hii, kwa hiyo, wachukue tahadhari kuliko kuacha giza bila ya utaratibu wa kuwajulisha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni *STABEX*. Mfuko huu kwa kweli mimi naona kama una ubaguzi baguzi, Serikali lazima iwe wazi. Kama mazao yaliyotajwa ni Kahawa, Chai, lakini Pamba haikutajwa, kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alivyojibu jana, alisema waziwazi kwamba suala la Pamba halipo katika Mfuko huu. Mimi nasema kama ni suala la mazao ya nchi lazima yawe pamoja. Kama tunatoa upendeleo kwenye sehemu fulani, sehemu zingine tusiwape ina maana kwamba hapa tunaangaliana kwamba sehemu fulani tuwape msaada na sehemu fulani tusiwape msaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Pamba ni muhimu sana na zao hili ni kubwa mno na kama halipewi Mfuko huu ina maana kwamba basi Serikali haioni umuhimu wa zao hili.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba tusionyeshe upendeleo wa aina hiyo na tamko hilo lipo kwenye *Hansard*, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, alisema waziwazi, vinginevyo labda aje afute usemi huo. Lakini ilibainika kabisa kwamba Kahawa ndiyo inayoshughulikiwa zaidi. Sasa tunachukulia kwamba labda kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula anatoka kwenye maeneo hayo ya Kahawa inawezekana amependelea kwa upande wake. Kwa upande wa zao la Pamba ambako sisi tunatoka halikutajwa.

Kwa hiyo, nasema Mfuko huu wa *STABEX* lazima utasaidia masuala ya kujenga barabara na kuimarisha maeneo na kuwasaidia wakulima. Lakini kama linafanyika kwa sehemu moja kwa kweli hili halijengi uhusiano mzuri na linatia dosari katika utendaji wa Serikali. Kuhusu suala hili, mimi naiomba Serikali tuone utendaji unakuwa wa pamoja, kama Mfuko huu unatumika kwenye zao la Kahawa basi vile vile na zao la Pamba, Korosho, Chai, Tumbaku lazima mazao haya nayo yapate msaada wa Mfuko huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa sababu Ushirika umekuwa wa muda mrefu lakini hauna benki ya Ushirika. Suala hili lisipotiliwa mkazo Vyama vya Ushirika vitayumba. Mara kwa mara tunakuwa tunategemea mabenki, kila tukitaka kuanza shughuli za ununuzi wa mazao, inakuwa kwanza tuwaone watu wa mabenki na wao wanatoa riba kubwa kiasi kwamba kuendesha shughuli hizo inakuwa ni vigumu sana.

Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali kwamba hakuna budi tufanye jitihada za kuweka Benki ya Vyama vya Ushirika ili viweze kujiendesha vyenyewe. Bila hivyo kwa kweli tutakuwa tunasema Ushirika uimarishwe, kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema ya mwaka 2000 kwamba Serikali itahakikisha Vyama vya Ushirika vinaimarishwa na kuboreshwa. Hilo tamko linakwenda kinyume sasa hivi kwa sababu hatujaimarisha wala hatujaviboresha Vyama vya Ushirika. Lakini tukiwa na Benki ya Vyama vya Ushirika ambayo itakuwa inasimamia masuala yote ya mazao haya ambayo yanalimwa na wanaushirika itasaidia kuweza kuimarisha na kuboresha Ushirika na masoko ya mazao. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, nazidi kuwapongeza na naomba kwamba Ushirika uimarishwe, ndiyo ambao una *impact* kubwa sana kwa kupambana na umaskini hapa nchini. Kwa hiyo, naomba suala hili lizingatiwe na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, ndiyo muasisi wa Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, naomba kabisa kwa nguvu zote afanye jitihada ili ukombozi huu wa Vyama vya Ushirika uimarishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nikushukuru sana kwa kuniruhusu nizungumze na nichangie katika hoja hii. Lakini kabla sijatoa mchango wangu ningependa

kwanza kabisa niwape pole Mheshimiwa Waziri *Sir* George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kufiwa na mtoto wao mpendwa na naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa niseme wazi kwamba naunga mkono hoja hii. Ni hoja nzuri na imeonyesha wazi baada ya kuundwa Wizara hii, kazi inayoendelea ni kazi nzuri kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuchangia maoni na kutoa ushauri katika masuala ya Ushirika na mara nyingi napenda kufanya hivyo, ni kwa sababu inahusu watu walio wengi hapa nchini ambao ni wakulima na watu ninaowawakilisha mimi katika Jimbo langu la Kalenga, walio wengi kabisa ni wakulima na wenye kipato kidogo na ambao wanahitaji Ushirika kama mbinu ya msingi ya kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napata faraja kuona kwamba Chama chetu Tawala, Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi, kinasema kama ifuatavyo: “Kwamba Chama cha Mapinduzi kinatambua kuwa Ushirika ndicho chombo cha uhakika cha ukombozi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo na pia wachimba madini wadogo wadogo. Ushirika wa Kuweka na Kukopa uliwekewa mkazo kwa sababu ndicho chombo muafaka katika kutatua matatizo ya maendeleo ya wanachama wake ambao ni wakulima. Kwa mfano, upatikanaji wa pembejeo na mikopo.”

Kwa hiyo, huu ni muundo ulio na uhakika kwa wakulima na wafugaji unaoweza kukusanya nguvu zao na kuwawezesha kupata mikopo, na vilevile kuwa ndicho chombo kinachoweza kikawatafutia bei nzuri wakulima kwa ajili ya mazao yao. Kwa hiyo, kama ambavyo nimesema huko nyuma Vyama vya Ushirika kwa wakulima ni Makampuni yao, ni *Cartels* zinazofanywa wawe na nguvu kuweza kupambana na wale wanaofanya biashara ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kumetolewa maoni hapa na upande wa Kambi ya Upinzani kwamba ni vyema Wizara hii ifutwe na iwe Idara katika Wizara ya Kilimo na Chakula. Ndiyo maana nime-*quote* msimamo wa Chama cha Mapinduzi ambacho ni Chama Tawala ni kwamba huko kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula, tumeshaondoka, haturudi huko nyuma. Wizara ya Ushirika na Masoko ni chombo kinachowakilisha *Organization* ya watu walio wengi katika nchi hii. Sasa inakuwaje tena unairudisha kuwa Idara na kazi hii iliishafanywa na Tume ya Rais chini ya Mheshimiwa *Sir* George Kahama na kuonekana wazi kabisa kwamba tunahitaji Wizara ya Ushirika na Masoko. Kwa hiyo, ningependa sana isije ikafika huko juu ikaonekana kwamba kuna hoja hapa tena ya kurudi huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huko nyuma Vyama vingi vya Ushirika vilipoteza uhai wake kwa matatizo ambayo yalikuwa nje ya uwezo wa wanachama au wakulima. Vyama hivi vinahitaji nguvu mpya ili viweze kufufuka na hili tatizo liko sana katika Wilaya ya Iringa na Jimbo langu la Kalenga ni kwamba, ili tupate Vyama vya Msingi na viweze kuwa na nguvu kwa kiwango kwamba sasa vinageuka vile vile kuwa Vyama vya Kuweka na Kukopa itabidi Serikali ambayo huko nyuma nayo ilichangia katika hali ya kuweka mambo yakawa si mema kwa Vyama vya Ushirika inalazimika na ina wajibu kufanya wajibu wake wa kisheria kuvilea Vyama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu mimi kwa Jimbo la Kalenga na Wilaya ya Iringa kwa ujumla, inabidi Vyama hivi vya Ushirika vipate mikopo kutoka Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Lazima hili jambo lifanyike safari hii, la sivyo itaonekana tunawafanyia mzaha wakulima kwamba tunawaambia waingie katika Vyama vya Ushirika, halafu hawapati mikopo. Isije tena ikatokea tukawaacha kuwa *at the mass of the Exim Bank.*

Mheshimiwa Spika, safari hii namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba ahakikishe Vyama hivi vinapata mikopo na ningependa katika kauli yake anapo-*wind up* kuhusu suala hili atamke kwamba Vyama hivi vitapata mikopo, ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika vya Jimbo la Iringa. Italeta faraja kubwa sana na itawafanya wengi wajiunge katika Vyama vya Ushirika kwa kule kusikia tu kwamba tutapata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa vilevile niseme kwamba ili kuwapa mikopo tusiogope kuwa pengine mikopo hiyo haitarudishwa, na pengine tena Vyama vya Ushirika vinaweza vikafa kwa hiyo ikawa ni hasara kubwa kwa Serikali. Kuna Mwandishi mmoja Mmerakani anaitwa Briant Trafy, ambaye anaitwa kuwa ni *American's leading business authority on success*, yeye anaeleza juu ya *overcoming failure* maana huko nyuma tumeshindwa. Sasa *overcome failure* anasema hivi: *"It is not failure itself that holds you back, it is the fear of failure that paralyzes you. Failure is a pre-requisite for great success."*

Kwa hiyo, kwa vile tumewahi kupata matatizo katika Vyama vya Ushirika na tukaelewa uchungu wake lazima huo utakuwa ni msingi mzuri wa kujenga Vyama vya Ushirika vilivyo bora na ambavyo vinaweza vikamkomboa mkulima kiuchumi akawa anaendesha maisha yake yaliyo mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba vilevile mara nyingi tunasita kuwapa mikopo wakulima. Serikali isiwe inaogopa kutoa mikopo kwa wakulima maana tumeishapata mifano safi. Mfuko wa *TASAF* fedha zimekuwa zinapelekwa vijijini na miradi mingi ya *TASAF* imefanikiwa. Mpango wa *MMEM* vilevile tumepeleka fedha nyingi sana vijijini na tumejenga madarasa mengi sana nchini Tanzania. Sasa hili la mikopo kwa nini linakuwa ngumu sana. Naomba sana kuwe na tamko hilo, na nina uhakika kwamba hilo litaleta maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa niseme kwamba hata kama tutapata hasara juu ya mikopo ambayo wanapewa wakulima. Lakini kama watakuwa wamepewa mikopo wakanunua pembejeo, faida tutakayoipata kutoka kwenye kilimo chenyewe itakuwa ni kubwa sana, hata hii mikopo itakuwa haina umuhimu sana hata kama wasipoirejeshe yote kuliko kutotoa mikopo halafu tunakuwa hatuna kilimo bora. Kwa hiyo, uchumi wa nchi unazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kusema kwamba katika urejeshaji wa mikopo ni suala tu la kuweka utaratibu mzuri. Kwa mfano, utaratibu wa masoko ulio wa kisheria kwamba wananchi wanauzaje mazao yao kwa kutumia Vyama vyao vya Ushirika.

Kwa hiyo, kila kijiji kiwe na soko au mnada ambapo inawanyima wale wafanyabiashara wanaokwenda majumbani na kuwaghilibu wakulima na kununua mazao kwa bei ya chini sana. Lakini ikiwa kwenye soko bei inakuwa nzuri, wakulima wanakuwa ni wengi pale. Vile vile inawezekana kurejesha mikopo au kwamba wao wenyewe wapewe mikopo ya mabenki ili wayanunue mazao na kuyauza. Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameeleza kwamba mikopo ile ambayo ilitolewa kwa ajili ya kununulia mazao imerudishwa. Kwa hiyo, huu ni msingi kwamba wakulima wako *very responsible*.

Mheshimiwa Spika, kama tungekuwa na Vyama vya Ushirika ambavyo vinafanya kazi nzuri kwa mfano kwa Mikoa minne ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa ilipotokea njaa kubwa Zimbabwe, Zambia, Malawi na sehemu nyingine Vyama vya Ushirika vingeweza kuwa vinapeleka mazao ya chakula kama mahindi na kadhalika huko Zimbabwe na vingepata fedha nyingi sana. Lakini walionufaika siyo wakulima, wamenufaika wale wengine ambao wanakuja katikati ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningeshauri kwamba ili kuendesha Vyama vya Ushirika ili tuweze kupata Vyama vya Ushirika vingi na vilivyo bora inatakiwa kuwawezesha Maafisa Ushirika walioko kule Wilayani waweze kuwa wanazunguka na kuonana na wakulima. Lakini wako chini ya Halmashauri za Wilaya na hawapati *OC* yoyote toka Wizarani ambayo itawafanya waweze kuzunguka huko na kuonana na wakulima. Wanategemea mpaka wapewe na Halmashauri, sasa kila Halmashauri ina *priorities* zake, inaweza ikaona kwamba suala la Ushirika siyo muhimu sana.

Kwa hiyo, ni vyema kuwe na utaratibu wa kama *MMEM* ambapo fedha zinaenda kule Wilayani, lakini Afisa Elimu ndiye *sanction* wa hizi fedha kwenda vijijini pamoja na kwamba Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya ndiye *Accounting Officer*.

Kwa hiyo, huyu Afisa Ushirika awe ni *Warrant Holder* pale Wilayani, fedha za kuendesha mambo ya Ushirika ziwe kwenye makadirio haya ya Wizarani ambayo tunayapitisha. Halafu zipelekwe kule

Wilayani na yule Afisa Ushirika wa Wilaya aweze kuzunguka ipasavyo na kuweza kuwashauri wakulima na kutatua matatizo ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba yale ambayo nilitaka kuyazungumza naona nimeyazungumza na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri amenielewa. Vinginevyo namtakia kila la kheri na Wizara nzima naitakia kila kheri wafanye kazi njema ila tupate mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa na mimi natoa pole kwa Mheshimiwa Waziri Sir George Kahama, pamoja na familia yake kwa yote yaliyowapata.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka nitumie nafasi hii kutoa wito kwa Wanaushirika walio vijijini ambao watahitaji umeme ambao hautumii waya waweze kujiorodhesha ili tuweze kuwasaidia na hili siyo la Chama. Hili siyo jambo la Chama, ni jambo la Kitaifa, siyo la Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua kusema hivyo maana hapa kwenye *Hansard* inaonyesha tumesema kwamba hakuna umeme usiotumia waya. Sasa umeme wa *solar* huwezi ukaufunga waya kwenye anga ukauleta hapa. Sasa nimelisema hapa kwamba upo na unakuja na pale *Kibosho Mission* wanatumia umeme huo kwa ajili ya kupikia na kwa ajili ya kufulia nguo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme sasa kuhusu Ushirika. Matatizo makubwa yanayowapata Wanaushirika ni kuhusu viongozi ambao wamewachagua wenyewe. Lakini baada ya kuwachagua viongozi wamehodhi madaraka, wamefanya sasa kile Chama cha Ushirika kama ni mali yao, kwa hiyo, wamekaa nacho hawataki tena kuwajua wale waliowachagua na wanatumia zile mali za Chama cha Ushirika kama mali zao.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumelipigia kelele kweli kweli, toka nimeingia Bungeni hapa, Mheshimiwa Waziri anajua hata tukiangalia kwenye *Hansard* kwamba kuna viongozi wamekaa zaidi ya vipindi viwili isivyo kawaida na hakuna utaratibu uliochukuliwa wa kuweza kumbana huyu na kwa kuwa anakuwa amechukua mali nyingi za wananchi na hawezi kuzirudisha anatumia kila njia, anakuwa na uhusiano na Afisa Ushirika ili asiweze kuitisha uchaguzi ili wachaguliwe wengine. Hilo limetokea kule kwangu na niliwahi kuondoka na Afisa mmoja wa Ushirika anaitwa Omari, nikaenda naye kwenye Mkutano katika Shamba moja la Shagiti, wananchi walitaka kumpiga huyo Omari, nikamkingia kifua, nikasema hapana, Mheshimiwa Waziri, yupo nitaenda kumwona na atatatia hili jambo.

Kwa hiyo, wanachodai ni kwamba Wizara inawalinda viongozi waovu na wanapata chochote kutoka kwa viongozi wa Ushirika ambao wamekaa kwa muda mrefu ili wazidi kuendelea kukaa madarakani.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana jambo hilo. Kwa sababu ni kero kubwa na linatia aibu Ushirika ambao kwa sasa hivi tunafikiri labda ndiyo ukombozi wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wizi unatokea katika Vyama vya Ushirika ambazo ni fedha za wananchi, unatokana na kutokukaguliwa na unatokana na kutofuatiwa kwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa namsikiliza Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika kipindi kimoja redioni, anasema kwamba kama mtoto akishika moto anaugua hapo hapo, ukianguka unaumia hapo hapo.

Sasa kama Ushirika hauwezi kufuatiwa kwa karibu kwani yule anayechaguliwa anachukua dhamana ya fedha za wananchi na anakuwa nazo, kama hatuwezi kumkagua mara kwa mara na kumwadabisha hakuna hata siku moja Ushirika utaendelea na wananchi wataendelea kuudharau Ushirika.

Wakati jambo lenyewe kama likiwekwa vizuri ni jambo la maana sana. Bila Ushirika hatuwezi kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *Procurement Act, 2001* Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 sijui hiyo sheria ya fedha ni kwenye Wizara ya Fedha peke yake au na kwenye Wizara zingine.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo sheria imetungwa toka mwaka 2001, kama Wanaushirika wangukuwa wanafuatilia hiyo sheria, leo hii mimi nisingekuwa hapa napiga kelele ninayopiga sasa hivi. Kwa hiyo, ningepomba kwamba hiyo sheria ifuatiliwe ili iweze kuwa *imposed* katika Vyama vya Ushirika na ili waweze kuadabishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa uchungu kwa sababu katika Jimbo langu nilikwenda sehemu za Uru iitwayo Kyaseni, nikamkuta karani wa Ushirika kwa miaka saba hajaitisha mkutano wa Wanaushirika na ameua treka la Ushirika na ameua lori moja aina ya *Leyland* na hilo lori ameliuma kwa shilingi milioni moja na treka akaliua kwa shilingi milioni tatu na hizo fedha mbele ya Afisa Ushirika na mimi nikiwepo akatoa maelezo kwamba nimelipia watoto wangu shule, watoto wangu walikuwa wanataka kusoma.

Kwa hiyo, samahani ndugu wajumbe, naomba samahani nimelipia watoto wangu shule, naomba nitazilipa hizi fedha, *after seven years*. Anaomba radhi kwetu sisi viongozi tuliokuwa pale.

Mimi nikamwambia Afisa Ushirika ni vizuri akasema ana mali gani tuka-*attach* sasa hivi, kwa sababu nilisikia aibu. Kwa hiyo, mambo haya nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kuwa yapo yanatia aibu. Lile lori kwanza limeuzwa kwa shilingi milioni moja tu *Leyland*. Halafu treka shilingi milioni 3.2 jumla ni shilingi milioni 4.2. Zile fedha amezichukua, yeye mwenyewe vile vile kama karani amekula na amesema nimetumia. Lakini ukiangalia wanaotia saina sio yeye peke yake aliyekubali kula.

Kwa hiyo, ina maana walishirikiana wakala zile fedha. Lakini akajitoa yeye mwenyewe akasema naomba jamani mnidai mimi nitalipa. Kwa hiyo, naomba liangaliwe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kelele nyingine ambayo kwa kweli ningepomba iangaliwe ni fedha za wakulima ambazo toka mwaka 1988 wameua mazao yao, fedha zimechukuliwa na Wizara kwa maana ya *Tanzania Coffee Board (TCB)* nikitoa mfano wa Kahawa. Bodi hiyo imechukua fedha hizo imehodhi, nimekuja hapa mwaka 2001 nimetumwa na wananchi kuja kufuatilia hizo fedha, Waziri akasema subiri katika Bajeti ijayo tutakujibu. Tumeita kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi, mbele ya Mwenyekiti Mheshimiwa Njelu Kasaka na nikaitoa hiyo hoja tena mwaka 2002 na Waziri akiwepo na wahuika wakiwepo wote na wakakiri kwamba hizo fedha atazilipa.

Katika ripoti namba 2 ya Bunge Kamati hiyo inasema kwamba: “Tunataka mwaka 2003/2004 tuisikie tena matatizo hayo.” Ilipokwisha miezi sita nilimkumbusha Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Njelu Kasaka, alichukua kalamu yake akaandika barua kumkumbusha Waziri ni vipi utekelezaji wa makubaliano ya fedha za *KNCU*.

Mheshimiwa Spika, alichojibu Waziri mimi sifahamu, lakini nimekuta katika ripoti mwaka huu 2003. Iko ripoti inasema kwamba Waziri alikwenda kujibu kwenye Kamati ya Biashara kwamba ametuua wasimamizi wa nje *auditor* ili waweze kukagua vizuri hayo mahesabu.

Mheshimiwa Spika, mahesabu ya mwaka 1988 yanateuliwa Mkaguzi leo mwaka 2003. Huyu mkulima atakuwaje na imani na Wizara hii na Serikali hii kwamba kweli inamtendea haki kwa uchungu ambao fedha yake imekaa hapati ruzuku kutoka Serikalini yaani *STABEX* aliyozoea, fedha yake hapati zinaliwa. Akidai vile vile katika ma-*document* anapewa sababu tu kwa miaka nenda rudi. Mimi nataka kusema jamani, hili ni la ubabe.

Mimi nafikiri fedha Serikali inayo nyingi sana. Hata hizi za fedha za *STABEX* tungegawa hapo shilingi milioni 426 wanazodai ukawapa ni nini, si watulua bwana? *What is the problem?* Tatizo ni nini? Kama fedha ingekuwa haipo Serikalini tugesema labda tunatafuta. Lakini kwa nini huyu mwananchi

ambaye hajui hata mahesabu umbane tu, umbane tu na wakati wakituma hata wawakilishi akina Ngawaiya, wanakuja huku. Lakini bado wanasema subiri.

Mheshimiwa Spika, wengine wako hapo nje wamesema leo hii tunataka tusikie unatoa shilingi au Waziri aseme kuhusu fedha yetu au kama kanuni zinaruhusu usiondoke huko Bungeni bila ya kuchukua fedha yetu.

Sasa ukweli kanuni haziruhusu, nilitoa rai kwamba Wizara hii ingestahili ikaunganishwa kwenye Kilimo. Kwa sababu nimeona kwamba hakuna anayemjua baba bila ya mwana na hakuna anayemjua mwana bila baba. Kwa hiyo, kilimo ndicho chenye uchungu wa kulima na ndio kitakuwa na uchungu wa kuuza.

Kwa hiyo, nimesoma mahali leo katika ukurasa wa 43. Programu ya Kuendeleza Mfumo wa Masoko na Kilimo (*Agriculture Marketing System Development Programme*). Inasema kwamba programu hii inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Basi kama hamtaki kuweka kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula, basi rudisha kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii programu ina shilingi bilioni 40 inaonyesha hapa. Kuna USD 37.92 ambazo kwa *exchange rate* ya leo ni shilingi bilioni 40. Kwa nini mapesa hayo yasimamiwe na Wizara nyingine kama kweli Wizara hii inaweza ikasimama kwenye miguu yake miwili na ikafanya kazi sawa sawa?

Sasa vitu kama hivi vinanifanya mimi niamini kwamba Wizara hii bado haijaamua kusimamia kwenye miguu yake miwili, kwa hiyo, aidha inatakiwa kiwe Kitengo katika Ofisi ya Waziri Mkuu au kiwe Kitengo katika Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha, lakini nizingumzie kidogo mambo ya *STABEX*. Mambo ya *STABEX* sitaki kuzungumzia hizo za Ulaya. Lakini sisi tulipata Uhuru hapa tukasema kwamba tunajitawala. Sasa tunavyojitawala wale wazungu si wanawapa *STABEX* wale wenzao wanaolima kule? Sisi tuna mpango gani wa kuwapa *STABEX* wakulima wetu kwa fedha yetu ya hapa? Tuna mpango gani?

Mheshimiwa Spika, tumekwishaona wanafanya nini na wanapata fedha nyingi na chakula wanatulisha. Sisi kwa miaka 40 tuna mpango gani kama Watanzania wa kuweza kuweka *STABEX* yetu kwa wakulima. Tunayo Almasi, Dhahabu, *Tanzanite* tunaauza hivyo vitu tunapata fedha kwa nini *tu-subsidy* hiyo fedha ya madini iende kwa wakulima ambao tunaamini kwamba ndio kitu ambacho kinatubeba sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo yako wazi ambayo hayahitaji mahesabu wala kusoma sana. Lakini tusiwatese hawa wakulima ambao ndio wote sisi hapa tumetoka kwenye kilimo, wengine wametoka kwenye Pamba, Miwa, Kahawa, Sukari hakuna mtu ambaye hakutoka kwenye kilimo. *Tu-subsidy* hiki kilimo jamani ili tuweze kupiga hatua ya kupata maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nimalizie tu kwa kusema kwamba mikopo inayotolewa ambayo Serikali inasaidia. Kama hamuwezi kuondoa *interest rate* kwa wakulima mkafanya kama mtu aliyenunua, basi au mtu aliyekuwa na duka huyu mkulima hawezi kulipa hilo deni, tuweke mikopo inayohusu wakulima basi na kwa *interest* ya wakulima *that's all*.

Lakini usidanganye kwamba kuna mabilioni ya kukopa za nini wakati mkulima hawezi kulipa. Hamna mkulima anayeweza kulipa kwa sababu anauza kwa mwaka mara moja. Lakini *interest rate* ina-charge kila siku au kila mwezi, huyo mkulima ambaya hajavuna mahindi yake atavuna mwaka mmoja mara moja, ataweza wapi kupata fedha za kulipa hiyo fidia kama sio uongo. Kwa hiyo, Serikali iangalie mambo yaliyoko wazi kama hayo ili tukitekeleza Mheshimiwa Waziri na mimi nitaendelea kuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba majibu haya ya fedha ya *KNCU*. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri wangu, tusiseme tena hayo hapa. Nashukuru sana ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa *Sir* George Kahama.

Lakini vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa *Sir* George Kahama na familia nzima kwa kuondokewa na mtoto wao hivi karibuni. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa *Sir* George Kahama, kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yake ya Bajeti. Aidha, nimpongeze vile vile Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuiongoza Wizara hii. Lakini vile vile nitumie nafasi hii nimpongeze Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzuri wa hotuba yenyewe nashawishika mapema kutamka kuwa ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa nielekeze mchango wangu kwenye suala la ushirika. Hivi sasa wananchi wengi huko vijijini wanajiunga na Ushirika lakini kuna tatizo la uongozi. Bado uongozi imeonekana ni tatizo hasa huko vijijini, viongozi wengi wamejaa ubinafsi. Viongozi hawa wanatumia nafasi ya wanachama kutokupata elimu ya kutosha juu ya haki zao. Kwa hiyo, viongozi wanatumia nafasi hiyo ili kujinufaisha wao wenyewe badala ya kuwasaidia wanachama wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeiomba Serikali ihakikishe elimu ya Ushirika inawafikia wanachama huko vijijini ambako ndiko waliko wengi zaidi. Wanachama wakiwa na elimu ya kutosha nina hakika hawataburuzwa na viongozi hawa wenye ubinafsi na watasimama kidete kutetea ushirika wao. Kwa hiyo, naomba Serikali itumie muda mwingi kuhakikisha elimu ya Ushirika inafika kwenye ngazi za chini kabisa hasa kwenye vyama vya ushirika vya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la uongozi imeonekana kuwa viongozi walioko ngazi za chini wanashirikiana na viongozi walioko kwenye ngazi za Wilaya kuhakikisha kuwa juhudi za wanachama zinakwamisha pale wanapotaka kuwadhibiti viongozi hao. Viongozi walioko kwenye ngazi ya Wilaya usimama kidete kuwatetea viongozi kwenye vyama vya msingi, kwa hiyo, hata wanachama wanapotaka kuwadhibiti aidha kwa kuwaondoa au kuwapeleka Mahakamani, lakini viongozi walioko kwenye ngazi ya Wilaya huwakingia kifua *simply* kwa sababu kwanza wanajuana, lakini vile vile wanakula nao pamoja. Kwa hiyo, hali hii isipodhibitiwa basi nina hakika Ushirika utakufa. Wengi tumeona faida ya Ushirika kwa hiyo tusiruhusu hali hii ikaendelea, kinachotakiwa ni kuipiga vita mara moja na kuwasaidia wananchi kuimarisha Ushirika wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningie kwenye masoko hasa nikichukulia kwenye Jimbo langu la Nanyumbu. Hivi sasa kwa zao kama Korosho limeonekana kuwa linapatikana karibu kipindi chote cha mwaka. Tofauti huko nyuma ambako Korosho zilikuwa zinazaa wakati wa kiangazi peke yake. Lakini sasa hivi hata wakati wa kifuku, Korosho zinazaa kwa wingi lakini cha ajabu ni kwamba soko la Korosho au msimu wa Korosho unapatikana kwa miezi michache kuanzia miwili hadi mitatu hivyo kuwafanya wakulima kwa kipindi kile ambacho msimu haupo basi hukosa sehemu ya kuuzia korosho zao. Matokeo yake ni kwamba kwanza mwananchi huona uvivu hata wa kwenda kuokota korosho zenye. Maana anajua kuwa hata kama ataokota lakini atakwenda kuuzia wapi. Sasa matokeo yake ni kwamba wezi nao hupita mashambani na kuiba korosho za watu kwa hiyo, mwananchi hukosa mazao yake mengi. Lakini hata kwa wale wananchi ambao wanajitahidi kuokotea Korosho zao mara nyingi wanunuzi ni hao walanguzi ambao wanapita na kununua kwa bei ya chini kabisa. Kwa hiyo, hapa napo mwananchi hupoteza kipato chake kwa sababu analazimika kutupa korosho zake kwa bei ndogo zaidi. Kwa hiyo, ningeiomba soko la Korosho kwa wakati huu ambapo Korosho zimeonekana kuzaa kwa mwaka mzima basi likawa wazi kwa kipindi kirefu zaidi ili wananchi waweze kuuza Korosho zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona mwaka huu wakati wa kifuku kuna watu wengine walikuwa na magunia sio chini ya matatu ya Korosho. Sasa haya yote sana sana walikuwa wanatumia kwa kuchoma na kula wenyewe na zile ambazo zilikuwa zinabaki ndio hizo ambazo zilikuwa zinachukuliwa na walanguzi kwa bei ya chini kabisa au kwa kubadilishana na bidhaa mbalimbali ambazo hazina faida yoyote. Matokeo yake mwananchi huyu alikuwa anakosa tija na kuona pengine kuwa Korosho zilikuwa hazimletei

mabadiliko ya aina yoyote. Kwa hiyo, ningeeomba angalau msimu wa Korosho ukaongezewa muda ili kwa kipindi kirefu wananchi waweze kuuza Korosho zao, Korosho ambazo sasa hivi zimeonekana kuzaa karibu kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko vile vile nizungumzie kwenye masoko ya mazao ambayo sio ya asilia. Wananchi hivi sasa wanalima mazao mengi, lakini mazao haya yameonekana kukosa soko la uhakika. Soko ambalo linapatikana mara nyingi ni soko hili ambalo tunaita la walanguzi. Walanguzi ni watu wajanja ambao hupita kwa wananchi na kununua mazao haya kwa bei ya chini kabisa lakini huyasafirisha hadi Dar es Salaam ambako yanapata bei kubwa. Sasa utaratibu huu wa kutegemea walanguzi kununua mazao yasiyo asilia kwa kweli haufai kwa sababu haumhakikishia mkulima kupata bei nzuri na mazao haya mara nyingi yanapatikana kipindi ambacho hali ya mawasiliano inakuwa sio nzuri, kwa hiyo, mara nyingi wanaofanya biashara hii ni wafanyabiashara ambao wanayakusanya wakati ule ambapo aidha barabara hazipitiki au barabara zinapitika kwa taabu wanayahifadhi na kipindi ambacho barabara inapitika kwa urahisi uyapeleka kwenye miji mikubwa kama Mtwara, Dar es Salaam ambako wanapata bei nzuri.

Kwa hiyo, hali hii kwa kweli hatumsaidii mkulima mdogo mdogo ila ni watu wachache ambao wanatumia mwanya wa kukosa soko kwa mazao yasiyokuwa asilia ili kuwanyang'anya wananchi wetu mazao hayo kwa *almost* kwa bei ya bure.

Kwa hiyo, ningeeomba Serikali ikahakikisha kuwa masoko kwa ajili ya mazao hayo vile vile yanakuwepo na utaratibu mzuri unakuwepo wa wananchi kuuza mazao yao. Bila hivyo wananchi watafunjwa moyo, wasiweze kulima na kuvuna mazao ya kutosha kwa sababu mara nyingi mazao mengi huwa yanaharibika au yanachukuliwa kwa bei ndogo sana. Kwa hiyo, ningeeomba Wizara ya Ushirika na Masoko ifanye juu chini angalau mazao haya nayo yakapatiwa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyazungumza hayo machache na kwa vile mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mimi nisingependa kuendelea zaidi. Labda nitamke tu kuwa ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Lakini mwisho, nikushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ambayo kwa kweli sikuitegemea na ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

*(Saa 06.50 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hoja ya Waziri wa Ushirika na Masoko. Lakini kabla sijaanza mchango wangu, ningependa kwa niaba ya Wananchi wote wa Jimbo la Mwanga, tutoe rambirambi zetu kwa Mzee wetu, Mheshimiwa *Sir* George Clement Kahama, kwa kufiwa na matoto wake na tumuombe kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu basi roho yake ikae mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Sir* George Kahama, leo ametoa hotuba nzuri ambayo imetuwekea malengo mazuri na inatupa matumaini kwamba, sasa Ushirika na matatizo ya masoko ya mazao yetu yako karibu kuondoka na huu siyo mwanzo mdogo. Kwa hiyo, tunapenda tuwape pongezi sana kwa hotuba hii nzuri Mheshimiwa *Sir* George Kahama, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Wataalam wote ambao wanatuangalia hapa wakati tunatoa hotuba hii. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Jimbo langu la Mwanga wana matumaini makubwa na mwelekeo ambao umelezwa hapa leo. Vyama vyetu vya Msingi hasa vile ambavyo vimeundwa kwa ajili ya ununuzi na uhamasishaji wa kukuza Kahawa vitakuwa vimefurahia sana hotuba hii na mazungumzo ambayo tulifanya awali na Mheshimiwa Waziri kuhusu kuviwezesha Vyama hivi vya Msingi.



Mheshimiwa Naibu Spika, vyama vyetu viko saba navyo ni Kindoroko, Chakamwala, Charaa, Uchamangofi, Uchamandambwe, Ngujini na Kilomeni. Vyama hivi vinategemea sana wataalam wa Wizara yako wafike kule wawafundishe Wakuu wa Vyama hivi ili waandikishwe rasmi na Wizara yako na waweze kupata *guarantee* wakope kwenye Benki ambazo mmezichagua waweze kununua mazao ya wakulima na kuyauza kwenye mnada na hasa hapa ninaongelea zao la Kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa zoezi hili ni kuhakikisha ubora wa Kahawa. Nimesema hapa mara nyingi kwamba, ubora wa Kahawa yetu uko chini sana na ulikuwa chini sana kwa sababu ya kununua Kahawa kiholela kulikokuwa kunafanywa na wanunuzi wa soko huria. Lakini baada ya kupitisha sheria ile mpya na kuhimiza kwamba, sasa Vyama vya Ushirika ndio vinunue, tuna matumaini makubwa kwamba Vyama vyetu hivi vya Msingi ambavyo vina uzoefu mkubwa wa kununua na kuuza Kahawa vitahakikisha ubora wa Kahawa, halafu wao kwa kuuza moja kwa moja kwenye mnada, Vyama hivyo vitahakikisha vinapata bei nzuri kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, ninategemea kwamba wataalam hawa watakwenda katika siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya kuanguka kwa kiwango cha uzalishaji wa zao la kahawa ni kukosekana kwa pembejeo. Kahawa kama hukupiga dawa na hukutumia mbolea vizuri, huwezi kupata mazao mazuri. Sasa, kwa kuwa Vyama vya Ushirika vitakapokuwa vimewezeshwa kununua na kuuza Kahawa vitapata bei nzuri, basi tunaomba na utaratibu ufanywe ili wakulima na Vyama hivi viweze kukopa pembejeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nihimize kabisa kwamba, huu Mfuko wa Pembejeo usiende *EXxim Bank*, binafsi sijui hii Benki ni ya nani! Lakini tungetegemea kabisa kwamba, Mfuko kama huu kwa Wanamwanga ungekwenda kwenye Benki ya Wananchi wa Mwanga. Maana ndiyo inawajua, ni benki yao. Kwa nini Wanamwanga wenye Benki yao waende kuchukua mkopo wa pembejeo kutoka *Exim Bank* iliyopo Dar es Salaam? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi sijui Benki hii ni ya nani! Tumeambiwa kwamba eti ili-*tender*, ikapata. Hivi kweli kama ume-*tender* kwa kununua sukari, mtu akileta ujuzi wa chumvi unampa *tender*? Maana bwana *Exim* hakai Vijijini, hawezi kabisa kutoa mikopo kwa watu wa Vijijini, anaweza kutoa pembejeo kwa watu wa Dar es Salaam? Sijui watu wa Dar es Salaam wanalima nini?

Lakini naomba sana kwamba fedha za Mfuko wa pembejeo wa Wananchi wa Mwanga zikae kwenye Benki ya Wananchi wa Mwanga na katika Wilaya zingine iwekwe kwenye matawi ya *NMB* au kwa wale wenye benki zao za Wananchi iende kwenye Benki za Wananchi. Tusiwe na kigugumizi hata kidogo kwa hili! Hili siyo suala la soko huria, hili ni suala la msingi la kuboresha kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni suala la Benki za Watu Maskini. Benki hizi kwa jina lingine zinaitwa *SACCOS* au Ushirika wa Kuweka na Kukopa. Kuna Waswahili walinifundisha wakasema: “Asili ya mtu duni hata ukimficha kwenye chupa atatoa kidole kidogo ili aonekane, kwamba jamani niko hapa!” Sasa, watu ambao ni maskini wanapokusanya nguvu zao bado nguvu zile ni kidogo sana, inatakiwa tufanye juhudi za makusudi za kuwasaidia watu hawa wanaokuwa na *SACCOS* ili waweze kununua vifaa vya kutunza rekodi na fedha zao ili kusiwe na ubadhilifu. Lakini pia tunatakiwa tuviwezeshe vikundi hivi kwa kuvipa mitaji midogo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu wanachohitaji watu ambao wana *SACCOS* siyo shilingi milioni 30 au milioni 40, wenyewe wanataka kukopa dola 50 au dola 100. Ukimwambia mtu wa Magharibi: “Watu wangu wanataka kukopa dola 100,” atakushangaa! Lakini ndio mikopo ambayo watu wetu wanayotaka. Kwa hiyo, tungeomba tuwasaidie, tuwawekee utaratibu maalum kabisa wa kuwawezesha hawa watu wadogo hawa waweze kupata mitaji na waweze kupata vifaa vya kuweka kumbukumbu na *records* zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hapa tuliombwa katika Bajeti ya mwaka 2001/2002 tuwahimiza Wananchi wajiunge katika vikundi vya Kuweka na Kukopa. Wananchi wale wamejiunga kwa nguvu na wameitikia kweli kweli. Katika Jimbo langu sasa kuna vikundi zaidi ya 45 vya Wananchi ambao wana Vyama vyao vya Kuweka na Kukopa. Wapo watu 50, wanapokusanya nguvu zao zote wanapata

shilingi milioni 1, wangependa sasa tuwe na utaratibu ambao watu hawa wataweza kukopa milioni 1 nyingine, kama wana milioni 1 basi waweze kukopa milioni 1 nyingine ili wakopeshane. Watu ambao wameshajikusuru wakaweka fedha zao wana nidhamu ya kuweka akiba. Kwa hiyo, tungeomba sana mtueleze ni utaratibu gani watu hawa watafuata ili waweze kupata kamtaji kadogo ka kuwawezesha waweze kukopeshana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana katika masuala ya kuweka na kukopa na katika Vyama hivi vya Ushirika ni riba ya mikopo. Nimeongea hapa na nisingependa niogope kurudia tena kwamba, utaratibu na hali ya hewa ya uwekezaji hapa nchini kuweka na kukopa ni ngumu sana kwa mtu maskini. Kwa sababu mtu maskini akiweka pesa zake kwenye benki kwa sasa hivi anapata riba ya asilimia 1.5 mpaka asilimia 3.0. Kiwango hiki kiko chini ya mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei wa nchi hii tumeambiwa ni kama asilimia 5. Sasa kama unaweka fedha zako zizae chini ya mfumuko, maana yake unaweka pesa zako kwa hasara. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama utakuwa na utaratibu huu, unazuia watu wote wanaojua hili wasiweke fedha zao katika benki. Kwa hiyo, tunajenga jamii ambayo inakuwa na utamaduni wa kutoweka fedha katika akiba. Sasa, sheria zetu za benki zinamtaka Gavana wa Benki Kuu aangalie jinsi riba zinavyokwenda na azirekebishe ili ziendane na mfumuko mdogo wa bei na watu wetu waweze kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa na vijana ambao zaidi ya asilimia 80 hawana kazi unataka uwarudishe wale vijana kwenye kazi na wajajiri, ni lazima uwawezeshe kupata mikopo ambayo wanaweza kufanya kazi wakajirejesha. Kwa mtindo wa kukopa kwa asilimia 21 hadi 30 haiwezekani vijana wakakopa! Pia, haiwezekani tukawaondoa vijana kwenye vijawe kwa sababu kama hatuwaambii: “Nendeni mkauze madawa ya kulevya,” hakuna kazi nyingine wanaweza kufanya wakakopa kwa bei hiyo wakalipa! Hakuna sababu kabisa ya kufanya vijana wetu wasikope kwa asilimia 10 hadi 12! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu kabisa kwa sababu Makampuni makubwa mfano *TBL, IVECO TPC* na kadhalika, yanayokopa kwenye benki yanakopa kwa riba ya asilimia 8 hadi 12. Sasa, wanasema wakopaji wadogo siyo waaminifu, lakini vikundi vyote vidogo hivi vya uzalishaji mali vimeonyesha uaminifu wa hali ya juu sana, hakuna kigugumizi hapa! Vikundi hivyo vimeonyesha kwamba asilimia 95 hadi 100 wanarudisha mikopo yao. Benki ya Posta ina uzoefu huu katika Jimbo langu la Mwanga na katika Majimbo mengine yote. Hivi tunangoja nini? Maamuzi haya ni lazima yafanywe na hatuwezi kuwa na Benki Kuu, Sheria ya Benki Kuu na Sheria ya Mabenki ambazo hatuzifuati! Utampaje mtu riba ya asilimia 1.5 halafu akikopa unam-charge asilimia 30? Ni soko gani hili? *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** *Point!*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna soko ambalo halina kidhibiti. *There must be regulatory organs and these regulatory organs must work and be seen to work.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na kupitia kwake tuombe Serikali. Sheria ile inampa nguvu Waziri wa Fedha, kama Gavana hataki kubadilisha, alazimishwe, sheria yetu ndivyo ilivyo. Gavana wetu siyo Gavana wa *Bundas leaguer*, kwamba anaweza kuamua mwenyewe, hapana! Sheria yetu inasema *very clearly* katika *section seven* na sehemu ndogo ya pili: “Kama Gavana hafuati Sera ya Serikali, Waziri wa Fedha amlazimishwe afuate sheria hiyo na sheria hiyo ni lazima itumike.” Kwa sasa sheria hii inavunjwa kwa utaratibu wa riba tulionao na wakulima wetu hawawezi kuondoka hapo walipo kama hatukuchukua hatua za dhahiri kabisa za kuwasaidia na kutumia sheria zilizopo na kutumia mazingira mazuri ya *inflation* ambayo yapo nchi hii. Tumejanya kazi kubwa, tumeteremsha mfumuko wa bei, basi Wananchi waone faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niungane na Wabunge wenzangu kumpa pole sana Mzee wetu, Mheshimiwa *Sir George Kahama*, pamoja na mkewe

Mama Janet Kahama. Poleni sana kwa msiba ambao mmepata wa mtoto wenu mpendwa na Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kusema jambo moja ambalo lilinivutia sana juzi. Juzi nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, nilivyoingia mle ndani nikamuuliza: “Waziri hapa tuko Dodoma, tupo Dar es Salaam au tupo wapi?”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli napenda kusema kwamba, nilivutiwa sana na uamuzi wa Wizara ile kuwa tayari wameamua kuhamia Dodoma. Wana ofisi nzuri ya kisasa na wale wenzetu wanaofikiri kwamba kuna haja ya kuanza ku-*revisit* wazo hili la kurudi rudi Dar es Salaam, nafikiri waende ofisini kwa Mheshimiwa Sir George Kahama, wakaangalie mambo pale. Mambo ni mazuri, pia amenionyesha *expansion scheme* yao, jinsi wanavyotaka kupanua ofisi ile. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Wizara kwa hatua nzuri ambayo wameichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tunaongea mara ya mwisho hapa tunapata matatizo kwa sababu, kwa kweli Wabunge wenzangu wameeleza vizuri sana jambo hili la Ushirika. Ningependa kuzungumzia yale maeneo ambayo nafikiri kwamba labda ni ya kujazilizia tu. Kwanza ni-*takeoff* kutoka hapo alipoishia Profesa Jumanne Maghembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirika ni utaratibu ambao unakubalika katika mifumo yote miwili. Ukiwa katika mfumo wa kibepari Ushirika unakubalika. Ukiwa katika mfumo wa kijamaa Ushirika unakubalika. Kwanza nataka kuiweka hivyo, nataka kuangalia mambo kihistoria, kwa sababu nataka kuwa *Scientific* katika *argument* yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa Wamarekani au Waingereza, hawa wamepiga hatua kubwa ya kimaendeleo. Ukiwauliza je, unadhani Ushirika ni kitu muhimu? Watakwambaia ndio. Ubepari ulipofika katika *level* ya ukiritimba ule wanaita *monopoly capitalism*, wote wale wakati ule ubepari una-*draw tentacles* unakwenda *beyond the borders*, unakwenda nje ya maeneo ambayo umekuwa una-*operate*, wasomi akina Rosa Luxemburg, akina Lenin, watakueleza una-*create syndicate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *syndicate* ni watu kuungana. Unafika mahali unafanya ma-*financial oligarch*. Wanajitengeneza hivi wanakuwa kitu kimoja, wanaungana ili kuweza kukabiliana na adui. Ni mabepari wala sio malofa kama nchi changa hii. Wajamaa walipoona mfumo huu unakwenda mbio namna ile na unawatupa nje ya *fence*, wakaona na wao njia ya kuweza kukabiliana na hali ile ni kujiunga katika Ushirika.

Kwa hiyo, sehemu zote hii ni *very peculiar*, wenye ujamaa wanazungumza habari ya Ushirika, kwenye ubepari wanazungumza habari ya Ushirika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alipoamua kwamba hii Wizara iwe ni Wizara pekee ya Ushirika na Masoko, kwa kweli nadhani aliliona vizuri na ninapenda kumpongeza kwamba alifikiri hivyo akaipa huo umuhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirika ni nini? Ushirika ni Muungano wa watu wanaokubaliana katika mkakati wa kukabiliana na matatizo yao. Wanakaa hivi wanafikiria wanajiunga. Kwa kawaida mnapojiunga ni hiari. Sisi hapa tumekubali, tumehama kwenye mtazamo na mwelekeo huo wa kijamaa tumekwenda kwenye mwelekeo wa kibepari. Sisi hapa hatuna *capitalism* kwa sababu huruhusiwi kujenga ubepari hapa, wala huruhusiwi kujenga ujamaa. Huruhusiwi kujenga *an independent economy*, huruhusiwi! Hili ni eneo la *colonial economy* na wenzetu mabepari hawa, hao tunaowaambia tuwape wakulima wetu ruzuku wanakataa, hawataki wewe utoe hicho kitu kwa sababu utajitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tukiwa Nairobi pamoja na Dr. Chegeni Masunga, tulizungumza na *World Bank* na tulizungumza na *IMF*. Mimi nikaleta *argument* hii ya ruzuku, nikawaambia, jamani, ninyi juzi hapa George Bush na akina Jacques Shiraq wamekutana pale Geneva wanaambiwa na hizi nchi changa, ondoeni ruzuku kwa wakulima wenu wanakataa. Sisi tumekwenda Nairobi pale tumesema maneno haya, kwa kundi kubwa la *World Bank* na *IMF*, *statement* yake Dr. Chegeni Masunga, anaikumbuka, wanasema: “*This is unreasonable argument,*” wanaiita hivyo. Wao wakitoa ruzuku kwa wakulima wao hiyo ni sawa sawa kabisa, ni sahihi, hiyo ni akili nzuri. Sisi tukisema wakulima wetu

wadogo wadogo hapa wapewe ruzuku tunaambiwa ni *unreasonable thinking*. Afrika ni lazima ifike mahali iwe na *carriage* ya kukataa mambo mengine na kusema *no*, ni lazima ifike hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, tulimheshimu hapa na mpaka tumemzika pale Butiama moja alilokuwa ana-*address* ni hiyo. Mtu anakuja hapa anakwambia: “Usiwape wakulima wako *subsidy*, sawa. *STABEX* imeambiwa inakuja hapa kuwasaidia wakulima, lakini wanasema usiwape hiyo hela wakaweka kwenye mfuko wao. Sisi tunakaa tu tunakubali kila kitu. Tufikie mahali tuwaambie, ondoa hela yako hapa, chukua basi kama mnakataa, mambo haya mlitwambia wenyewe. Kabla ya kufanya mambo haya wadau wote wakulima wa Tanzania washirikishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelia hapa, tumeieleza hapa karibu wanifunge *POP* kwenye sikio na kwenye shingo. Hakuna.

Napenda kuiomba Serikali na Mheshimiwa *Sir* George Kahama, Serikali nzuri ni ile inayo-*respond*. Hili jambo limesemwa na kila mtu humu ndani. Hebu tufikiri vizuri tunafanya kumsaidia mkulima mdogo mdogo? Si kwamba tunakuwa king’ang’anizi hapa. Hiyo hela ya *STABEX* kama ipo hapa nendeni mkatafute matamshi au maandiko ambayo yanaweza yakasaidia walau kuhalalisha utoaji wa hii hela. Msitoe yote kwa sababu wataawaambia kwamba hatutotoa tena. Walau sehemu fulani itolewe kwa ajili ya wakulima, iende *direct* kwenye mikono ya wakulima kuhamasisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha (*Siha Kiyeyo Cooperative Society*). Mkutano Mkuu umeniomba nije hapa, *Kengia Cooperative Society* wamenionba nije hapa, *Wanri Cooperative Society* wamenionba nije hapa. Mae, Koboko, Kalansi wanaomba, nenda Mbunge kamwambie Waziri, mwambie Spika tunaomba sehemu fulani ya hela za *STABEX* zije kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tuliambiwa hapa kwamba kuna *element* ya *kitochi* na nini, nimesema na nimeeleza. Nataka nirudi pale pale kwenye Ushirika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimefanyika kwenye hii hotuba na ndiyo maana naipongeza na ninaiunga mkono moja kwa moja. Sisi hapa, tulisema soko huria. Soko huria ni *component* ya *capitalism*. Soko huria linachotafuta ni faida kibao, si faida tu ni *super profit*. Hawapeleki pale kitu kinachoitwa *constant capital*, wanapeleka pale *variable capital*. Unachukua *constant capital*, jumlisha na *variable capital*, jumlisha na *surplus labour* ndiyo unapata *total value*. Ni mpaka umnyonye mkulima mdogo mdogo, ukishamnyonya ndio wewe utatengeneza faida kibao! Sasa sisi tunashindwa kuona hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa tukasema ainisha soko huria lisijihusishe na mkulima mmoja mmoja kule Kijijini, liende kwenye mnada. Tukapitisha mazungumzo hapa na ikawekwa katika utaratibu. Hivi tunavyozungumza, Vyama vyangu ambavyo nimevitaja hapa vimepata malipo ya pili ya shilingi 100/= kwa kilo. Juzi tu tumeanza kujaribisha hapa, mara ya kwanza, wako wengine wamepata shilingi 150/=. Sasa, waulizeni wale watu ambao walikwenda wakauza kwenye soko huria kama walipata kitu, hawakupata hata senti tano. *They never got*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya leo ndugu yangu Benedicto Mutungirehi, hayupo hapa, maana ndio huwa tunashindana naye katika jambo hili. Labda nimuulize, wale walioko Kagera waliokwenda kuuza kwenye soko huria hawakupata haya malipo ya pili ambayo Waziri anayazungumza humu ndani? Sasa sisi tumekamatia hapo. Mambo yanayofanyika ni kwamba, kwanza tumeweke *government guarantee* katika jambo hili, tumewasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi Benki zetu za Ushirika zipewe mikopo ziende zikanunue mazao ya wakulima. Ndio hiyo anayosema Profesa Jumanne Maghembe, hapa. Tuliizungumzia hapa, tukasema wapewe na wamepewa. Wanaoamua kuuza kutoka kwenye Chama cha Msingi kupeleka sokoni wauze, wanaoamua kwamba watakwenda kwenye *APPEX* kwa maana ya kupitia kwenye *union* waende.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nafikiri kama tunataka ku-improve quality ya Kahawa inayozunguzwa hapa, Kahawa ya Koboko usiichanganye na Kahawa ya Wanri, ya Wanri weka mahali pake. Ama hata kama imepitia kwenye KNCU pale, weka label kwamba hii Kahawa ni ya Koboko Cooperative Society. Hii hapa ni ya Wanri Cooperative Society, hii hapa ni ya Siha Kiyeyo Cooperative Society, ndivyo tulivyokuwa tunafanya.

Kwa hiyo, ukipeleka Kahawa ikienda kule inajulikana watu ambao wanaonekana wanatunza kahawa yao vizuri, lets say watu wa Siha, Kiyeyo Cooperative Society. Kwa hiyo, watu wa Vuasu wakitengeneza Kahawa nzuri watapeleka Kahawa yao ita-fetch market. Competition tunayozungumzia hapa ni hiyo. Sasa hapa tunachanganya kahawa yote inabebwa inakwenda kule, wengine tunawaruhusu inakwenda kwenye soko huria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema kwamba kutakuwa kuna regulations ambazo zitolewa na nina habari kwamba kuna watu wa soko huria wanaanza kupitapita humu, ambao ndio wananunua kahawa mpaka ile mbichi. Chonde chonde Mzee wangu, Sir George Kahama, kama unaruhusu, ruhusu maeneo mengine yote, Jimbo la Siha naomba msiruhusu kitu kinaitwa soko huria lisije! Kwa sababu huwezi leo ukasema Ushirika ni muhimu humo humo unaweka kidudu mtu ambacho kitatafuna ule Ushirika, haiwezekani! Ni lazima ufike mahali uchague useme hivi: “Angalia bwana, wewe Doorman, wewe Tailor winch, ukitaka kwenda kununua kahawa ya wakulima nenda minadani, kwisha! Huhitaji kwenda Chuo Kikuu, elimu ya darasa la saba inakutosha kuelewa jambo hili. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wazee wangu hakuna ugomvi hapa, politics za Kilimanjaro, kule ninakotoka, usipozungumza habari ya Kahawa hapa, sirudi humu ndani, sirudi! Ndio ninaagana na ninyi moja kwa moja! Anayesema nina-impress ni kweli, nina-impress, ninataka ni-impress. Tunaomba mtusaidie. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuzungumzia issue ya mashamba ya KNCU. Naomba mnisikilize vizuri kwa hili. Sina ugomvi kuhusu mambo ya kukodisha mashamba yale. Mheshimiwa Sir George Kahama, mashamba yale yakodishwe, lakini wakati huo huo tukitilia maanani wale Wananchi ambao wanayazunguka. Habari ya kuwa tunakodisha yale mashamba yanakwenda kwa watu tu kutoka sehemu nyingine kwa sababu tu wana uwezo wa kifedha na unaacha ku-consider hao wananchi walioko katika maeneo haya ambayo na wao wameonyesha interest, you are sitting on a time bomb, on a very high voltage wire. Hawatakubali! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza namna hii na Mkuu wangu wa Mkoa yumo humu ndani. Ni vizuri tukawa-consider na wao, kama wanaonyesha interest kwamba na wao wako tayari kuingia katika ule mchezo. Wapewe nafasi ya kuweza kukodisha yale mashamba na kwa maana hiyo kwa vile tunazungumza habari ya wakulima wadogo wadogo ni lazima uweke special provision kwa ajili ya hawa wakulima wadogo wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia tena kuhusu suala la STABEX na ninaiomba sana Serikali, wala hamtakuwa mmefika mahali mkaonekana watu wa ajabu! Serikali itakuwa imeonyesha kukomaa. Kukomaa (maturity) maana yake ni kufanya jambo hata kama hulipendi. Tafuteni language, tafuteni maandiko, tafuteni namna ya kuliweka walau sehemu fulani for political purposes, mtoe hiyo hela ya STABEX iende kwa mkulima mdogo mdogo ipitie mkononi mwake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia tena kusema kwamba sina ugomvi. Wabunge wenzangu hii hoja tunayoizungumza hapa imekuwa addressed katika hiki kitabu, tupitische hotuba hii. Nami namtakia kila la kheri na fanaka, walikuwa wanasema wewe ni Mzee, ona kazi ambayo umefanya hapa, kazi ya maana sana na nakuombea maisha mazuri, uendelee hivyo hivyo, tunataka watu wa type yako na sisi tuko nyuma yako tutakuunga mkono. Naomba niseme ahsante na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpa pole Mheshimiwa Sir George Kahama na Mama Janet Kahama, kwa msiba uliowapata, ni hali ya dunia na ninaomba Mwenyezi Mungu awazidishie nguvu na waweze kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Ushirika na Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wasemaji wenzangu walionitangulia walivyosema kwa sauti kubwa na za msisitizo, si kwamba labda wana chuki, hapana! Ni kuonyesha kwamba ni kwa namna gani Wizara ya Ushirika na Masoko, inagusa sana Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara ya msingi sana na hasa ukizingatia kwamba tunategemea kilimo kwa asilimia kubwa sana hapa Tanzania. Kwa msingi huo, Vyama vyetu vingi vya Ushirika vimekumbwa na matatizo ya kila aina ambayo ndio yenye mtandao wa wakulima walio wengi. Wenzangu wengi wamezungumzia juu ya Kahawa, mimi naomba nizungumzie juu ya matatizo ya Pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba nikiri kwamba hotuba hii ya Wizara ni nzuri na Mheshimiwa *Sir* George Kahama, ameandaa vizuri sana na pengine labda niridhie kwamba wanasema uzee ni dawa, basi ametumia busara yake katika kuleta hotuba nzuri. *(Makofi)*

Kwa kweli wengi hawakutegemea lakini tumeona kwamba Wizara hii katika kipindi cha miaka miwili na nusu sasa imeanza kuonyesha dira na mwelekeo wa shughuli zake. Watu wengi ilikuwa ukiwahoji kwamba Wizara hii inafanya kazi gani ilikuwa ni vigumu sana kuelezea. Lakini tumeanza kuona jinsi ambavyo mikakati na mipango inavyoanza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba si kweli kwamba Vyama vya Ushirika vimekuwa havikopesheki ni kwa sababu Vyama vingi vya Ushirika vina matatizo mengi sana. Kwa mfano, *Nyanza Cooperative Union*, hiki chama kilikuwa ni chama kikubwa sana katika Kanda ya Ziwa na katika nchi hii. Lakini kimegubikwa na madeni mengi sana, kimegubikwa na matatizo mengi sana. Sasa hivi kimewekwa kwenye ushindani wa soko huria. Sasa katika soko huria, hiki chama kinachechemea na wengine hawana *investment* zozote katika ununuzi wa mazao. Lakini hawa wana mtandao mkubwa sana. Vyama hivi vina viwanda na vinu vya kuchambulia Pamba ambavyo vingi vimeshazeekea havifanyi kazi vizuri, kina mali ambazo zimeshachakaa na bado vimegubikwa na ubadhilifu uliokithiri.

Lakini sasa ukisema kwamba vyama hivi viende Benki vikakope na vitozwe riba kubwa mimi nashangaa sana kwamba ni kwa nini pasiwe na mpango wa makusudi kabisa *under export guarantee* ili vyama hivi vipewe fedha si sambamba na taasisi za mabanki ambazo zinakopesha wanunuzi wengine wa mazao ya Pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kusema kwamba tatizo moja katika Ushirika ni kwamba hakujawa bado na mafunzo ya elimu ya ushirika shirikishi unaolenga kuwawezesha wana Ushirika na jamii kuleta mabadiliko katika utendaji wa shughuli zao. Kila siku tumekuwa tukizungumza lakini naona haifanyiki hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirejee kwenye zao la Pamba. Zao la Pamba ni zao ambalo linatoa ajira nyingi sana kwa Watanzania wengi. Kuna wakulima, kuna wakamua mafuta, kuna viwanda vya nguo, yote hii ni sehemu ya ajira kutokana na zao la Pamba. Vile vile Pamba inatoa malighafi ya viwandani, linachangia Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa na vile vile ni zao lenye lina mvuto wa pekee kwa wahisani wengi kwa sababu siku hizi Pamba inaitwa ni dhahabu nyeupe. Sasa kwani mpaka kufikia kuitwa dhahabu nyeupi maana yake ni zao ambalo lina mvuto wa peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zao hili linachukua Watanzania asilimia 48 ambao wananufaika na zao hili. Mwaka 1994 liliweza kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 24.6. Lakini zao hilo hilo mwaka 2000, lilichangia kwa asilimia 4.4. Hii ni kutokana na kwamba mwaka 1994 lilizalisha marobota 532,440. Lakini msimu wa mwaka 1999/2000 yakakomea marobota 196,000. Sasa uone jinsi ambavyo zao hili halijapewa msukumo wa kutosha. Ni zao ambalo linachangia sana Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Watanzania wote tunaguswa sana na mabadiliko yoyote yanayojitokeza kwenye zao la Pamba na hasa wakulima wa Mikoa 13 ambao wanalima zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la Pamba licha ya kulimwa katika Mikoa 13, wakulima kama shamba limeweza kutunzwa vizuri, wanaweza kuvuna hadi kilo 750 za Pamba mbegu kutoka kwenye hekta moja. Lakini kwa wastani wa kiwango cha kimataifa inapaswa kuwa kilo 1,800 kwa hekta. Lakini mkulima wa Tanzania hana ruzuku kwenye pembejeo na bado unakuta kwamba anaweza angalau kuvuna karibu nusu ya wastani wa uzalishaji wa kiwango cha Kimataifa. Mimi bado natoa hoja kabisa kwamba kuna haja ya makusudi kabisa kuweza kulipatia msisitizo na mkazo zao la Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli soko la zao la Pamba limekumbwa na matatizo mengi sana. Ukiangalia kwamba huku limevurugukiwa na mfumo wa usambazaji wa pembejeo. Mimi napenda kuwashukuru sana Bodi ya Pamba kwa kweli kuanzia mwaka jana na msimu huu kumekuwa na mikakati mizuri sana walau inawa-*focus* katika kuboresha zao la Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Msukuma ukimwondoa katika zao la Pamba unataka afanye nini? Kwa sababu tunategemea sana zao la Pamba, hii kwa kweli ni mikoa mingi 13 hapa nchini inategemea zao la Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakulima wamekuwa wakiathirika sana na mabadiliko ya bei ambao kila siku mtu analima pamba hajui atapata kiasi gani. Hii inaondoa *incentive* kwa mkulima kuweza kulima Pamba kwa sababu anapolima anakuwa hafahamu bei. Mwaka huu bei ya Pamba imeweza kuwa katika kiwango cha juu sana, kiwango cha kilo moja shilingi 225 kwa Pamba mbegu mpaka shilingi 330. Lakini hiki ni kiwango kizuri tunashukuru, tatizo moja linalokuja sasa hivi ni kwamba bado kwa kutokuwa na mfumo wa Vyama vya Ushirika bado mkulima huyu anaona ni bei ya juu lakini bado anaibiwa kwa sababu wanunuzi huru wengi hawako (*sincere*) wakweli.

Katika kilo tano wanazonunua kwa mkulima wanakuambia kilo tano hizi kumbe ni kilo 8 na wanasema nakupa shilingi 330/= . Sasa Mkulima kwa sababu hafamu na kwa sababu mizani nyingi zinazotumika kupima Pamba hii hawana ujuzi nazo, wengi wanaibiwa kwa mfumo huo. Mimi ninachoomba Wizara hii ichukue jitihada za makusudi kabisa za kuimarisha Ushirika. Ushirika ndiyo chanzo na mkombozi wa mkulima katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuna tatizo la kutokuwa na takwimu sahihi za taarifa za bei ya soko. Hili naomba iwe ni mkakati naomba uwe ni mkakati mmoja wa makusudi kabisa kwa Wizara hii, ili iweze kufanya kazi *in advance*. Mkulima anapolima pamba yake anaweza kujua kwamba atapata bei kiasi gani ili mtu aweze kufanya mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka zamani ilikuwa wazee wetu wanalima Pamba wanajua kabisa kwamba mwaka huu nikilima Pamba nikivuna nitaoa mke, nitanunua baiskeli na nitajenga nyumba. Lakini leo hii hakuna mkulima anayeweza kuwa na hizo ndoto kwa sababu hajui kwanza Pamba yake atauza kwa bei gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushindani uliopo katika soko la Pamba mimi naona bado siyo *fair*. Kuna haja kwa kweli kufanyike mikakati ya kuweza ku-*rationalize* na kuvisaidia vyama ambavyo vina mtandao mpaka kwa wananchi ili iweze kupewa kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna haja ya Wizara hii kuangalia tumekuwa tukiuza sana Pamba ghafi, kwa nini tuendelee kuuza Pamba ghafi, kwa nini sehemu nyingine ya Pamba tusiitumie hapa hapa kwetu kwenye viwanda vyetu na kuuza vitu ambavyo vimeshakamilika ama *finished goods* hii itasaidia sana kuweza kuongeza soko na thamani ya Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kifanyike? Rafiki yangu mmoja Mjapan aliniambia siku moja akasema kwamba sisi tunapenda kula samaki ambao ni *fresh*, sasa kumchukua samaki *fresh* kutoka Mwanza kumpeleka mpaka Japan si rahisi lazima uweke *ice* na um-*freeze* uweze kupeleka. Lakini ukipeleka samaki bado wanakuwa ni wale ambao wamepoteza ladha yao.

Sasa akasema tumia *fishing container*. Basi tukatumia *fish container*, lakini bado samaki wakawa bado siyo *fresh*. Sasa likaja wazo kwamba basi mkiwa na *fishing container* wekeni angalau na ka-*shark* kadogo humo ndani ambako kataendelea kuwala wale samaki walau katika samaki 100, 20 wataliwa lakini 80 wata-*survive*. Maana yake nini ni kwamba *this is the challenge*, wale samaki kila mmoja atakuwa anakwepa huyu *shark* asimle ili kusudi aweze kufika mzima na huyu mlaji aweze kumpata samaki akiwa bado *fresh*. Sasa Wizara hii naipa changamoto ili iweze kuweka mikakati makusudi kabisa ya kumsaidia mkulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuanzisha Mfuko wa Pembejeo ni muhimu sana, hii itasaidia wakulima wengi waweze kupata pembejeo kwa muda unaotakiwa na vile vile kwa uwezo uliopo. Kwa sababu mkulima unapompelekea pembejeo wakati msimu wa kilimo umeshaanza hana fedha na hawezi kununua. Hii itasaidia sana. (*Makofi*)

Vile vile kufanyike utafiti wa kupata mbegu bora za pamba. Naisifu Bodi ya Pamba kwamba imechukua jitihada za makusudi kabisa safari hii na ningeomba kutumia nafasi hii kusema kwamba hii Bodi basi ipanuliwe. Jinsi ilivyo hailingani na mahitaji ya wakulima wa Pamba. Ni vema ingepanuliwa ili ipewe uweze mkubwa zaidi ambao utaweza kuwa-*service* wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni utoaji wa taarifa za soko ili ziweze kuwafikia wakulima mapema zaidi ikiwa sambamba na mafunzo. Sasa hivi unakuta kwamba hizi huduma za ugani hazipo kwa wakulima. Kumekuwa na mabwana shamba lakini hawafanyi kazi za ubwana shamba. Naomba kwa kweli safari ijayo Mheshimiwa Waziri, tunaomba Wizara yako iweze kutenga fedha ambazo zitasaidia sana kuweka *extension service* mpaka kwa wakulima, hii itawasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kwamba kuboreshwe masoko na biashara ya Pamba. Vile vile kuweza kuhuisha miundombinu. Huko nyuma tulishazoea kunapokuwa na msimu wa Pamba karibu barabara zitatengenezwa, miundombinu itaimarishwa ili kuweza ku-*service*. Lakini siku hizi wenzangu hapa wenye *STABEX* wanazungumzia fedha hiyo, mkulima wa Pamba yeye afanye nini? Kwa nini naye kusiwe na mfuko maalum wa kuweza kum-*service*? Serikali ifanye jitihada za makusudi kuwasaidia wakulima wa pamba nao. Kwa nini mkulima wa Kahawa na mkulima wa Chai pekee ndiyo anapewa nafasi ya kupewa fedha za *STABEX*? Kwa nini mkulima wa Pamba asipewe fedha za namna hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kuwe na mkakati ambao utasaidia kuweza kuboresha zao la pamba na kuwasaidia wakulima wa Pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote naomba kwa niaba ya Wananchi wa Arumeru Mashariki, kutoa rambirambi zetu kwa Mheshimiwa Waziri, *Sir George Kahama* na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kufiwa na mtoto wao mpendwa, naomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri ambayo imeonekana waziwazi kwenye hotuba yao yenye dira nzuri kwa Sekta ya Ushirika na Masoko. Napenda kuchangia kwenye maeneo mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kukumbusha ahadi ambayo tumekuwa tukikumbusha hapa Bungeni kwa muda mrefu nayo ni kuhusu soko letu la Tengeru Jimboni Arumeru Mashariki. Naipongeza Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko kwa kutupatia mradi wa kuendeleza mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo (*Agricultural Sector Marketing Development Program*) na ombi langu ni kwamba kwenye mradi huo na hasa *component* ya tatu inayoshughulikia msaada wa miundo mbinu ya masoko tuweze kupata kuendelezewa Soko la Tengeru na hasa lijengwe kama ambavyo wakati fulani tulishaahidiwa kwamba litajengwa.



Ombi letu ni kwamba mwaka huu wa fedha hilo soko lijengwe na ni ombi letu rasmi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Serikali nzima kwamba mwaka huu watuondolee hiyo kero ya Soko la Tengeru na tuna imani kwamba ombi letu mwaka huu litasikilizwa na litatekelezwa. (Makofi)

Tuna imani kwamba tutakapoliona tuna mila zetu Wameru, pale Mlima Meru kuna Ukoo wa Mbise, ambao ukiona mambo mazuri yanatendeka unapanda mlima unakwenda kutoa sadaka za kimila kwenye *Kirumbi Kya Varwa* wanatoa shukrani za mila. Tutakapoona hilo Soko la Tengeru limejengwa, tutafanya hivyo kwenda kushukuru Serikali na Wizara kwa kutoa Asali, Mbege, Maziwa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri tutakuaribisha uje kunywa Loshoroo. (Makofi/Kicheko)

La pili, Mheshimiwa Waziri ni kuhusu makato kwenye mauzo ya Kahawa. Labda hili siyo kahawa tu huenda pia na mazao mengine ambayo yanauzwa nje kama vile Pamba na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano hai wa mauzo ambayo yamefanyika na kikundi cha Kahawa Jimboni kwangu, kikundi hicho kinaitwa Muungano wa Vikundi vya Kahawa King'ori na Legeruki (*MUVIKAKILE*). Hiki ni mojawapo ya vikundi ambavyo vimeitikia wito wa kuboresha zao la kahawa na kuuza kahawa ambayo ni ya ubora wa hali ya juu kwa matazamio ya kupata bei nzuri. Kweli tumeshaanza kuona mafanikio makubwa. Lakini kuna kitu ambacho wengi tumeanza kulalamika ambacho kinatokana na unafuu ambao tulikuwa tumeahidiwa kwamba kodi nyingi zitapunguzwa kwenye bei ya kahawa ili kumpunguzia mzigo mkulima anayelima kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi hiki cha *MUVIKAKILE* kiliuza Kahawa yao ya msimu wa 2002/2003 kati ya Novemba, 2002 na Machi 2003. Kwa kila mauzo waliyoyafanya huko Moshi, walikatwa kama ifuatavyo:-

Kwenye *Auction Sale No. TCB/M/16* ya tarehe 23 Januari 2003 waliuza kilo halisi yaani *Net Weight Grade A* na kupata dola 6760.26 wakauza tena kilo halisi *Grade B* na kupata dola 7,375.20. Jumla ya mauzo hayo mawili kwa mfano dola 14,135.46 makato waliyokatwa, kuna *TCB Levy* ya 1.5% dola 2120.3, wakakatwa tena asilimia 2 ya *VAT 20%* kwenye *TCB Levy* dola 42.41. Wakakatwa *research cess* dola 35.34 na jumla dola 289.78. Halmashauri nayo ilikuwa awali wameahidi kukata shilingi 5/= kwa kilo, lakini wakabadilisha wakaanza kukata kwa kufuatana na bei ya mauzo mambo yakabadilika. (*Export bags*) magunia ya kuuzia kahawa nje wanalipa shilingi 1,422 unaweza kupata *effect* ya bei ya gunia kwenye bei ya kilo ukichukua kwamba inapopeleka kwenye *curing wastage rate* iko kwenye asilimia 20 mpaka 23 unaweza uka-*compute* hapo kwamba basi bei yao inakuwa kwa kiasi gani. Halafu kuna *curing Levy*, *Curing Levy* kwenye *patchment coffee* shilingi 46/= kwa kilo. Hiyo *Levy* kwenye *curing* ya *patchment coffee* inakatwa pia asilimia 20 ya *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu tunaomba Serikali kupitia Wizara hii husika kwamba *Tanzania Coffee Board Levy (TCB)* iondolewe kabisa na kama haiwezekani eti inakatwa hivyo kwa sababu ya sheria iliyopo basi hiyo sheria irejewe. Hiyo *levy* iondolewa huo mzigo utolewa kwa mkulima. Hiyo siyo tu kwa zao la mkulima na kwa *TCB* pia na bodi nyingine za mazao zinafanya hivyo nazo pia zitazamwe. Pia hii *VAT* ya asilimia 20 kwenye *Levy* ya *TCB* na kwenye *Levy* ya *Curing*, mimi siilewi kwa kweli. *Levy* mimi nadhani ni kodi *in a way* ni kodi. Sasa hapa *VAT* pia nayo ni kodi, kwa hiyo, tunatoza kodi kwenye kodi yaani unalipa kodi halafu, unatoza tena ile kodi uliyolipa unaitoza tena kodi. Mkulima ni yule yule, zao lake ni lile lile linalotzwa hii kodi. Mimi nadhani hii kidogo waziwazi tunamwonea mkulima na hii nadhani ni unyang'anyi kama tuna- *rob*. (Makofi)

Kwa vile zao la Kahawa ni zao kama lingine kama vile Mahindi, japo linaitwa ni zao la biashara lakini sidhani kwamba ni tofauti sana na mazao mengine ambayo yanaleta hela kama mahindi, kabichi na kadhalika. Kama tumemsamehe mfanyabiashara wa mazao madogo madogo kwenye biashara ndogo ndogo anapopeleka sokoni tukamsamehe kodi anakwenda sokoni akauza hilo zao lake, huyu mkulima wa kahawa anapofungasha kwenye gunia akaenda kupeleka kwenye soko mbona yeye anakatwa kodi hiyo *VAT*? Hiyo *VAT* inakatwaje jamani yaani kwa vile tu soko lake ni tofauti na Soko la Tengeru badala yake anapeleka Moshi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa kweli naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa jumla ilitazame hili suala mkulima aondolewa haya makato na huu mzigo wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu pembejeo. Mimi hasa nitatumia hasa kwenye mfano wa Jimbo langu ambalo kwenye zao la Kahawa na mazao mengine pembejeo, kuzipata kwanza ni matatizo, bei yake ni kubwa mno, ukweli uwezekano wa kukopa kupitia fursa zilizopo kama vile *Export Import Bank* na tuna *branch* Arusha na ni kweli inakopesha nakumbuka karibu watu arobaini walipeleka maombi yao yalikubalika lakini watu walishindwa kwenda kuchukua sijaelewa sababu ni nini. Hii benki nafahamu kwamba Serikali yetu ina-*share* kule nafahamu kwamba benki ya dunia pia kupitia shirika lao la *International Finance Corporation (IFC)* au *private arm* ya *World Bank* ipo kule na nina imani wameanzisha kwa nia njema riba yao ni asilimia 12. Lakini watu sijaona wakienda kwenye hii *Export Import Bank* kuchukua msaada unaopatikana kwa njia ya mkopo. Kama wengi walivyozungumza ni kwamba kweli ...

*(Hapa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya alisimama mbele ya Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, unavunja Kanuni kaa chini haraka. Haya endelea kuchangia Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Ahsante nashukuru. Ombi langu hapa ni kwamba Serikali ebu ifikirie tena kwamba japo kwa njia ya mkopo wengi hawakatai kwamba kwa njia ya kukopa tupate mikopo kwa ajili ya pembejeo hatukatai na riba kidogo itazamwe, asilimia 12 japo mnaweza mkaona si kubwa kwenye *Commercial Banking Sector*, lakini kwa kweli kwa mkulima hiyo riba ni kubwa mno. Tuna imani inawezekana kuipunguza kidogo. Pendekezo langu ni kwamba inawezekana kupunguza hiyo riba mpaka kwenye asilimia 5 mpaka 6 lakini isizidi 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani inawezekana kabisa ku- *negotiate* na hawa *Share Holders* wengine katika *Exim Bank* ikawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu hili shirika linalo-*audit* Ushirika, *COASCO* ambalo limezungumziwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 10. *Corporate Audit and Supervision Corporation (COASCO)*.

Mimi hapa napendekeza kwa mara nyingine nimetazama jinsi wanavyofanya shughuli zao matatizo yamekuwepo kwa muda mrefu na nina imani Serikali imekuwa ikiliona hili. Mimi napendekeza kwamba litazamwe upya, *COASCO* ionwe upya, sheria iliyoanzisha irejewe. Mimi nina imani kwamba kwa mfumo wake ulivyo sasa hivi nadhani haitusaidii sana kuboresha ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Bunge hili la Bajeti nina bahati kwamba kila mara ninapochangia nakuwa wa mwisho. Sasa unapokuwa wa mwisho unajikuta mambo yote yameguswaguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningependa nichukue nafasi hii, kuungana na wenzangu kumpa pole mzee wetu Mheshimiwa Waziri *Sir George Kahama* kwa kufiwa na mwanawe. Tunamwomba Mwenyezi Mungu amepe nguvu ili aweze kuendelea na kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii nimpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umakini na umahiri mkubwa sana. Hongera sana. Kabla sijaanza kuchangia na mimi niungane na wenzangu kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baba yangu alinifundisha jinsi Ushirika ulivyoanza katika maeneo ya kwetu hasa Ushirika wa Kahawa. Ushirika kule kwetu ulianzishwa siyo kwa sababu ya kibri, isipokuwa kwa sababu ilionekana kwamba kuna watu 10 wanalima Kahawa pamoja, halafu watu 9

wakapiga dawa za kuua wadudu, halafu mmoja akaacha, maana yake wale wadudu watakimbia kwenye shamba lile ambalo halikupigwa dawa ya kuua wadudu na baadaye watasambaa na hivyo kuharibu mazao. Hii ndiyo ilikuwa ni misingi hasa ya Ushirika. Sasa kwa mantiki hiyo suala la soko holela au soko huria katika baadhi ya mazao yanayohitaji nidhamu kwa kweli halifai.

Mimi naungana kabisa na wenzangu kwamba kule kwetu mfano tuliona mwaka 2002 wananchi walikubali kuuza mazao kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi, lakini kutokana na watendaji ambao wana uchu wa kupata fedha za pembeni walianza kuwapa wanunuzi binafsi kununua kahawa na matokeo yake ni kwamba wako wakulima ambao leo hawajalipwa fedha zao.

Sasa mimi nasema kwamba safari hii sitatoa shilingi lakini nasema kama hawa wanunuzi binafsi hawataruhusiwa, safari hii wakawakopa watu mazao yao halafu wasiwalipe na Serikali isichukue hatua, nitatoa shilingi katika Wizara tatu. Wizara ya Kilimo na Chakula, TAMISEMI pamoja na Ushirika na Masoko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana na nashukuru sana kwamba nilipopiga kelele mwaka jana, zile leseni zilifutwa na wananchi walifurahi sana. Sasa mimi ningependa kabisa kwamba tunaposhughulikia haya mazao, lazima Serikali ihakikishe kwamba panakuwa na uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa nianze kuchangia hasa suala la Ushirika lenyewe. Kwa kweli kasi ya kufufua Ushirika mimi binafsi naona ni ndogo. Inakwenda polepole. Kwa sababu pamoja na kwamba imeundwa Wizara mpya, lakini bado watumishi na viongozi wa Ushirika, bado ni wale wale ambao walisababisha kuua hivi Vyama vya Ushirika. Sasa Serikali inafanya nini? Kwa nini isiwaondoe? Lazima tuwafanyie tathamini, tuwafanyie upekuzi, tuone kwamba kama walihusika, basi wang'olewe mara moja tuanze upya. Hii ni dawa pekee, vinginevyo hawa viongozi wataendelea kutumia jeuri ya fedha ambazo wamezikusanya na zile ambazo wanazikusanya ili kunyanyasa wanachama.

Kwa hiyo, mimi nasema wazi kabisa kwamba kama tunataka kweli na tunadhamiria kufufua Ushirika, basi tuanze kuwa na watu ambao wanaushirika watakuwa na imani nao. Sasa hivi wakulima wengi wamepoteza imani na baadhi ya viongozi wa Ushirika na Serikali inawajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichangie suala la masoko. Mwezi Mei, nilikuwa nazungumza na wakulima wa kahawa Wilayani Mbinga. Niliwauliza nani leo amekunywa kikombe cha Kahawa? Hakujitokeza hata mmoja. Lakini nilipouliza nani amekunywa chai, watu wengi wakanyoosha vidole. Sasa hapo kuna hatari. Tunalima kitu ambacho hatuli na si kweli kwamba watu hawali, lakini hakuna chombo cha kuhamasisha na kuweza kutengeneza ile Kahawa ili inywewe, kwa hiyo, Kahawa yetu yote inauzwa ikiwa malighafi.

Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tunajandaa tu kwa ajili ya soko la nje badala ya kuendelea soko la humu ndani. Kwa hiyo, mimi ningependekeza na kushauri kwamba pawepo na mikakati ya makusudi kuhakikisha kwamba kwa kiwango kikubwa tunatengeneza kahawa hii ili tuwe tunauza mali yenye thamani kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, suala hili la masoko vile vile naomba tukubaliane kwamba wakulima wetu wengi ni watu wenye elimu ndogo hasa katika fani ya masoko na ikizingatiwa kwamba kwa muda mrefu masuala ya masoko yalikuwa ni masuala ya Serikali. Sasa hivi tunapowaambia wakulima wapate taarifa ya bei ya masoko kutoka kwenye *Internet*, kwa kweli hii inawezekana! Mimi ningeshauri moja ya kazi kubwa ya Wizara hii hasa Kitengo cha Masoko ingekuwa ni kuandaa mikakati ya kuhakikisha kwamba wanatutafutia masoko ya nje na humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi, nilikuwa nazungumza na Ubalizi wa China, wakasema wanashangaa sana wenzetu Waganda wamefungua migahawa yao Uchina na Wachina sasa hivi wanaanza kunywa Kahawa. Sasa je, sisi tunafanyaje?

Kwa hiyo, mimi nikaona ni changamoto kwamba ni vizuri Wizara hii isibaki tu pale Ofisini kwake, lakini iwe na kitengo maalum cha kupita, kufanya mawasiliano na Balizi zetu ili kuweza kupata

soko na vile vile kuweza hata kufungua migahawa katika nchi zile ambazo tunaweza baadaye tukauza kahawa yetu ili tujihakikishie soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo ambalo wenzangu wameligusia ni lile la gharama. Makato ambayo kwa kweli yanamfanya mkulima asiweze kuhudumia zao lake sawasawa. Sisi tunao mfano, kahawa inasafirishwa kutoka Mbinga, inakwenda Makambako. Kila kilo moja ikitoka Mbinga kwenda Makambako unalipa shilingi 30/=. Kadhalika ikilala Makambako kwenye yale maghala, kilo moja inatozwa shilingi 30/=. Sasa nauliza, kuna mantiki gani ya kupeleka kahawa Makambako? Kwa nini kahawa isichukuliwe Mbinga ikapelekwa moja kwa moja kwenye mnada halafu likawa ni jukumu la wanunuzi kuja kusafirisha kahawa hiyo kama vile walivyokuwa wanafanya wakati wanunuzi binafsi walikuwa wameruhusiwa. Kwa hiyo, mimi bado ni ombi langu kwamba ni muhimu kabisa tuweze kuondoa gharama hizo ili mkulima aweze kupata fedha za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, moja ya tatizo ambalo linachangia kuporomoka kwa bei ya mazao Vijijini ni mfumo wa Taasisi za Fedha hapa nchini. Kuna wakati nilisema katika Bunge lako Tukufu kwamba noti ilivyokuwa inasambaa sana katika nchi hii kwa asilimia 56, ni noti ya shilingi 10,000/= na asilimia 28 ni noti ya shilingi 5,000/=. Hii inayobaki ndiyo hela ambayo ni noti ya shilingi 1,000/= na shilingi 500/= na kwenda chini.

Sasa ukiangalia mfumo wa Benki, Benki zote ziko katika Miji. Sasa maana yake nini? Imewahi kutokea kwamba baadhi ya Wafanyabiashara wanadiriki kubeba fedha kwenye magari mpaka milioni 500 kwenda kununua Kahawa. Sasa najiuliza ni Benki gani inaruhusu kiasi hiki cha fedha?

Sasa matokeo yake, fedha huwa hazisambai Vijijini. Kule Vijijini wakulima wanakuwa hawana fedha na wanunuzi wanapokuja, akiwa na shilingi 10,000/= anaweza akanunua gunia la kahawa. Anakwambia moja kwa moja bei ya gunia hili shilingi 10,000/=. Kama hutaki, kula. Bahati mbaya ile kahawa huli. Basi unakubalina na bei hiyo. Kwa hiyo, nashauri kwamba suala la hizo fedha pengine lingiangaliwa upya. Mfumo huu umetupeleka pabaya, watu sasa hawatumii hundi. *Negotiable instrument* haziheshimiwi tena. Mimi nadhani ipo haja ya kufutilia mbali hizi noti kubwa kubwa badala yake tuongeze kwa kiwango hiki hizi hizo hela ndogo ndogo kama shilingi 500/= ili ziweze kusambaa vijijini. Mtindo huu utawafanya sasa wakubwa wanaotorosha fedha au kufanya Benki zao za chini chini, wakome.

Kwa hiyo, hili suala sio dogo na mimi ningeshauri kabisa wenzetu wa fedha waende huko Vijijini waone jinsi gani noti ya shilingi 1,000/= inavyoweza kumsumbua mtu kupata *change*. Hali ni mbaya sana. Matokeo yake tunarudi kwenye uchumi wa ujima. Mtu anachukua ng'ombe, anakwenda kutibiwa hospitali kwa sababu hela hamna. Hii nadhani ni uchumi wa hatari sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa ni vizuri tukautazama huo mfumo kwa makini zaidi ili tuelewe na huo mfumo wa ujima au *barter system* kwa sababu tutakuwa tunajidanganya kwamba uchumi wetu unaendelea kumbe tunarudi kwenye uchumi wa mwaka 1947.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema tena, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpa pole nyingi Mheshimiwa Waziri, *Sir* George Kahama na familia yao kwa msiba mkubwa waliopata, Mungu ampe subira.

Napenda kumshukuru Waziri kutokana na umuhimu wa ushirika kwa nchi nzima, badala ya kuunda Benki Maalum ya Ushirika ambayo itakuwa ni gharama kubwa sana na mzigo kwa Watanzania, afadhili utaratibu wa kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika, yalazimishwe Mabenki yetu ya Tanzania hasa *NMB, NBC, CRDB, PBZ* na kadhalika wavipe Vyama vya Ushirika na *SACCOS*. Hii itasaidia

kupunguza gharama zisizo za lazima za kuanza *Giant* mwingine. Nina hakika tukishirikisha *BOT*, basi hili lingeweza kutekelezwa na kuratibiwa vizuri tu na Mabenki yetu haya ambayo tayari yana mtandao mkubwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua katika fedha za *STABEX* zilizokuja Tanzania ni ngapi zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya kuendeleza zao la Karafuu? Ningefurahi nikielezwa kwa miaka tangu mwaka 1995.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampa pole sana Mheshimiwa *Sir* George Kahama, kwa msiba mkubwa aliopata wa kupoteza kijana wake tarehe 19 Julai, 2003. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo wa kuwakomboa wakulima na hivyo naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kuweka sawa yafuatayo:-

(i) Mikopo inayotolewa ielekezwe kwa wingi kwa Vyama vya Wanawake vya Ushirika (*SACCOS* na Kuweka na Kukopa) na vinginevyo, kwa sababu wanawake wakisimamiwa vizuri katika Vyama vyao hurejesha mikopo bila ubadhirifu wowote. Sina maana wanaume wasipewe mikopo la hasa, ila wanawake ni waaminifu sana.

(ii) Wizara iweke utaratibu wa kuhakiki ubora wa bidhaa na kutoa ushauri na elimu kwa wananchi ili wanapopeleka sokoni mtu asipunjwe bei kwa mapungufu ya ubora wa bidhaa zake. Pia itaepusha chuki kati ya muuzaji na mnunuzi wa bidhaa. Kwa hiyo, elimu ya ushirika itolewe kwa wananchi ili wajue wanachofanya kitawaletea uchumi wa uhakika kwa kujua gredi za bidhaa zao na kadhalika.

(iii) Bei za bidhaa zizibitiwe kwa mazao yote siyo kiholela kwa misingi tu kwamba tuna soko huria. Mwenendo huu unavunja uhai wa Vyama vya Ushirika na kuwapa uwezo mkubwa watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namalizia hapo na kuunga tena mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Ushirika na Masoko, na nimpongeze kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara na Serikali kwa ujumla wake wafuatilie tena karibu sana suala la Kiwanda cha *TANICA*, Bukoba kwa lengo la kukibinafsisha kwa mwekezaji mwenye uwezo wa kusindika kahawa yote inayozalishwa Mkoani Kagera. Maana Uganda wanajenga kiwanda kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la msingi zaidi ni kuwa kwa kusindika Kahawa yote inayozalishwa Kagera kunaweza kuongeza bei ya Kahawa zaidi ya mara 30 kwani soko la *AGOA* lipo, vinginevyo bei ya Kahawa ya Kagera zitabaki chini wakati zile za Kahawa ya Uganda zitakuwa za juu zaidi, hii itasababisha ghasia Mkoani Kagera.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimpongeze mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache ya kuchangia katika hoja hii, nayo ni kuhusu wanunuzi binafsi wa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na utaratibu wa kuwapa vibali wanunuzi binafsi, tatizo langu ambalo hata mwaka jana nililieleza kwa maandishi, ni mtindo unaotumika kununua mazao.

Wanunuzi binafsi wanakwenda nyumba kwa nyumba na mlango kwa mlango katika kununua mazao. Wengine wanaojali wamefungua vituo vyao binafsi vya kununulia mazao. Hii inadhoofisha wakulima na hakuna faida inayobaki katika kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa mara nyingine ni kwamba vituo vyote vya ununuzi wa mazao vifungwe. Wanunuzi wote wawe na kituo kile kile cha Chama cha Msingi cha Ushirika. Iwapo Chama hakina fedha, wanunuzi binafsi watanunua. Lakini kusiwe na vituo tofauti na vile vya ushirika katika Chama cha Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida inayotarajiwa ni pamoja na udhibiti wa mazao yote yanayozalishwa katika kijiji/eneo hilo. Pili, kijiji kitaweza kukusanya mchango wa maendeleo kutoka katika kilo ya mkulima, kama Vyama vya Ushirika vifanyavyo. Tatu, wakulima wataweza kupata malipo ya pili, sawa na wale waliouza kwenye Vyama vya Ushirika. Nne, Vyama vitalipwa pango (japo dogo) kutoka kwa wanunuzi binafsi. Tano, wakulima watajenga imani na mfumo wenyewe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hasara nyingi tunazopata kutokana na kuwaacha wanunuzi binafsi waendeleo kununua mazao huria, mfano kununua bei ya udanganyifu kwa wakulima, kukwepa kulipa pato la kijiji na hata kununua mazao yasiyofikia kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nisiache kulizungumzia ni kuhusu *STABEX*. Ni kweli tunahitaji kuboresha miundombinu na kufanya utafiti wa mazao hasa ya biashara lakini ni kwa kiwango gani mkulima anafaidika hasa yule auzaye katika Chama cha Msingi cha Ushirika, lisiachwe hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Kilimo na Chakula waone uwezekano wa kupeleka *STABEX* moja kwa moja kwa mkulima binafsi. Ukizingatia maoni yangu yaliyotangulia, utanikubalia kwamba inawezekana. Wakulima sasa wamekata mibuni, hawalimi pamba ipasavyo na kadhalika kwa sababu ya malipo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia uboreshaji wa soko la mazao ya mkulima lifanyiwe kazi zaidi. Tanzania bila mazao ya biashara kuongezeka, uchumi wetu utayumba. Wanaoweza kutusaidia katika hili ni wakulima wa Tanzania. Uwepo utaratibu mzuri wa kuwasaidia hasa kupitia huduma za ughani na pia mipango mizuri ya kuwapatia ruzuku iwekwe. Fedha zetu zote za kilimo zisiishie katika utafiti tu, wakulima wafaidike na fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpa pole Mheshimiwa *Sir* George Kahama, kwa msiba wa kuondokewa na kijana wake mpendwa. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri na hotuba safi yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio na maendeleo yaliyoelezwa katika Ibara Na.8 - 10 ya hotuba ambayo kwa Wizara naipongeza, bado mbele yetu kuna kazi kubwa katika kuuendeleza ushirika nchini mwetu. Zipo sababu nyingi ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa miaka miwili tangu kuundwa kwa Wizara ni mfupi sana kuweza kuleta mabadiliko makubwa.

(b) Tanzania ni nchi kubwa, hivyo si rahisi kusambaza maendeleo katika kila sehemu ya nchi hata kama pangukuwa na muda mrefu.

(c) Kwa kuwa Ushirika ulikufa kwa muda mrefu, kazi ya kuufufua itachukua muda mrefu pia, hasa suala la kujenga imani mpya ya wananchi dhidi ya viongozi wao wa sasa.

Kwa hiyo, ingawa Ushirika umeanza kufufuka hasa katika Mikoa ya Kaskazini na Nyanda za Juu, Mikoa mingine ya Tanzania hasa maeneo ya Pwani bado hali haijabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuimarisha ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kupitia *COASCO*, hatua iliyopunguza malimbikizo ya ukaguzi.

(ii) Kwa kuanzisha utaratibu wa elimu ya ushirika shirikishi na kuendeleza elimu ya Maafisa Ushirika wa Wilaya. Ushauri wangu ni kuharakisha uteuzi wa Maafisa ili wawepo katika kila Wilaya bila ya kuchelewa.

(iii) Kwa kuandaa sheria mpya itakayokuwa na kipengele cha Maadili ya Uongozi. Naamini kuwa kutokuwepo maadili kulichangia katika kuporomoka kwa ushirika kabla ya mwaka 2000.

(iv) Azma ya kuanzisha Benki ya Ushirika ni nzuri. Benki hiyo itatatua tatizo la ukosefu wa mitaji kwa wanaushirika. Sasa tutasahihisha kosa la kuondoa sehemu ya ushirika katika *CRDB*.

(v) Kwa kuanzisha Mfuko wa kusaidia ununuzi wa mazao. Ushauri wangu ni kuwa mfuko huu uongezewe uwezo ili usiishie kwenye ununuzi wa mazao tu bali usaidie kutoa mitaji na katika uendeshaji wa bidhaa mbalimbali. Wafanyabiashara wengi katika sekta isiyo rasmi wanashindwa kuendelea kwa sababu ya ukosefu wa fedha na ujuzi wa kuendesha biashara zao. Lakini hii ni sekta inayokua haraka. Tukiisaidia kwa mitaji, mafunzo na kuipatia masoko, mchango wake kwenye uchumi wa Taifa utakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa soko kwa bidhaa zetu nyingi ni moja ya matatizo makubwa ya uchumi wetu. Pamoja na jitihada za Wizara kulitatu tatizo hili bado ni kikwazo kikubwa. Kwa bidhaa zetu kubwa za kilimo (Kahawa, Pamba, Chai, Korosho hata Madini) tuna kazi kubwa ya kufanya katika kutafuta masoko mapya na bei za kuridhisha. Kwa kuwa hatuna uamuzi wa mwisho katika kupanga bei, njia za kujiokoa ni kuzitangaza bidhaa zetu kwa nchi mbalimbali na kuongeza ubora wa bidhaa hizo ili ziweze kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei, tuweke mifuko ya kufidia bei kwa wazalishaji wetu waratibu kwenye masoko ya dunia zinapoporomoka. Yapo mazao ambayo hayana walaji wengi hapa nchini lakini hatuwezi kuyasafirisha nje. Mfano ni matunda mengi. Tubuni mbinu za usagishaji ili tuweze kuuza nchini na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yetu ya vijijini tunawahamasisha wananchi kujiunga kwenye vikundi ili wazalishe bidhaa mbalimbali. Lakini wananchi hao wanapozalisha wanapambana na matatizo ya ukosefu wa mitaji, ujuzi mdogo wa kuendesha biashara na ukosefu wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili wananchi waendeleo kupokea ushauri wetu hapanabudi tuwatatule matatizo hayo. Kwa hiyo, Wizara itilie mkazo upatikanaji wa masoko, mafunzo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na kuwapatia mitaji. Ndiyo maana naipongeza Wizara kwa mpango wa elimu shirikishi, uanzishaji wa Benki ya Ushirika na Mfuko wa Mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni yangu, napenda nikuhakikishie kuwa naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nichukue fursa hii kumpa pole Mheshimiwa *Sir George Kahama* na familia yake kwa kifo cha mtoto wao mpendwa kilichotokea huko Afrika ya Kusini, naungana nao katika muda huo wa huzuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa makini na umahiri makubwa, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hata hivyo naomba nichangie maeneo machache kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kufufua ushirika inaenda kwa kasi ndogo hasa ikizingatiwa kuwa watumishi na viongozi bado wale wale walioshiriki kudhoofisha/kuua ushirika, licha ya Wizara kuundwa upya. Nashauri Serikali iwatangaze viongozi na watumishi hao kuwa wameshindwa kazi na waondolewe. Inaudhi pale viongozi hao wabadhirifu wanapotamba na kuwanyanyasa wanachama wa ushirika kwa sababu ya jeuri ya fedha walizoiba na wanazoendelea kuiba. Fedha hizo za wizi ndizo zinatumika kutoa hongo hata kwa Wakaguzi wa Vyama vya Ushirika. Matokeo yake hakuna mtu anayewajibika kwa maovu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo viongozi ndani ya ushirika ambao wanawahifadhi, kuwashabikia na kuwapa umaarufu bandia watumishi/viongozi hao waovu. Ni wakati muafaka, Serikali sasa ikawa wazi bila kuonea au kuogopa katika kuwaadhibu viongozi wanaohujumu jitihada za kuanzisha na kuimarisha ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wakulima ni moja ya maeneo yenye ufanisi unaolegalega hapa nchini. Imefika wakati Serikali itambue kuwa wengi wa wakulima Watanzania ni watu wenye elimu ndogo sana. kwa hiyo, ni dhahiri kuwa uwezo wao katika kutafuta masoko kutumia utandawazi bado ni mdogo. Nashauri, Serikali iimarisha eneo la utafutaji masoko ya bidhaa hapa nchini na nje, hasa mazao yanayolimwa kwa ajili ya biashara hususani kahawa, korosho, katani na chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya majibu niliyopata kutoka kwa Naibu Waziri, bado nasisitiza kuwa hakuna mantiki ya kupeleka Kahawa ya Mbinga, Makambako kwa gharama ya mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanunuzi binafsi wananunua Kahawa Mbinga, wengi walikuwa hawapitishi Kahawa waliyoinunua Makambako kwa sababu ya kuogopa gharama za usafirishaji na utunzaji fedha hizo ni nyingi.

Kwa hiyo, kama Bodi ya Kahawa inalazimisha basi gharama hizo ilipie yenyewe, nashauri Serikali ikubali kahawa ya wakulima wa Mbinga *sample* ipelekwe moja kwa moja kutoka Mbinga na mfunuzi awe na jukumu la kuisafirisha kutoka Kiwandani Mbinga (*Ex-factory*).

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Vyuo. Pamoja na kwamba yapo matatizo ya kibajeti lakini angalau mmeonyesha mfano mzuri kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya madeni ya Vyama Vikuu vya Ushirika ikoje? Serikali inachukuliaje suala la wakulima wa Pamba wanaodai malipo yao kwa Pamba ya mwaka 1989 hadi 1990?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi unaosema: “Soko Huria ni Shetani.” Ushetani unakuja kutokana na ununuzi wa mazao hafifu na kupeleka nje. Hii hali itapelekea bidhaa na mazao hafifu yenye ubora wa chini kabisa na kupunguza heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Bodi za Mazao kama za Pamba, Mkonge, Kahawa, Pareto na kadhalika zipo chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula? Ninapendekeza kuwa Bodi hizi za Mazao ziwe chini ya Wizara hii.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake kuendeleza Wizara hii.



Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, zao la dengu lenye soko lake nchini India na linalolimwa Mikoa ya Singida, Shinyanga, Arusha, Manyara na Tabora lipewe kipaumbele katika kuhakikisha wakulima hawapotezi ari na wanapata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, zao la alizeti lifanyiwe utafiti kuboresha mafuta yake ili kuongeza thamani na kuuza masoko ya nje.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na ninashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si sahihi kuchanganya Ushirika na *Private Enterprises*. Lazima mmoja atakwama hasa ushirika ambapo maamuzi yake mpaka yapite kwenye mkutano mkuu, Wizara ione namna gani tatizo hili linaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika katika *WCGA* vya Pamba ni sharti warudie utaratibu wa zamani wa kununua pia mazao mengine (*mixed produces*), hii itawaongezea mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vema *Distribution Department* zirudishwe katika shughuli za ushirika hii husaidia maana mtu hata kama ameua kondoo, mbuzi ama ng'ombe Ushirika utapata fedha zake na kupunguza gharama za ushirika. Wanunuzi wengine wa pamba wanazo biashara nyingine zaidi na hii inawawezesha kuwa na mapato ya ziada. Ufanywe utafiti ili Vyama Vikuu viweze kuwa na biashara hizo tena. Wakati mwingine hata importation ya baadhi ya bidhaa kutoka nje kama inabidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiwa Mhasibu Mkuu wa *SHIRECU (1984) Ltd* nilianza kuagiza kutoka nje vitu kama basikeli, mabati na sukari ilisaidia sana lakini baada ya *Distribution* kupungua wakati pamba siyo nyingi ushirika huwa unayumba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia utekelezaji mwema wa malengo mliojiwekea.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono haja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma unalima sana mazao ya karanga, alizeti na ufuta, tatizo kubwa ni soko la kuuza mazao haya ya biashara ili wananchi wainue kipato chao. Je, Serikali ina pango gani wa kuwatafutia soko la uhakika la kuuza mazao yao wananchi wa Mkoa wa Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali itaunda lini Bodi ya Mazao Mchanganyiko kama vile karanga, alizeti, ufuta na kadhalika ili kuendeleza mazao hayo katika Mkoa wetu wa Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaajiri Maafisa Ushirika 300 kama ilivyoahidi ili wapelekwe vijijini kuendeleza sekta ya Ushirika?

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri ni nzuri na imeonyesha mipango madhubuti ya kuendeleza ushirika na masoko nchini. Ninaunga mkono hoja ya Waziri mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika Ibara ya 41, Mheshimiwa Waziri anazungumzia juu ya maandalizi ya mpango wa kukibadili Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo

Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Utaratibu wa kuwa Chuo Kishiriki ni utaratibu uliopitwa na wakati. Chuo cha Ushirika Moshi chenye kina uwezo kitaaluma na ki-*organization* kuwa Chuo Kikuu kamili. Utaratibu wa kupachika Chuo kimoja kwa kingine ni utaratibu ambao ni wa gharama isiyo ya lazima na unaongeza urasimu. Ni kielelezo cha uvivu wa kufikiri na wa ubunifu. Ni dalili za kukwepa kujitegemea na badala yake kutafuta njia rahisi ya kukifanya kuwa kishiriki. Kijiografia Moshi na Morogoro ni mbali mno kwa Chuo cha Ushirika Moshi kuwa sehemu ya Chuo cha *SUA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha mambo mawili, kwanza, vyuo ambayo sasa ni Vishiriki vimeshindwa kabisa kujitegemea kama Muhimbili na Ardhi. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sababu ya majukumu yake mengi hakina muda wa kulea Vyuo vingine na hivyo imevifanya Vyuo hivi kudumaa.

Pili, vyuo vilivyoanza kwa kujitegemea kama *Mzumbe University, Saint Augustine University of Tanzania* Mwanza na kadhalika vimeonyesha mafanikio makubwa na mifano ya kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sikubaliani kabisa na wazo la Chuo cha Ushirika kuwa Kishiriki cha Chuo Kikuu cha *SUA*. Tena ukweli ni kwamba Chuo cha Ushirika ndicho kilichoanza kuanzishwa kabla ya *SUA*. Ni aibu kwa Baba kushirikishwa kwa mtoto. Nitaunga mkono Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu kamili cha Ushirika na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaendelea na hoja hii mpaka mabadiliko yatakapoletwa Bungeni na nitawaomba Wabunge wengine waniunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uundaji wa Bodi za Mazao Mchanganyiko ni mpango ambao umechukua muda mrefu. Bodi hii ni muhimu sana sana. Naomba Wizara nayo ione umuhimu wa kuwepo kwa Bodi hii. Bodi za Mazao zimefanya na zinafanya kazi kubwa kuendeleza mazao husika. Kutokuwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko siyo tu kunadidimiza maendeleo ya mazao hayo lakini pia wananchi wanaolima mazao haya hawatendewi haki hata kidogo.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami niruhusu nitoe rambirambi zangu za dhiti kwa Mheshimiwa Waziri *Sir* George Kahama na mama Janet Kahama, kwa kuondokewa na mtoto wao mpendwa. Mwenyezi Mungu atawapa moyo wa subira, waelewe tu kwamba *Allah* ndiye atoaye na ndiye anayetwaa, poleni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niungane na wenzangu waliochangia kumpongeza yeye binafsi na Naibu wake kwa kazi kubwa na jitihada walioifanya kusimamia Wizara hii mpya na kwa kweli ni moja kati ya Wizara muhimu kwa nchi yetu hii kiuchumi. Bila ya Wizara hii ni vigumu kuratibu uuzaji wa bidhaa na masoko hasa ukizingatia wakati wetu huu wa uchumi wa utandawazi. Hapana shaka wazalishaji na wakulima sasa wana pa kukimbilia na wa kumda baada ya kuzalisha viwandani au bidhaa za kilimo pale wanapokosa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niruhusu vile vile kuwapongeza watendaji wa Mheshimiwa Waziri kama vile Katibu Mkuu na Wakurugenzi mbalimbali wanaoongoza taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesema kuwa biashara za nje ni suala la Muungano. Nataka nifahamishwe Waziri amesaidia vipi kutafuta soko la karafuu bidhaa ya biashara kwa SMZ?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada za pamoja wanazochukua baina ya Wizara yake na Wizara mbalimbali Zanzibar kama vile Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika na Wizara ya Biashara na Viwanda ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri apokee pongezi maalum kwa hilo. Kwa kukutana na Mawaziri wenzake wa Zanzibar ni kuonesha ukomavu wake wa kisiasa wa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemshauri katika wakati wake wa faragha awafunze na kuwashauri Mawaziri wenzake juu ya umuhimu wa suala hilo kwani yeye Mheshimiwa *Sir* George Kahama, anafahamu tofauti na wenzake kwa kuwa kukua kwa uchumi wa Zanzibar ni kukua kwa uchumi wa Tanzania kwa jumla na kinyume chake ni matatizo ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako, ningemsihi Mheshimiwa Waziri aendelee kushirikiana hasa Wizara ya Biashara na Viwanda na Masoko katika kukuza biashara na maingiliano yatakayojitokeza kwenye soko la Afrika ya Mashariki (*EAC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa hivi karibuni Novemba, 2003 tutaanza kutumia *East African Common Tariff* na kwa maana hiyo mzunguko mkubwa wa biashara kuwa baina yetu bila ya kusahau kuwa wenye viwanda ndio watakaofaidika kwani soko hilo na wasionavyo kama Zanzibar tutakuwa wasindikizaji.

Kwa umahiri wake Mheshimiwa *Sir* George Kahama, alitakiwa aishike mkono Zanzibar kwani hata kimapato sisi tutakuwa si wapataji bali wanunuzi. Hilo nalo ashirikiane na taasisi za biashara tukiwa kwenye kivuli cha Muungano atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua fursa hii kuwapongeza kwa uamuzi wenu wa kuhamia Makao Makuu Dodoma.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kwa niaba ya wapiga kura wangu na mimi mwenyewe kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa *Sir* George Kahama na mkewe Mheshimiwa Janet Kahama, kwa msiba mkubwa uliowapata wa kuondokewa na mtoto wao mpenzi Kiiza Kahama, aliyefariki huko Afrika ya Kusini. Mwenyezi Mungu amuweke marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika sehemu mbili tu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ushirika na Masoko, kwa kuchukua hatua thabiti zinazopelekea katika uanzishwaji, kama anavyosema katika hotuba yake wa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika ni matarajio ya watu wote hususan wale wapendao kilimo kwamba uanzishwaji wa Benki hii utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wakulima ambao wataweza kujipatia mahitaji yao ya mikopo kwa ajili ya kuendeshea kilimo chao kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Benki hiyo zitaweza kurahisishwa endapo hatua za makusudi kabisa zinachukuliwa hivi sasa kuwahusisha wakulima kwa kupitia Vyama vyao vya Ushirika, Vyama vya Akiba, *SACCOS* pamoja na Benki za Ushirika kama ile ya Kilimanjaro na Kagera. Kwa kushirikisha na kutumia mtandao huu wa Taasisi hizo ninaamini gharama za uendeshaji wa Benki zitakuwa ndogo na hivyo kuiwezesha kutoa mikopo yenye unafuu wa riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kutumia Taasisi hizo hata ulipaji wa madeni utaboreka kwa vile huko chini wanachama wote wanajuana na wataweza kubanana vilivyo katika ulipaji wa madeni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. Kwa niaba ya wakulima wa Ruangwa, naomba Wizara ilitazame Jimbo hili kipekee. Vyama vyetu bado dhaifu na ni vichache, kwa hiyo basi, vinahitaji msaada kutoka juu katika kusimamia na kutoa miongozo katika kuanzisha Vyama vipya hususan Vyama vya Akiba na Kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtaalam angalau mmoja afike Jimboni atusaidie katika suala hili. Mimi mwenyewe naahidi kutoa kila msaada uwezekano ili kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko na kumtakia afya njema ili ahitimishe shughuli zake.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Balozi *Sir* George Kahama, Waziri wa Wizara hii, pamoja na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri na Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri Wizara mambo mengi lakini kwa leo ninashauri maendeleo ya Vyama vya Ushirika yatiliwe mkazo, wakulima wapatiwe mikopo bila ya urasimu mkubwa na riba nafuu, Serikali isikubali kwa urahisi kuchukua madeni ya shilingi bilioni 22 ya Vyama vya Ushirika kwa Mabenki ya Biashara, badala yake mabenki yasamehe madeni hayo, ikiwa Mataifa ya nje yanatusamehe iweje sisi wenyewe kwa wenyewe tudaiane, Wizara ifanye utafiti kwa nini Tanzania hatujanufaika na fursa ya *AGOA, EBA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeze Wizara kwa ushirikiano mzuri uliopo baina yao na Wizara ya Biashara Zanzibar na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika (SMZ).

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa vema fedha za *STABEX* zingeweza kulisaidia zao la Karafuu ambalo limeathirika na soko duni la ulimwengu hata kuwafanya wakulima kuvunjika moyo kama ilivyo kwa zao la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Ahsante sana.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeze Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya 2002/2003. Mungu awajalie wafanye kazi nzuri zaidi 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwatafutie soko wakulima wa Tangawizi katika Jimbo langu la Kasulu Mashariki. Kwa miaka mitatu mfululizo wamekosa soko lakini hawajakata tamaa wanaendelea kulima. Tafadhali tuwasaidie. Ahsante.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mapema kabisa napenda kuweka msingi mkuu wa mjadala wangu kama ifuatavyo:-

(a) Tanzania inategemea kilimo kwa maendeleo ya uchumi wake, kilimo hicho ni cha wakulima wadogo wadogo.

(b) Wakulima popote hawapokei mabadiliko yoyote kwa urahisi sababu kazi yao haina *security*.

(c) Kwa wakulima wa Tanzania mabadiliko hayakubaliki kwa urahisi sababu wamepatwa na majanga kama maduka ya Vijiji kuliwa na pia Vyama vyao vya Ushirika kuliwa.

(d) Wakulima wa Tanzania wamekata tamaa sababu hawaoni nani ni kinga yao ya kukimbilia. Hivyo wameamua kujilinda wenyewe kwa kuunda Sungusungu na kuachana na mazao yanayowaweka katika hatari ya kupoteza nguvu zao bure. Wanaachana na kilimo cha mazao yanayoitwa ya biashara.

Wizara ya Ushirika na Masoko, inalo jukumu la kwanza kutafuta dawa ya kuyatoa matatizo niliyoyaaanisha juu. Wizara inakabiliwa na tatizo la kujenga uongozi mzuri wa Vyama vya Ushirika toka Msingi, *Union* hadi *Appex* ambako kumejaa walaji. Mkulima wa Tanzania anahitaji msaada wa Wizara hii kwa sababu wajanja hawa wanatumia *Rochidale humiples* kwa manufaa yao. Kama chama ni cha wanachama hivyo kisiingiliwe kwa vyovyote ikiwa ni pamoja na wanachama kuwachagua viongozi wao. Viongozi wabovu (wezi) hung'ang'ania kanuni hii na kuwahadaa wakulima ili waendeleo kuchaguliwa na waendeleze ulaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yanayolima pamba kama Shinyanga na Tabora yameathirika na wananchi ili wajitete utetezi wao ni kuachilia mbali kilimo cha pamba. Inabidi Wizara izingatie hili kuwa Vyama kama *IGEMBENSABO* havitafufua kilimo cha pamba na iwapo hakitafanyika chochote kuweka uongozi mpya la sivyo mtakubaliana na wakulima kuwa wakikopeshwa fedha ati wanunue pamba sehemu ya fedha itatiwa tu naogopa sana. Kileeni chama hiki kwa kukipelekea Meneja Mkuu Mlezi toka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii kwa kweli imekuwa ngumu kiuendeshaji kwa sababu ya historia ya ushirika wenyewe ulivyoweza kubadilishwa badiilishwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kwa kuwa taratibu za uundaji wa ushirika hapo nyuma ulivyofuata misingi ya siasa, naomba sana ushirika utakaoendelea kuundwa kwanza uzingatie taratibu za uundaji wa ushirika ambao ni wa kuzingatia taratibu zinazofuatwa za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunavyo Vyama vya Ushirika mbalimbali katika nchi yetu, ushirika kwa ujumla umezorota kama nilivyoanza ni kwa sababu nyingi za kihistoria. Ushirika na Muungano wa watu kwa hiari yao wenye dhamira moja, ili waweze kutatua matatizo yao kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo nimeliona limekuwa likisumbua sana, mfano, ushirika wa wakulima wa tumbaku kwa sababu hivi ndiyo Vyama nilivyonavyo katika Wilaya yangu hususan Jimboni kwangu. Wakulima wanalazimika kujiunga bila kujua lolote ili waweze kuuza tumbaku yao. Baada ya kuuza Tumbaku yao hawaoni maana ya kuendelea kuzungumzia masuala yanayohusu maslahi ya chama chao. Kwa kuwa sasa kutakuwa na mabadiliko tena mwaka huu 2003 ya sheria ya ushirika pengine itakidhi haja ya kuwa na ushirika ulio imara na utakaofanana na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wangu ushirika unaendelea vizuri, lakini nimpongeze Afisa Ushirika wa Mkoa wa Rukwa Ndugu Kasya, kwa juhudi zake za kufufua na kuendeleza ushirika katika Mkoa wetu. Kwa kuwa afisa huyu anaonyesha kuipenda kazi yake na pengine kuifanya vizuri sana, naomba Serikali iangalie namna itakavyomsaidia zaidi katika utendaji wake mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Afisa Ushirika anatakiwa kutegemea *funds* za *RAS* lakini ninapendekeza kama ilivyofanyika hapo nyuma, Wizara ingefanya maandalizi ya kufufua ushirika katika nchi yetu, kama programu maalum magari yatafutwe kupitia wafadhili na fedha za kujikimu watumishi hao, watumishi waongezwe ili kukidhi haja ya kusimamia Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wa Vyama vya Ushirika waelimishwe kwa nguvu zote, tukizingatia kuwa ushirika ndiyo chombo pekee kitakachowaondoa wananchi kwenye unyonge na ukizingatia hii ni Ilani ya CCM inayotakiwa kutekelezwa kwa nguvu zote. Kuundwe vyombo vitakavyosaidia kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika kwa mfano, *Cooperative Banks* zitakazotoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wote wa Vyama vya Ushirika wachukuliwe hatua mara tu watakapobainika kufuja mali ya chama, katika hili napenda nitoe mfano kwa viongozi wote waliofuja mali katika katika Vyama vya wakulima huko Jimboni kwangu. Afisa Ushirika alifanya ukaguzi na kutoa taarifa na hivyo kuwafanya Halmashauri kuwashtaki watendaji hao. Hili ni jambo la kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini sote tukiimba wimbo mmoja kwamba tunajenga ushirika ni imani yangu kuwa tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuwapongeza wote waliomo katika Wizara jinsi wanavyojitahidi kusaidia katika kuhakikisha kuwa ushirika unafanikiwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuwapongeza kwa kazi zote. Hata hivyo nina maswali:-

(a) Kutokana na azma ya Bodi ya Pamba kufanya kampeni ya kuongeza uzalishaji wa zao la pamba. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vya nguo ndani ili kuongeza wigo wa soko? Je, Wizara yako ipo tayari kuwa na vyombo (mashine) za kuchambua pamba ili mkulima auze pamba na mbegu tofauti tofauti?

(b) Katika zao la Tumbaku ambalo hukopeshwa na wanunuzi na kulipa deni hilo kwa riba (*interest*) kubwa, je, Wizara ina mpango gani wa kuwapa fedha za mkopo kama vile za kahawa (*STABEX*) ili kuwaepusha na riba kubwa wanayolipa kwa wanunuzi na wawe huru kuuza kwa mnunuzi yeyote?

(c) *Exim Bank* na *KNCU* ndizo zilizopewa fedha za kukopesha kwa ajili ya pembejeo. Kwa nini Wizara isitumie Benki zenye mtandao hadi Vijijini kama *NBC*, *NMB* na *CRDB*? Hivi hii *Exim Bank* ni ya nani?

(d) Wizara itafute soko la mchele hasa wa wakulima wa Manonga ili kuwaondolea kupunjwa na wafanyabiashara. Nawataki kazi njema.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa jitihada zao za kuimarisha ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 37(vii) ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetolewa orodha ya Vyama vya Ushirika vilivyofanyiwa uchunguzi kwa nia ya kutatua migogoro. Miongoni mwa Vyama hivyo ni *MICU*. Naomba nipewe taarifa ya uchunguzi wa Chama cha Ushirika cha *MICU*, pamoja na ushauri jinsi ya kukiimarisha chama hicho. Kama inavyofahamika, chama hiki ni kichanga na tunahitaji msaada na ushauri wa karibu kutoka Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika aya ya 24 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri yametolewa maelezo kuhusu tatizo la soko la Pareto. Tathmini imefanyika na kuainisha vyama kadhaa vya msingi vitakavyopatiwa mikopo katika msimu huu. Wilaya ya Ileje tunalima Pareto maeneo tunayopakana na Wilaya ya Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wakulima wa Pareto Wilayani Ileje watasaidiwa kuuza Pareto yao kama majirani zao wa Mbeya Vijijini? Tunaomba msaada wa Wizara katika suala hili ambalo ni tatizo sugu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kutoa salaam zangu za rambirambi kwa Waziri wa Ushirika na Masoko Mheshimiwa *Sir* George Kahama, pamoja na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa msiba wa mtoto wao mpendwa Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimpongeze Waziri na hotuba yake. Vile vile naomba kuwapongeza watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi ngumu wanayoifanya kujaribu kupambana na umaskini.

Kwa kuwa mojawapo wa kazi za Wizara hii ni kusaidia Vyama vya Ushirika kupata mitaji endelevu ikiwa ni pamoja na kusaidia kuvikutanisha na vyombo vya fedha na inapobidi kuvidhamini kwa ajili ya kupata mikopo na kuviwezesha vyama kukidhi haja za wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi namwomba Waziri na Wizara yake waone umuhimu wa kukisaidia Chama cha Ushirika cha UKI kilichopo Kibondo kwa kukidhamini ili kipate mkopo kwa ajili ya kununulia *containers* zenye ubora wa kuhifadhi na kusafirishia asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo soko kubwa la asali Afrika ya Kusini, Germany na Waingereza shida yetu ni ubora. Ili kufikia ubora tunahitaji fedha. Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wananchi kufikia ubora huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wananchi wapatiwe mikopo itakayowasaidia kufikia ubora unaohitaji. Fedha hizi zikatwe baada ya mauzo. Ili kufikia ubora ziko mashine za aina mbili ambazo zinapatikana Uingereza kwa bei nafuu sana. Mashine za umeme ni *USD 5,000* na zisizo za umeme ni *USD 1,000* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi zikinunuliwa na kusambazwa zitawasaidia wananchi. Vile vile upimaji wa ubora wa asali unahitaji fedha. Hivyo ni imani yangu kwamba mikopo ikipatikana zao la asali litasaidia kuinua uchumi wa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wataalam wa Wizara hii waende Vijijini ili kutoa ushauri kwa wananchi kusudi waweze kuanzisha Vyama vya Akiba na Mikopo ambayo vitawasaidia wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nikitegemea Wizara kuwasaidia wananchi kupata mikopo ya kuwawezesha kufikia soko la mazao yao.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii toka Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wanavyowajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara hii mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara za kutoa mafunzo kwa wananchi, ningeshauri utaratibu wa kutoa mafunzo kwa njia ya Posta urudishwe ili kutoa nafasi kubwa ya kujifunza kwa wananchi maana ya Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utafiti ni muhimu hasa kwa mazao ambayo yanaweza kutengenezwa pombe za kigeni kama bia na kadhhalika ufanyike kwa mazao kama ulezi na kadhhalika badala ya kutumia ngano na shayiri peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wizara kutoa mafunzo kwenye vikundi vya uzalishaji mali na kuvikopesha, nashauri Wizara ipanue uwezo wake ili wananchi wafaidike na mpango huo na hasa Kituo cha Ushirika (Tawi) kilichopo Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Wizara kuhamasisha wananchi kujianzishia vikundi na kuweza kusindika mazao yanayolimwa katika maeneo yao, ombi langu kwa Serikali ni kuviwezesha vikundi kupata mkopo ili kuvipa uwezo wa kuendeleza kazi zao hasa kwa Mkoa wa Dodoma. Tunahitaji mashine ndogo za kusindika maziwa, karanga na kadhhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoona katika orodha ya idadi ya Vyama vya Ushirika kwa sasa vinaongezeka siku hadi siku ningeshauri kama ikiwezekana kila Mkoa uanzishe Vyama vya Ushirika katika Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumsaidia mkulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera ambaye bei ya kahawa imekuwa ya chini mno, kuna haja kubwa ya Serikali kuhakikisha Kiwanda cha *TANICA* ambacho kimeshatangazwa kuuzwa na hatua zipo ukingoni, kiwanda hicho kiuzwe kwa wanaushirika wa *KCU* ambao hivi sasa wanamiliki asilimia 34 ya kiwanda hicho. Hatua hiyo itasaidia *KCU* kuuza zaidi nje *processed coffee* ambayo ina bei kubwa zaidi na hivyo kuwasaidia wakulima kupata pato zaidi na bei zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ijikite zaidi katika kuongeza *network* ya kuwawezesha wananchi kuelewa mwenendo wa masoko ndani na nje. Kuanzishwe vituo vya upashanaji habari za masoko angalau katika kila Makao Makuu ya Wilaya na Vituo/Miji ya kibiashara kama vile Isaka, Makambako na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, itolewe elimu zaidi kwa wafanyabiashara itakayowawezesha kuelewa techniques za biashara za kidunia (*Global Business Trend*). Hii itasaidia kuwaongezea uwezo wa kumudu biashara ya kiushindani na mbinu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa *Sir* George Kahama na safu yake nzima ya uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya dira nzuri ya Wizara hii ya kufufua na kuendeleza ushirika, nashauri Wizara ikazanie zaidi masoko, lakini hili halitakuwa bila Wizara hii kupewa nyama zaidi ya kusukuma maendeleo ya masoko na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na *favourable balance of payments* na nchi zingine. Nashauri Wizara hii ipewe pia biashara, kwa hiyo, iwe Wizara ya Biashara, Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2001/2002 sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia tatu wakati sekta ya biashara ilikuwa kwa asilimia 0.3 ikiwa na maana ya kuelezea kukosekana kwa kudhibiti uzalishaji na usukumaji wa mauzo ya bidhaa zinazozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitegemei kila kinachozalishwa lazima kiuzwe bali tu kinachozalishwa kiweze kuuzika zaidi kuliko hivi sasa *through concerted and coordinated efforts* za sehemu zote mbili. Jibu moja ni kukabidhi majukumu haya yote mawili kwa Wizara moja. Kama soko la *AGOA, EAC, EU, Japan* na *SADC* lipo na kwa bidhaa bora hakuna sababu ya kusababisha tofauti hii kubwa kati ya sekta hizi mbili yaani sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri huo hapo juu wa kuhakikisha uuzaji zaidi wa bidhaa zetu basi Wizara hii ingeimarisha maghala Vijijini ili mikopo kwa stakabadhi, programu hii isaidie kupunguza uharibifu wa mazao Vijijini kwa kosa la hifadhi mbovu kwa kukosekana maghala ya uhakika. Hili likichangiwa na usindikaji wa matunda na mboga kupitia mikopo ya *SIDO* basi ujazo wa fedha wa nchi pia utapanda kwa kasi. Huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Waziri *Sir* George Kahama, kwa msiba uliomkuta napenda kuunga mkono hoja ya Wizara yake kwa asilimia mia moja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Maafisa wa Wizara pamoja na wafanyakazi wote. Hotuba hii ni nzuri na ambayo inafafanua vipengele mbalimbali ikiwemo namna ya kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo chemchem ya kuondoa umaskini kwa sababu endapo Wizara hii itasimamia vizuri vikundi vya ushirika, huenda umaskini ukapungua au ukaondoka kabisa. Ni vema Wizara hii ikatilia mkazo vikundi vya ushirika huko Vijijini.



Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifanye ziara Vijijini ili wananchi wafahamishwe jinsi ya kuanzisha mashirika baadaye, baada ya wanaushirika kuzalisha mazao yao Wizara itafute masoko. Vipo vikundi vya akinamama na vijana ambao wameanzisha vikundi vya ushirika lakini vikundi hivyo ni dhaifu kwa sababu ya ukosefu wa elimu wa namna ya kuanzisha vikundi vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, washirikiane ili yapatikane masoko ya uhakika ya kuuza bidhaa zetu kama kahawa, korosho, pamba na bidhaa zingine ikiwemo na kutafuta soko la kuuzia karafuu.

Baada ya kupata masoko hayo, Serikali zote mbili ziwe na uongozi wa pamoja kujadili masuala ya kutafuta masoko ya vikundi vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Waziri *Sir* George Kahama na Mama Janet Kahama, kwa msiba mkubwa uliowapata hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyotoa kwa Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi ya mazao yaliyoko ghalani kama dhamana ya mkopo. Iwapo utaratibu wa malipo taslimu ungezingatiwa kama ndiyo mpango halali kwa mkulima, mfumo huu usingekuwa na maana yoyote kwa mkulima kwani mazao yako tayari yameshatoka shambani na yako tayari kwa mauzo. Hivyo mazao yake kuwa dhamana ya mkopo ni kiini macho wala siyo mkopo halali na kama analipia interest basi ni sawa na kumdhulumu mkulima zaidi ya fikra za kudhani tunamsaidia.

Nashauri kwamba ili kweli tuwe tunatoa mkopo kwa mkulima basi mfumo huo ulenge kumpa uwezo mkulima kupata fedha hizo mapema ili zimsaidie katika kulima, kupalilia, kuweka madawa na kusafirisha mazao yake kwenye maghala. Fedha za malipo ya mazao ya mkulima ziwepo mapema na alipwe mara anapopeleka mazao ghalani na kulipia deni lake wakati huo. Kwa hali hiyo, lazima kiwepo chombo kitakachobeba *risk* ya kukabiliana na bei za soko la nje na sio kumwachia mkulima peke yake *risks* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirika wa Mafundi Seremala - Muheza Mjini. Huu ni ushirika wa zamani sana ambao bado upo hai. Ushirika huu umejitahidi sana kuwa na vifaa bora na kujiendeleza sana.

Hata hivyo, sasa ushirika huo una matatizo makubwa ukiwa ni pamoja na kunyimwa kazi na vyombo vya Serikali ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika huu ulikopa fedha benki na kuanza ujenzi wa jengo kubwa la biashara lenye ghorofa. Kutokana na kazi kupungua ujenzi uliokuwa umefikia wastani wa asilimia 80 ulikwama zaidi ya miaka 15 iliyopita na hivyo *interest* ya mkopo kuwa mzigo mkubwa unaoendelea kutishia kuua ushirika huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya wanaushirika hao kupitia kwa Mbunge wao kuomba msaada wa Wizara angalau kuwatembelea na kuwapa ushauri yaliyotolewa mwaka 2002 hadi sasa bado hayajafikiriwa na hakuna msaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena rasmi Wizara itume viongozi wake kuwapa moyo na ushauri wanaushirika hao. Pia Wizara ifikirie kutoa mapendekezo Serikalini kuhusu mzigo wa *interest*

unaokabili mikopo ya zamani ya wanaushirika wengi hapa nchini ili ikiwezekana vyombo hivi vya Serikali vifikirie kuzifuta kama njia moja ya kufufua ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muheza ni wazalishaji wakuu wa matunda hasa machungwa. Ili kuendeleza umoja wa biashara na kilimo cha matunda wakulima wa Kata na Vijiji vya Mtindiro Wilaya ya Muheza wameanzisha umoja wa ushirika wa wauza machungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa wanaushirika mafundi Seremala wa Muheza Mjini nao pia waliomba kutembelewa na viongozi wa Wizara ya Ushirika na Masoko tangu mwaka 2002, lakini mpaka leo bado hawajaona viongozi wa Wizara. Nia yao ni kupata ushauri wa ziada ili kuboresha ushirika wao mpya. Ziara ya viongozi wa Wizara iwashirikishe wanaushirika hawa na wengine nitakaowataja hapo chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chama cha Ushirika wa Maziwa Mkoa wa Tanga. Chama hiki chenye Vyama vya Msingi vya Ushirika wa wafugaji na wauzaji wa maziwa katika Wilaya ya Tanga Mjini, Muheza na Korogwe kimejiendeleza sana na kufikia kuwa na hisa katika Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha *Tanga Fresh* na pia kuanzisha vikundi vya vijana 300 ambapo chama kimewatafutia ardhi na sasa kinawakabidhi ng'ombe (Mitamba) ili vijana hao waanze kujitegemea. Chama hiki kimekuwa kikisaidiwa na Serikali ya Uholanzi.

Hivi karibuni Serikali ya Uholanzi imejitoa katika kufadhili Vyama hivyo vya Msingi vya wafugaji na kuomba kukabidhi mali zilizokuwepo kwa wafugaji. Katika kuandaa chombo cha kupokea mali hizo Mkoa umenda chombo kipywa kinaitwa *TADAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa chombo hiki kimeanza kuunda vikundi vingine vidogo vidogo kutokana na wanachama vya Vyama vya Msingi vya Ushirika na kuanza kufanya kazi ile ile iliyokuwa ikifanya Chama cha Ushirika na hivyo kuleta hali mbaya ya mgongano ndani ya Wilaya za Tanga, Muheza na Korogwe. Hali hii inatishia maendeleo ya ushirika uliokuwa umekomaa sana. Tunaomba Wizara ya Ushirika na Masoko ifuatilie mgogoro huu kabla hali haijafikia pabaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, mwaka 2002/2003 wakati wa Bajeti niliomba Wizara hii iiweke Wilaya ya Muheza katika mpango wa kusaidia ujenzi wa maghala na magulio ya mazao ya kilimo hasa matunda (machungwa) baada ya kukamilisha mpango uliokuwepo kwa Wilaya za Kongwa (Kibaigwa) na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya mwaka huu 2003/2004, inaonyesha kwamba mpango huo wa ujenzi wa maghala Kongwa na Morogoro utatekelezwa 2003/2004. Hivyo narudia tena kuomba Wilaya ya Muheza ifikiriwe kuokoa matunda yanayoharibika ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi imekuwa ni kawaida ya viongozi mbalimbali kutumia fedha za wakulima ambao ni maskini sana bila ridhaa yao na kuwadhulumu! Ni kwa sababu hizo wananchi wa Moshi Vijijini ambao ni wakulima wa kahawa walipoamua kuachana na CCM na kunituma mimi ili nije kuuliza kulikoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno ya utangulizi ni mazito sana na yanahitaji ufafanuzi ili Serikali kama ilikuwa haijui kisa cha wananchi wale kuwachukia, basi wajue na ikibidi wajisahihishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mazito yenye dhuluma ya waziwazi aidha, ni kwa makusudi au kiseru mimi sijui ila Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko kwa kuwa ni wa muda mrefu Serikalini anaweza akafahamu na kututatulia au kufafanua jambo hili.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi upo kwamba kabla ya Uhuru, shule za Moshi Vijijini zilikuwa zikiongoza Tanzania lakini baada ya Serikali kutuambia tupige *marktime* mwaka 1964 hadi leo hakuna shule inayofaulisha tena na katika shule 7 za mwisho kwa ripoti ya mwaka huu ambayo ninayo

ni za Moshi Vijijini naambatanisha ripoti. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Cynthia Ngoye, ni shahidi baada ya kutembelea eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, achilia mbali kutelekezwa kwa Jimbo hili, mwaka 1988 wakulima waliuza kahawa yao na kawaida walikuwa wanalipwa kiasi na kiasi kinachobaki hulipwa baada ya mauzo ya kahawa hiyo katika soko la Dunia! Mwaka huo fedha iliyokuwa imezidi kwenye mauzo ya *KNCU* ilikuwa shilingi bilioni 1.3! Fedha zilitumwa na kupokelewa na *Tanzania Coffee Board (TCB)* badala ya kuwakabidhi wakulima fedha zao kupitia *KNCU* walipewa nusu y fedha hiyo na nusu nyingine ikabaki huko huko *TCB* na inaaminika kuwa walifungulia maduka ambayo baadaye waliyafilisi wenyewe. Nilipokuja kumda Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni mwaka 2001 aliahidi kuchunguza! Mwaka 2002 nikiwa kwenye Kamati ya Fedha chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge, nilikumbushia tena deni hilo kwa niaba ya wananchi, wakulima wa *KNCU* na ndipo wadau walipoitwa mbele ya Kamati akiwemo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na kukiri madeni hayo pamoja na mengineyo kama nitakavyoeleza hapa!

Kamati iliridhika na kuagiza utekelezaji mara moja na Mheshimiwa Waziri aliahidi kufanya hivyo mbele ya Kamati ya Bunge, baada ya miezi sita, Mwenyekiti, alimwandikia Mheshimiwa Waziri barua kukumbushia kuhusu utekelezaji wa malipo hayo! Naamini hakujibiwa maana hadi sasa bado fedha hizo hazijalipwa kwa maskini hawa!

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 nikiwa kwenye Kamati ya Kilimo, nilikumbushia tena na nikajibiwa kuwa nanukuu: “Mheshimiwa George Kahama, Mbunge na Waziri wa Ushirika na Masoko, alitoa majibu ya Serikali mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara iliyokutana Mjini Dar es Salaam tarehe 2 Juni, 2003 kwa kukiri agizo Na. 2, ahadi ya Wizara kusaidia katika kumaliza tatizo la madai ya Vyama Vikuu vya Ushirika vya Nyanza na *KNCU* kwa bodi ya mazao ya pamba na kahawa itekelezwe mapema. Kamati ya Bunge isingependa tatizo hili lijitokeze tena wakati wa kujadili Bajeti ya 2003/2004.”

Maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kama ifuatavyo, madai ya *KNCU* kwa bodi ya kahawa, Wizara imefuatilia madai haya na kubaini kwamba jumla ya fedha zinazodaiwa na *KNCU* ni shilingi milioni 548. Fedha hizi zinatokana na makato ya fedha za wakulima wa kahawa msimu wa 1988/1989 shilingi milioni 426. Madawa aina ya *Kocide* shilingi milioni 59 na makato kuhusiana na gharama za benki, Bima na Bandari *Clearing and Forwarding Charges* shilingi milioni 63.

Hata hivyo, bodi haikubaliani na *KNCU* kuwa hayo ni madai kwake, (Bodi ya Kahawa) kwa sababu makato hayo kwa wakulima wa *KNCU* ni matokeo ya utekelezaji wa mfumo wa malipo kwa wakulima wa kahawa nchini kama ulivyokuwa umepitishwa na Serikali kuanzia mwaka 1968/1969 hadi 1989/1990 na utaratibu huu ulipatikana kama *Pull System* na kwa hii ni *Pool System* aliendelea kujibu kuwa kutokana na utata uliopo katika suala hili na umuhimu wa kupata maelezo sahihi yatakayowezesha kufikia uamuzi unaostahili, Wizara huteua makampuni mawili ya ukaguzi wa hesabu yanayojitegemea *Independent Auditing Firms* kulichunguza suala hili na kulitolea mapendekezo ili Serikali itoe uamuzi.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwepo kwa deni hilo la muda mrefu na kwamba deni hilo limetokana na *Pool System*, je, mkulima anapata haki gani hapo? Badala ya kumfidia mkulima huyo, hata kile kidogo anachopata anayang'anywa! Je, huyu mkulima ataelewa Serikali? Hapo bado sijainishiwa makato ya benki ambayo *interest* kwa wakati huo ilikuwa asilimia 31.

Mimi sikubaliana na hali hii ya kuwatesa wananchi hawa wa Kilimanjaro kwa kipindi cha *Marketingtime* kimekwisha kwa sasa tumefanywa kuwa wa mwisho Kitaifa. Tuliwakosea nini? Nataka maelezo ya kina au sina sababu ya kutoondoa shilingi kutoka kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na ni pamoja na Naibu Waziri wake.

Nikiingia kwenye sheria za Ushirika ndiyo ulaji mtupu. Siku moja nilikwenda na Afisa Ushirika aitwae Omari kwenye Ushirika wa Shamba la Sangiti ilibidi nitumie uzoefu kumkinga kwani

wananchi walitaka kumpiga. Nilipotaka kujua kulikoni wale Wanaushirika waliniambia kuwa Mwenyekiti wao aitwae Kitau ameshakaa kwenye kiti hicho kwa muda zaidi ya makubaliano na analindwa na huyo Afisa Ushirika. Wenyewe walitaja ubadhirifu mbalimbali aliofanya kwenye Chama ikiwa ni pamoja na kufilisi SACCOS na ni pamoja na kujiuzia tractor zima! Na Tail mpya kwa shilingi 170,000/= tu. Kwa kutumia jina la ndugu yake.

Natoa wito Wizara sasa iweke sheria zinazoendana na wakati na sheria zinazowalinda wenye Ushirika wao, na ni pamoja na kuangalia upya kuhusu ujamaa kwa mfano viongozi wanakopeshana fedha ya wanachama na hazikulipwa! Kama wale viongozi wamekula njama hakuna namna ya kuwashitaki kwani ni lazima Mwanaushirika mwenyewe aende kushitaki na zinatakiwa fedha nyingi kwa Wakili kitu ambacho hawa maskini hawana.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ruzuku kwa wakulima nataka kujua, Serikali ya Tanzania ina mpango gani wa kuwapa wakulima wake ruzuku kama nchi zingine zinatoa ruzuku kutokana na kodi ya wananchi wao, je, kwa nini Serikali yetu isiwe na mpang huo? Nataka jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza sehemu ya fedha zinazotokana na madini yaani Dhahabu, Almasi na Tanzanite itolewe kama ruzuku kwa wakulima wa Tanzania ikiwa ni pamoja na sehemu ya kodi ili tuweze kuendeleza vizuri dhana yetu ya kilimo kuwa Sekta Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hili la mikopo ya benki. Mheshimiwa Waziri anawadhamini wenye Vyama vya Ushirika kukopa katika Benki ya Kibiashara (Commercial Bank) ikiwa na riba kama tu mwenye duka au daladala, wakati Wizara ikijua wazi kuwa deni kama hilo halilipiki kwani mkulima anavuna mara moja kwa mwaka! Lakini fidia hudaiwa kila mwezi au kila siku! Tafuteni njia nyingine kama mnataka kukomboa nchi hii ili iweze kujitegemea.

Mwisho, napendekeza wataalam wa Ushirika watokane na eneo husika kwani pamoja na sheria kunakuwa na uelewa zaidi na uzoefu wa hasa mazao husika hii itapunguza (Over head coast). Kuwe na ukaguzi kila baada ya miezi mitatu ili kuendana na sheria ya fedha ya mwaka 2001 (Procurement Act) kwani hivi sasa wananchi wamekata tamaa na Ushirika pia kusiwe na Ushirika wa kulazimisha, Ushirika uwe na Common Interest kama sheria inavyotaka kutokana na kuwabana na kuwadhulumu wakulima wanalazimika kuweka pamba maji ili kupata uzito zaidi.

Aidha, wanaweka mawe kwenye kahawa ili kuongeza uzito, lakini vyote hivyo huongeza uzito na kuua ubora na hatimaye kupata bei ndogo kwenye soko la dunia kama nilivyoeleza tangu mwanzo Serikali itupie macho Moshi Vijijini kwani ni aibu hawa wananchi wamekuwa wakitii kila kilichoagizwa na Serikali kama vile kuchangia bomba la maji, kuchangia barabara, kuanzisha Ushirika, lakini Serikali imeamua kuwa bubu tuvunje ukimya huo.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza hivi zao la Korosho liko katika mpango wa STABEX? Kama ndiyo, je, fedha hizo zinatumiakaje?

Kama sivyo, Serikali iko tayari ili zao la Korosho nalo liwemo katika mpango huo wa STABEX? Bei ya Korosho ghafi mwaka huu inatarajiwa kuwa shilingi 400/= kwa kilo. Je, bei ya Korosho zilizobanguuliwa ni kiasi gani kwa kilo na je, nchi ina uwezo gani wa kubangua Korosho?

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko na hivyo naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali ya Vyama vya Ushirika nchini. Vyama vya Ushirika bado vinafanya kazi zake kama zimamoto kwa vile havina mitaji na kwa kuwa havina mitaji hata uwezo wa maamuzi unakuwa mdogo. Mikopo inayotolewa kwenye Vyama hivi haizingati msimu wa mazao husika, hivyo inachelewa kiasi cha kuvifanya Vyama kununua mazao machache na kushindwa kufikia malengo. Ushauri wangu ili kuviimarisha Vyama vya Ushirika Serikali ivipatie mitaji ili viwe na maamuzi ya haraka kuhusu kukabiliana na soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo linachangia kwa kiwango kikubwa kuua Vyama vya Ushirika vya Msingi ni ukaguzi hafifu uliopo hivi sasa kwenye Vyama vya Msingi. Ukaguzi huu umekuwa hafifu kwa vile Maafisa waliopo hivi sasa hawatoshi. Aidha, kila Wilaya ina Maafisa Ushirika wasiozidi watatu. Hali inayowafanya Maafisa hawa washindwe kufikia Vyama vya Msingi kwa muda muafaka ili kuvifanyia ukaguzi na kuzuia ubadhirifu kwenye Vyama vya Msingi. Ushauri wangu napendekeza Serikali iajiri Maafisa Ushirika Wasaidizi kila kata ili waweze kusimamia kwa ukaribu Vyama vya Ushirika vya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kero ya wakulima kutolipwa fedha yao ya mauzo ya pamba. Bodi ya Pamba ni chombo cha Serikali ambacho kinasimamia zao la Pamba ikiwa ni pamoja na kutoa leseni kwa wanunuzi wa pamba. Wanunuzi wanapokiuka masharti, Bodi ya Pamba ina wajibu wa kuwafungia, hali ilivyo hivi sasa ni mbaya sana kwa wakulima wetu. Makampuni yamekuwa yakichukua Pamba ya wakulima kwa mkopo na baadae kushindwa kuwalipa na Bodi kama chombo cha Serikali haisaidii na badala yake inaendelea kutoa leseni kwenye makampuni hayo.

Naiomba Serikali ieleze kwa nini inaendelea kutoa leseni ya kununua Pamba kwa kampuni ya *NAMERA Group* ya Kahama wakati haijalipoa wakulima wa Wilaya ya Bukombe jumla ya shilingi 11,500,000/= . Je, Bodi ya Pamba kama chombo cha Serikali inasimamia vipi hali ya malalamiko ya wakulima wa Pamba ili kujenga imani ya kuendelea kuzalisha zao la Pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha aeleze jinsi Serikali itakavyowasaidia wananchi wakulima wa Pamba kulipwa fedha zao na Kampuni ya *NAMERA Group* iliyoko Kahama kwa msimu 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na jitihada za kuimarisha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi na mapendekezo ni kuwa Bodi za mazao zipelekwe katika Wizara hii. Vipi masoko bila Bodi ya mazao. *This is an anomaly.*

Pia Makambako pajengwe soko kubwa ya Kanda ya Mazao ya Kilimo. Mazao yanawekwa mbugani tu. Hivi sasa pale Makambako wamejaa wanunuzi wa mazao ya kilimo (viazi, mbao, matunda, mboga na kadhalika) kutoka Kenya, Malawi, Kongo, Zanzibar, Comoro na kadhalika. Kuna wakati hasa wakati wa njaa watu hutoka Arusha, Mwanza, Dodoma, Shinyanga na kadhalika. Haya ni maombi ya siku nyingi. Hii ni njia muhimu ya kuwapatia wakulima soko la mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa Tanzania kupita Wizara hii ijenge *Marketing Centres* katika maeneo fulani, *strategic* ikiwa ni pamoja na maeneo ya mipakani kama vile Tunduma, Kigoma, Isaka, Arusha, Mtwara, Makambako na kadhalika. Halmashauri za Wilaya haziwezi kufanya kazi hii ya ujenzi kutokana na kufutwa kwa kodi. Hili ni wazo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makambako ni lango la kuingilia Kusini, ni njia panda kubwa, ni katikati ya Mji wa Iringa, Mbeya na Songea. Pana hudumia *Kilombero Valley*, Mikoa ya Iringa, Ruvuma na Mbeya na ni bandari ya nchi kavu. Naomba majibu kutoka Wizara hii. Nimeleta maombi na mapendekezo haya kwa maandishi. Naomba ufafanuzi wa maana ya *Marketing Development Centre*. Ni nini kitu hiki?

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole nyingi kwa kifo cha mtoto wa Mheshimiwa *Sir* George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu uhaba wa wafanyakazi Lushoto. Lipo tatizo kubwa sana la Maafisa Ushirika na Wakaguzi. Ushirika hauwezi kustawi bila washauri wa Maafisa Ushirika na wakaguzi. Lushoto hatuna wakaguzi na Maafisa Ushirika. Tunaye mtumishi mmoja wa Idara ya Ushirika Wilayani Lushoto. Naomba Mheshimiwa Waziri na Maafisa wako mtupie macho tatizo hili. Kwa nini Lushoto kuna mtumishi mmoja? Atafanyaje kazi, Vyama tunavyo zaidi ya 45?

Pili, kuhusu vitendea kazi. Nashauri uwepo mkakati rasmi wa kuwapatia Maafisa Ushirika na Wakaguzi, vyombo vya usafiri. Suala hili lisiachiwe Halamshauri zenyewe. Ni wazi kwamba Halmashauri hazina uwezo. Pawepo na mpango mahsusi utakaotayarishwa na Wizara ikibidi hata mkopo wa muda mrefu utafutwe tuwawezeshe.

Tatu, kuhusu Elimu ya Ushirika, ipewe msisitizo mkubwa zaidi wanachama wapewe elimu ili waupende Ushirika. Wajanja katika Ushirika wanaowadhulumu wanachama wachukuliwe hatua kali tusioneane aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhusu fedha za *STABEX*. Nakubaliana na mpango wa Serikali kuzitumia fedha za *STABEX* kuimarisha miundombinu. Nashauri barabara zitakazotengenezwa zitangazwe bayana. Ipo hofu kwamba wajanja katika maeneo yenye uzoefu watapewa upendeleo kuliko maeneo mengine. Lushoto tunalima kahawa lazima tupate mgao wa haki na ujulikane, tushirikishwe.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kwa kuipongeza Wizara hii chini ya Mheshimiwa Sir George Kahama, pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu na watendaji wake wote, chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpa pole Mheshimiwa Waziri, kwa kufiwa na mwanaye. Mungu awape nguvu yeye na mkewe kwa kufiwa na kipenzi chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mchango wangu ni kama ifuatavyo. Naiomba Wizara hii iimarishe Vyama vya Msingi vya Jimbo la Songwe. Cha kufurahisha ni kwamba Vyama vya mwanzo vya msingi bado vina nguvu ila tu Chama Kikuu cha *Union* cha *CHUDET* ndicho kilichokufa. Sasa naomba Ushirika au Wizara irudishe au isaidie kuanzisha Chama kingine cha Wilaya ya Chunya kwa maana ya Jimbo la Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, baada ya kuvunjwa kwa Chama cha Ushirika, bado madeni ya wakulima na madeni ya Serikali na wadau wengine wa Chama Kikuu cha *CHUDET*. Zipo baadhi ya mali nyingi zilizotafishwa au vipo kwa mfilisi. Sasa tatizo hata uuzaji wake ni mgumu sana. Wananchi wanahoji, magari yao yapo wapi, mashine za kiwanda cha kuchambulia pamba zipo wapi na kadhalika.

Naiomba Wizara sasa isiadie kuwaelevesha wananchi juu ya jambo hili. Naomba kusaidiwa kuandaa mkutano wa wanaushirika wa Jimbo langu la Songwe, ili kuunda upya Ushirika katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba Wizara ianze kusimamia uuzaji wa mazao hasa ufuta, mahindi, ulezi na mazao mengine kwa maana baada ya kufa zao la Pamba hakuna tena usimamizi wa ununuzi wa mazao uliopo hivi sasa. Hata pia kuwepo kwa watu wanaonunua wapitie Wizara yako, ili iwe rahisi kupata *cess* na kadhalika. Bado tunayo ma-*godown* ya kutosha kuliko ilivyo sasa na nne, naomba sasa Katibu Mkuu afanye uhamisho kwa Wakuu wote wa Ushirika wa Mikoa na wale wa Wilaya ili kuleta *effective management*, wamefanya kazi kubwa huko nyuma sasa waende sehemu nyingine. Bila shaka kutaonekana wazi utendaji wao wa kazi. Hata kama hakuna pesa Wizara iombe labda haikuwa *budgeted for*. Mara baada ya zoezi hilo ambalo bila shaka hata Mheshimiwa Rais atakubaliana nalo, itafute elimu ya Wanaushirika kuwepo. Naomba wazo hili lisipuuzwe na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, ili kufufua Ushirika, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wanapaswa watembelee Wanaushirika. Hata Katibu Mkuu anaweza kufanya hivyo. Wananchi watakuwa tayari kuupokea Ushirika na hautazorota tena, Serikali sasa haipati

kodi sehemu zingine kama kodi ya kichwa na kadhalika. Ni rahisi sana kuanza kujenga masoko ya ununuzi wa nafaka mbalimbali ili Serikali iweze kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu katika maeneo haya niliyoyaongelea. Naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa yenye matumaini mazuri ya kazi kubwa ya kufufua Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufikia hatua ya kuandaa Muswada wa Sheria ya Ushirika (2003) jambo ambalo linatufanya tusiwe na mambo mengi ya kuzungumza hivi sasa. Naamini sheria mpya itarekebisha mambo mengi yenye utata katika sheria ya zamani. Naomba kuishauri Wizara kuweka mikakati mizuri zaidi hivi sasa katika kuvijenga Vyama vya Msingi. Huko ndiko kunakuwa na matatizo mengi ya ubadhirifu, wizi, uzembe na kutowajibika na ndiko kwenye wanachama wengi. Vyama vingi hivi sasa vimeshindwa kujiendesha kwa kukosa mitaji na hasa baada ya kushuka bei ya mazao ya biashara katika masoko kwa mfano Kahawa. Kuhusu Vyama vya Kuweka na Kukopa, Serikali au Wizara ikubali kulea Asasi zote za Kuweka na Kukopa bila kujali ni vya Ushirika au aina nyingine kwani hiyo ni nguzo kubwa ya kujiimarisha kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vipengele ambavyo ni vema viangaliwe ni kama ifuatavyo. Kifungu cha 45 sheria namba 15 ya mwaka 1991 kinasema Katiba ikitayarishwa na Halmashauri iende kwa wanachama kuthibitishwa, kisha iende kwa Mrajisi Msaidizi wa Mkoa aithibitishwe ndipo itumike. Katiba nazo zipitie hatua hizo hizo. Matokeo yake, kunakuwa na ucheleweshaji wa utekelezaji kwani asasi zinachelewa kupata Katiba zake. Asasi nyingine zinashindwa kuandaa Katiba zake zenyewe na kutumia miongozo iliyotolewa na Idara ya Ushirika kuwa ndiyo Katiba. Utaratibu ambao unawanyima nafasi wanachama kuchangia hoja zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla, Msajili wa Asasi za Kuweka na Kukopa nje ya Asasi za Ushirika awepo Wilayani na kufanya kazi kwa karibu sana na Afisa Ushirika wa Wilaya. Aidha, Afisa Ushirika apewe kibali kisheria kukagua Asasi zote za Kuweka na Kukopa bila kujali aina ya Asasi hizo. Pia Halmashauri za Wilaya ziwe karibu kisheria ili kusimamia Asasi zote za Kuweka na Kukopa ili ziweze kuwaadabisha viongozi wanaokiuka sheria na kufanya ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *Rural Financial Services* unaofanya kazi katika Mikoa kama Mbeya, Kilimanjaro, unafanya kazi nzuri ya kutoa mafunzo na kusimamia mikopo katika Asasi hizi za Kuweka na Kukopa. Wanachama wengi wameanza kuelewa kuwa msingi mkubwa wa kujiimarisha kiuchumi na hivyo kujenga mitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana azma ya Mheshimiwa Waziri kukipa hadhi ya Chuo Kikuu Chuo cha Ushirika Moshi. Tunahitaji sana wataalamu wasomi katika ujenzi wa Ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko mia kwa mia.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali napenda kumpa pole nyingi sana Mheshimiwa *Sir George Kahama*, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko na familia yake kwa msiba mkubwa uliowafika. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pole hizo napenda nimpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba nzuri mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kujielekeza katika hoja kwenye kipengele cha kuimarisha Ushirika kwa kuanza na faraja niliyopata.

Nimefarijika kwa hatua ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa Mikopo kwa ajili ya Sekta isiyo rasmi (*Credit Agency for the Informal Sector*), pia kwa hatua ya Wizara tatu, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Wizara ya Ushirika na Masoko, kutoa mwongozo wa pamoja kwenye Halmashauri kuhusu jinsi ya kuandaa Mpango Shirikishi ya Kilimo, Mifugo na Ushirika na nimefurahishwa pia kwa kauli kwamba fedha za kuendeleza ushirika chini ya sera muafaka ya ushirikishwaji zimetengwa chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi, hasa wazalishaji wadogo wadogo na wa kati wamehamasika sana, na kuwa tayari kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa (*Savings and Credit Societies (SACCOS)*), basi tutumie mazingira haya mazuri yaliyopo kuimarisha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba kazi nzuri zilizofanywa na Serikali na Wizara zetu tatu kama ilivyobainishwa chini ya vipengele (i) mpaka (iii) katika mchango wangu hapo juu zipelekwe kwa wadau, wananchi moja kwa moja kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge, kupitia mwongozo wa Mpango Shirikishi uliobainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nashauri Waheshimiwa Wabunge tugawiwe mwongozo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho abainishe kuimarisha Ushirika. Waheshimiwa Wabunge wawe mstari wa mbele na wafanye hivyo kwa vitendo. Mfano, uanzishaji wa *SACCOS* zisizopungua 5 kwa kila kata na kuanzia kata tano awamu ya kwanza hadi 2005. Hatua hii itazaa Vyama  $294 \times 5 \times 5 = 7350$ . Ushirikishwaji wa aina hii utakuwa na faida kuu nne. Moja, ongezeko kubwa katika kipindi kifupi, pili, Vyama vitaongezeka vijijini na kupunguza umaskini, tatu, Vyama vitakuwa endelevu na nne, wigo wa utoaji mikopo utaongezeka na ajira itaongeza pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la kuangalia na kuchukua hatua ni suala la masoko, hasa kwa mazao yasiyo asili kama asali. Huko Wilayani Kibondo zipo tani mbili za asali iliyosafishwa ambazo zimekosa soko kwa zaidi ya mwaka sasa.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa *Sir* George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa kwa umahiri mkubwa licha ya kuwa katika hali ngumu na ya huzuni ya msiba.

Aidha, napenda kwa msingi huo huo kuwapongeza Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, pamoja na viongozi wengine wote na wafanyakazi wa Wizara, Mashirika yake na Asasi zake nzuri kwa kushiriki katika matayarisho ya hotuba hii na kwa jitihada zao kubwa katika kujenga upya na kuimarisha Ushirika na kuweka misingi imara ya kuendeleza masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika ndizo Asasi zilizo mstari wa mbele za kuwawezesha wananchi kupambana na umaskini, kiuchumi na kijamii, hasa vijijini. Pamoja na kuipongeza Wizara kwa dira, sera na hatua zenye madhumuni ya kuendeleza Ushirika. Maaafisa wa Ushirika Wilayani na vijijini bado wanahitaji msukumo mkubwa ili waweze kuhamasisha, kujasirisha, kukagua, kutoa ushauri na misaada mengine kwa wanaushirika ili Vyama vya Ushirika vikue na kuendelea pamoja na wanaushirika kufaidika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyogusia moja ya tatizo kubwa linalowasumbua wakulima na wanaushirika ni ukosefu wa taarifa muhimu za masoko hasa mkondo ya uuzaji na bei. Ingawa Taasisi ya ukuzaji masoko (*MDC*) na taasisi nyingine zinaweza kuwa na taratibu nzuri za kupata na kusambaza taarifa za masoko, kuna hatari ya taarifa hizo zikaishia katika ngazi ya Mikoa au Wilaya iwapo hakutakuwepo utaratibu na mfumo mahsusi na madhubuti wa kuhakikisha



kwamba taarifa hizo zinawafikia wakulima na wanaushirika kwa hali na wakati muafaka. Vinginevyo jitihada hii haitoleta manufaa yanayotarajiwa.

Kuna umuhimu kubwa sana wa kuwa na utaratibu madhubuti wa kulinda Vyama vya Ushirika dhidi ya wahujumu, wizi na ubadhirifu. Ni muhimu Serikali ikawaelimisha wanaushirika kuwa makini sana katika kuchagua na kuwadhibiti viongozi wa Vyama vya Ushirika. Vilevile, nashauri kwamba pale Vyama vya Ushirika vinaposhamiri, Serikali iwe macho kutoruhusu kuwepo Asasi nyingine ambazo zinaathiri uhai na maendeleo ya Vyama vya Ushirika halisi vya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa vitimbi vinavyofanyiwa Chama cha Ushirika cha Wafugaji wa Maziwa Mkoa wa Tanga (*TDCU*). Chama hiki ambacho kina Vyama vya Misingi 9 wanachama 2,500 na miradi mbalimbali ukiwemo mradi wa *Youngsters* ambao una vijana wapatao 300 waliwekeza katika Kiwanda cha *Tanga Fresh*, kimepiga hatua kubwa sana kutokana na ari kubwa ya viongozi na wanachama wa *TDCU*, chama hiki kimeweza kupiga hatua kubwa zaidi kutokana na mradi maalumu wa kuendeleza ng'ombe wa maziwa (*SPDP*) ambao ulikuwa ukifadhiliwa na Serikali ya Uholanzi. La kushangaza ni kwamba badala ya kuutambua Ushirika huu wa Mkoa uliojengeka vizuri na kuimarika, wakati mradi ulipomalizika Ushirika huu haukukabidhiwa vifaa na mali zilizoachwa na mradi bali badala yake uliundwa udhamini (*Trust*) unaojulikana kama *Tanga Dairy Trust (TADAT)*. *TADAT* ndiyo iliyokabidhiwa mali na vifaa vilivyoachwa na mradi kwa matarajio kwamba itaendeleza mifugo kwa ajili ya maziwa kupitia vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, hatua hii naiona kuwa inaelekea katika kuubomoa Ushirika uliokwisha kujengeka. Matokeo yake ni kwamba hisia za Wahisani ni kwamba Tanzania haiwezi kuwa na Mradi Endelevu. Kwa upande mwingine wanachama wa *TDCU* na wanaushirika wengine watarudia hali ya kutokuwa na imani na Ushirika. Hivyo, jitihada za Serikali kufufua na kuendeleza Ushirika zitagonga ukuta. Hatua za urekebishaji wa hili ni muhimu iwapo kweli tunataka Ushirika uwe ukombozi wetu kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kushauri kwamba Wizara isimamie kwa nguvu zaidi katika kuhimiza kuwepo na kutumiwa vizuri kwa magulio. Aidha, kuharakisha kuundwa kwa Benki ya Ushirika, *SACCOS* na sheria mpya ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampa pole Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichangie suala la masoko. Mwezi Mei, nilikuwa nazungumza na wakulima wa kahawa Wilayani Mbinga. Niliwauliza nani leo amekunywa kikombe cha Kahawa? Hakujitokeza hata mmoja. Lakini nilipouliza nani amekunywa chai, watu wengi wakanyoosha vidole. Sasa hapo kuna hatari. Tunalima kitu ambacho hatuli na si kweli kwamba watu hawali, lakini hakuna chombo cha kuhamasisha na kuweza kutengeneza ile Kahawa ili inywewe, kwa hiyo, Kahawa yetu yote inauzwa ikiwa malighafi.

Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tunajandaa tu kwa ajili ya soko la nje badala ya kuendeleza soko la humu ndani. Kwa hiyo, mimi ningependekeza na kushauri kwamba pawepo na mikakati ya makusudi kuhakikisha kwamba kwa kiwango kikubwa tunatengeneza kahawa hii ili tuwe tunauza mali yenye thamani kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, suala hili la masoko vile vile naomba tukubaliane kwamba wakulima wetu wengi ni watu wenye elimu ndogo hasa katika fani ya masoko na ikizingatiwa kwamba kwa muda mrefu masuala ya masoko yalikuwa ni masuala ya Serikali. Sasa hivi tunapowaambia wakulima wapate taarifa ya bei ya masoko kutoka kwenye *Internet*, kwa kweli hii inawezekana! Mimi ningeshauri moja ya kazi kubwa ya Wizara hii hasa Kitengo cha Masoko ingekuwa ni kuandaa mikakati ya kuhakikisha kwamba wanatutafutia masoko ya nje na humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi, nilikuwa nazungumza na Ubalozi wa China, wakasema wanashangaa sana wenzetu Waganda wamefungua migahawa yao Uchina na Wachina sasa hivi wanaanza kunywa Kahawa. Sasa je, sisi tunafanyaje?

Kwa hiyo, mimi nikaona ni changamoto kwamba ni vizuri Wizara hii isibaki tu pale Ofisini kwake, lakini iwe na kitengo maalum cha kupita, kufanya mawasiliano na Balozi zetu ili kuweza kupata soko na vile vile kuweza hata kufungua migahawa katika nchi zile ambazo tunaweza baadaye tukauza kahawa yetu ili tujihakikishie soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo ambalo wenzangu wameligusia ni lile la gharama. Makato ambayo kwa kweli yanamfanya mkulima asiweze kuhudumia zao lake sawasawa. Sisi tunao mfano, kahawa inasafirishwa kutoka Mbinga, inakwenda Makambako. Kila kilo moja ikitoka Mbinga kwenda Makambako unalipa shilingi 30/=. Kadhalika ikilala Makambako kwenye yale maghala, kilo moja inatozwa shilingi 30/=. Sasa nauliza, kuna mantiki gani ya kupeleka kahawa Makambako? Kwa nini kahawa isichukuliwe Mbinga ikapelekwa moja kwa moja kwenye mnada halafu likawa ni jukumu la wanunuzi kuja kusafirisha kahawa hiyo kama vile walivyokuwa wanafanya wakati wanunuzi binafsi walikuwa wameruhusiwa. Kwa hiyo, mimi bado ni ombi langu kwamba ni muhimu kabisa tuweze kuondoa gharama hizo ili mkulima aweze kupata fedha za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, moja ya tatizo ambalo linachangia kuporomoka kwa bei ya mazao Vijijini ni mfumo wa Taasisi za Fedha hapa nchini. Kuna wakati nilisema katika Bunge lako Tukufu kwamba noti ilivyokuwa inasambaa sana katika nchi hii kwa asilimia 56, ni noti ya shilingi 10,000/= na asilimia 28 ni noti ya shilingi 5,000/=. Hii inayobaki ndiyo hela ambayo ni noti ya shilingi 1,000/= na shilingi 500/= na kwenda chini.

Sasa ukiangalia mfumo wa Benki, Benki zote ziko katika Miji. Sasa maana yake nini? Imewahi kutokea kwamba baadhi ya Wafanyabiashara wanadiriki kubeba fedha kwenye magari mpaka milioni 500 kwenda kununua Kahawa. Sasa najiuliza ni Benki gani inaruhusu kiasi hiki cha fedha?

Sasa matokeo yake, fedha huwa hazisambai Vijijini. Kule Vijijini wakulima wanakuwa hawana fedha na wanunuzi wanapokuja, akiwa na shilingi 10,000/= anaweza akanunua gunia la kahawa. Anakwambia moja kwa moja bei ya gunia hili shilingi 10,000/=. Kama hutaki, kula. Bahati mbaya ile kahawa huli. Basi unakubalina na bei hiyo. Kwa hiyo, nashauri kwamba suala la hizo fedha pengine lingeanjaliwa upya. Mfumo huu umetupeleka pabaya, watu sasa hawatumii hundi. *Negotiable instrument* haziheshimiwi tena. Mimi nadhani ipo haja ya kufutilia mbali hizi noti kubwa kubwa badala yake tuongeze kwa kiwango hiki hizi hizo hela ndogo ndogo kama shilingi 500/= ili ziweze kusambaa vijijini. Mtindo huu utawafanya sasa wakubwa wanaotorosha fedha au kufanya Benki zao za chini chini, wakome.

Kwa hiyo, hili suala sio dogo na mimi ningeshauri kabisa wenzetu wa fedha waende huko Vijijini waone jinsi gani noti ya shilingi 1,000/= inavyoweza kumsumbua mtu kupata *change*. Hali ni mbaya sana. Matokeo yake tunarudi kwenye uchumi wa ujima. Mtu anachukua ng'ombe, anakwenda kutibiwa hospitali kwa sababu hela hamna. Hii nadhani ni uchumi wa hatari sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa ni vizuri tukautazama huo mfumo kwa makini zaidi ili tuepukane na huo mfumo wa ujima au *barter system* kwa sababu tutakuwa tunajidanganya kwamba uchumi wetu unaendelea kumbe tunarudi kwenye uchumi wa mwaka 1947.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema tena, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

#### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpa pole nyingi Mheshimiwa Waziri, *Sir* George Kahama na familia yao kwa msiba mkubwa waliopata, Mungu ampe subira.

Napenda kumshukuru Waziri kutokana na umuhimu wa ushirika kwa nchi nzima, badala ya kuunda Benki Maalum ya Ushirika ambayo itakuwa ni gharama kubwa sana na mzigo kwa Watanzania, afadhili utaratibu wa kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika, yalazimishwe Mabenki yetu ya Tanzania hasa *NMB, NBC, CRDB, PBZ* na kadhalika wavipe Vyama vya Ushirika na *SACCOS*. Hii itasaidia kupunguza gharama zisizo za lazima za kuanza *Giant* mwingine. Nina hakika tukishirikisha *BOT*, basi hili lingeweza kutekelezwa na kuratibiwa vizuri tu na Mabenki yetu haya ambayo tayari yana mtandao mkubwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua katika fedha za *STABEX* zilizokuja Tanzania ni ngapi zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya kuendeleza zao la Karafuu? Ningefurahi nikielezwa kwa miaka tangu mwaka 1995.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampa pole sana Mheshimiwa *Sir* George Kahama, kwa msiba mkubwa aliopata wa kupoteza kijana wake tarehe 19 Julai, 2003. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu kwa kumsaidia Mheshimiwa Mtoa hoja Waziri kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kwamba kwa sababu hoja zenyewe ni nyingi na kusema kweli nyingi zilikuwa na michango mizuri ya ushauri, hatutaweza kupata nafasi hapa kujibu zote, lakini tutajitahidi kupitia zile tutakazoweza na zitakazokuwa zimesalia, basi tutaziandalia majibu rasmi na kuziwasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge. Lakini niseme tu kwamba tunaithamini sana michango yao wote iliyotolewa hapa Bungeni na tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pengine kabla sijajielekeza katika kujibu hoja mbalimbali na mimi pia niungane na wachangiaji wengine wote walionitangulia kumpa pole sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mama Janet Kahama, kwa msiba mzito uliowapata kwa kuondokewa na kijana wao siku chache zilizopita. Kwa hiyo basi, tumwombe Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba awali kabisa kutamka kwamba naunga mkono hoja. Napenda vile vile niwashukuru wenzangu wote walionitangulia katika kuchangia, waliounga mkono hoja hii pamoja na wale ambao hawakupata fursa ya kuchangia lakini kwa fikra na vitendo wanatuunga mkono. Kwa hiyo, wote nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijielekeze katika baadhi ya hoja ambazo nitapata fursa ya kuzipitia kama nilivyosema, sio zote lakini nyingine baadaye Mheshimiwa Mtoa hoja atakuja kuzikamilisha hapa na niseme tu kwamba kwa wale wote waliochangia kwa kusema hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Waziri atawatambua rasmi kwa kuwataja majina atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuangalia hoja mbalimbali na ya kwanza ambayo ningependa niipitie ni suala lilolozungumzwa hapa juu ya kuundwa kwa vyombo vitakavyosaidia kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika kama vile Benki za Ushirika, *SACCOS* na kadhalika. Sasa hoja hii imezungumzwa na watu wengi kidogo na sio rahisi kuwataja wote kwa haraka haraka, lakini Mheshimiwa Lephy Gembe, alikuwa ni mmojawapo, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, hapa mwisho mwisho, Mheshimiwa George Mlawa na wengine kadhaa waliongelea hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema tu kwamba Serikali itaendelea kuwa mhamasishaji wa wananchi kuunda asasi za fedha zikiwemo *SACCOS* na kama tutakavyoona huko mbele kwamba vyombo

hivi vya wananchi, hizi *SACCOS* pamoja na *Community Banks* na hatimaye Benki ya Ushirika ndiyo tegemeo la wananchi kwamba hapo baadaye hata malalamiko haya mengi ambayo tunayazungumzia habari ya riba kubwa, masharti magumu ya upatikanaji wa mikopo na kadhalika inaweza kuwa ndio suluhu yetu katika kuanzisha Taasisi ambazo zinasimamiwa na kuundwa na wananchi wenyewe.

Kwa hiyo, tunaungana kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliotoa hoja hii na ndio maana na sisi tunasimamia utaratibu wa kuhamasisha wananchi waweze wakajanzishia vyombo vyao hivi vya kujiletea mikopo pamoja na huduma nyingine za kifedha.

Pia iko hoja ambayo imezungumzwa na watu wengi kidogo juu ya suala la elimu ya ushirika pamoja na uongozi kwa ujumla kwenye Vyama vya Ushirika ambayo kwa kusema kweli ndiyo chimbuko la matatizo mengi ambayo tunayapata kwenye Vyama vyetu vya Ushirika kwamba kuna elimu duni ya ushirika, wanachama wanakuwa hawajui wajibu wao, hawajui kwamba Vyama hivi vya Ushirika ni vyao, lakini isitoshe hata hao viongozi wanaoongoza Vyama vyao wanakuwa hawana Elimu ya Ushirika na hatimaye wengine wanatumia madaraka vibaya kwa kujichukulia madaraka na kwa hiyo kuteka nyara Ushirika.

Sasa hili suala limeongelewa kwa kina sana na wengi wamependekeza kwamba dawa ni kutoa Elimu ya Ushirika na sisi tunakubali kabisa kwamba hiyo ndiyo suluhu ya kuhakikisha kwamba wanachama wetu kwanza kabla hata hawajaanzisha Vyama vyao vya Ushirika, basi waelimishwe waweze wakaona haja ya kuanzisha Vyama na hatimaye wavisimamie, waviendeshe na waone manufaa yake na vile vile viongozi wao pamoja na Watendaji waweze wakaelimishwa ipasavyo. Sasa hii tunasema kwamba bahati nzuri tulikuwa tumeshaibaini hata kwenye ile Kamati ya Rais ambayo ilikuwa inaangalia matatizo mbalimbali na kutokana na hiyo, mapendekezo yaliyojitokeza na ambayo yanatekelezwa sasa hivi na Wizara pamoja na Taasisi yake ya Chuo cha Ushirika Moshi, tumeanzisha mpango wa elimu shirikishi ya ushirika ambayo inagusa sekta zote za umma pamoja na wananchi kwa ujumla wakiwemo viongozi pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kwamba pengine ingekuwa ni vizuri basi kupitia katika mpango huu na sisi kama Wabunge tukishiriki tukaelewa, basi itakuwa ni rahisi tukasaidiana kuwashauri na kuwaelekeza wananchi wote kwa ujumla tuweze tukaanzisha Vyama vya Ushirika ambavyo ni imara vyenye wanachama ambao wanavisimamia kwa ukamilifu lakini hasa hasa nikizingatia kwamba suala la uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika liko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo Chama kinachotawala.

Nadhani kwa upande wetu sisi kama Wabunge pamoja na viongozi wengine wote wa Chama cha Mapinduzi, tukielewa vizuri tunaweza tukasaidiana tukawa mstari wa mbele angalau kuanzisha Vyama vya Ushirika mmoja mmoja tukawa wanachama katika Vyama vya aina mbalimbali kwa hiyo tukasaidia katika suala hili la kujenga Ushirika ambao uko imara.

Sasa hili limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Talala Mbise, hapa mwisho, pamoja na wengine. Kwa hiyo, sasa huo ndio ushauri ambao ningeweza nikasema kwamba pengine unaweza ukatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa suala la fedha za mkopo wa Pembejeo na Waheshimiwa Wabunge wengi sana na kama nilivyokuwa nimeshaeleza awali kwamba hili kusema kweli Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanajaribu kuelezea juu ya ugumu wa upatikanaji wa mikopo kwa ujumla, lakini wakawa wanapendekeza vile vile kwamba hata huu mkopo wa Pembejeo ambao unatolewa na Serikali wakawa wanadhani kwamba ni vizuri badala ya kuuelekeza katika vyombo vichache vya fedha, basi ukapanuliwa vyombo vingi vya fedha vikawa vinahusika na wametaja baadhi ya Benki hapa na sisi tunataka kukubaliana nao kwamba kusema kweli ukitaka kupanua huduma hii vizuri, ni lazima uhusishe na vyombo vingi sana vya fedha.

Hivi sasa kama tulivyokuwa tumeshasema siku mbili, tatu, zilizopita, sio *Exim Bank* peke yake ambayo sasa hivi inahusika na utoaji wa mkopo huu wa Pembejeo lakini vile vile iko Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro, iko Benki ya Wakulima wa Ushirika wa Kagera, kiko Chama Kikuu cha Ushirika wa Vyama

vya Akiba na Mikopo *SCCULT*, ziko *SACCOS*, iko Benki ya Jamii yaani *Community Bank* ya Mufindi pamoja na Vyama vingine ambavyo vinaweza vika-*qualify*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kazi kubwa kusema kweli ni kuhimiza uundaji wa hizi Taasisi za Fedha zinazoundwa na wananchi hasa hasa *SACCOS* pamoja na *Cooperative Banks* na hatimaye Benki ya Ushirika ya Taifa ambavyo kwa ujumla wake tunadhania kwamba zitakuwa zinahusisha wanachama wenyewe na wananchi kwa ujumla.

Kwa hiyo, hata haya masharti ambayo tunayalalamikia, riba kubwa pengine kwa ushindani ambao utakuwa umepanuka zaidi, kwa hiyo, hata pengine hizi Benki za binafsi ambazo zinatoza riba kubwa sasa hivi, masharti magumu kwa sababu kutakuwa na ushindani, inawezekana kabisa masharti haya yakapungua. Lakini la msingi hapa ambalo sisi tunadhania kwamba ni wajibu wetu wa kusimamia ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuimarisha Vyama vya Msingi vya Akiba na Mikopo pamoja na Taasisi nyingine za Fedha ili ziweze zikashiriki katika zoezi hili la kuhudumia wakulima katika utoaji wa mikopo ya aina yoyote, sio lazima tu hii ya Benki ya Mfuko wa Pembejeo lakini ni mikopo ya aina yote pamoja na vikundi vya akina mama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa iko hoja pia ambayo pengine ni mahususi ambayo ameitoa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Ileje na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuhusiana na uchunguzi wa mgogoro ambao Wizara imekuwa ikiifanya miongoni mwake ikiwemo Chama Kikuu cha Ushirika *MICU* yaani *Mbeya Ileje Cooperative Union*. Taarifa hiyo ipo, tutahakikisha kwamba hiyo taarifa tutakupatia.

Nadhani ukishaiangalia na kwingine pamoja na wanachama wote ambao wanahusika katika eneo lile inaweza ikasaidia kuimarisha Vyama vya Ushirika na kusema kweli jukumu letu kubwa sisi katika azma ya kupeleka hizi Tume za Uchunguzi ni kuhakikisha kwamba tunavisaidia hivi Vyama vyote ambavyo viko katika matatizo ya uongozi, matatizo ya aina mbalimbali ili viweze kuimarika na hatimaye vihudumie wanachama wetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja imejitokeza ya Sheria ya Ushirika kutambua vikundi vya Ushirika, wametoa ushauri Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, ambao wanasisitiza tu kwamba vikundi hivi vya Ushirika lazima vitambuliwe.

Sisi tunasema kwamba katika mapendekezo kama mtakavyoona katika sheria ambayo tunakusudia kuiwasilisha Bungeni katika kikao kitakachokuja, hiki kipengele kimezingatiwa kwamba sheria itavitambua hivi vikundi vya Ushirika vya aina mbalimbali vikiwemo vikundi vya akinamama, vijana, walemavu na wa aina nyingine viweze vikalelewa na hatimaye viweze sasa kama vitaamua vyenye kuweza kuamua kuandikishwa kama Vyama vya Ushirika na hatimaye viweze vikatoa huduma kwa wanachama wake kama Vyama vya Ushirika kamili.

Kwa hiyo, sheria imezingatia hilo na sisi tumeomba kwamba sasa maadam sasa hivi tunatazamia kuileta hii sheria Bungeni na kwa sababu tayari tunao Muswada, basi nadhani mawazo yenu yatasaidia sana katika kuiboresha na hatimaye tuweze tukaanzisha sheria ambayo ni bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika lipo suala la mali za Vyama vya Ushirika vilivyovunjwa mwaka 1976 pamoja na hisa za Vyama vya Ushirika katika *CRDB*. Waheshimiwa Wabunge wameliongelea, Mheshimiwa Jacob Shibiliti na Mheshimiwa Semindu Pawa.

Sasa katika hili nataka niseme kwamba Kamati ya Rais ilishabaini hili tatizo na ikatoa mapendekezo ya namna ya kulishughulikia. Sasa mapendekezo hayo yanashughulikiwa hatua kwa hatua kwa sababu mali hizi ziko katika maeneo mbalimbali na ziko katika sura mbalimbali, kama tulivyosema, hapa kuna hisa, mahali pengine majengo na kadhalika.

Kwa hiyo, yapo mapendekezo na kwa vile tulikwishatoa ile taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, nadhani tukirejea, tuangalie tutaona jinsi ambavyo Kamati ilivyokuwa imependekeza na kwa bahati

nzuri taarifa ile ilikuwa imeshakubalika na sasa hivi ni *document* rasmi ambayo inaweza ikatumika. Kwa hiyo, mapendekezo yale yana uhalali wa kufuatiliwa kwa hiyo hilo litakuwa linafuatiliwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo hoja ya Maofisa Ushirika Wilayani waongezwe, hili kama tulivyokuwa tumeshasema kwamba ilishabainika vile vile na mapendekezo yalishatolewa kwamba ili tuweze kukidhi haja ya kujenga Ushirika kwa kasi inayotakiwa kwa hivi sasa, tunadhani kwamba tuna mapengo ya wafanyakazi wa Idara ya Ushirika kama 300 hivi.

Hivi sasa kama nilivyokuwa nimesema wiki mbili tatu zilizopita, baadhi ya maeneo, watumishi hao wameshaanza kuajiriwa. Lakini tulichosisitiza tu ni kwamba kwa sababu watumishi hawa wanaajiriwa kupitia utaratibu wa Mamlaka za Tawala za Mikoa pamoja na maombi kutoka kwenye Idara Kuu ya Utumishi, kusema kweli tulichosisitiza ni kwamba basi kupitia Halmashauri zetu tuainishe mahitaji yetu na hatimaye yale mahitaji tuweze tukayapeleka kwenye mamlaka zinazohusika kibali kipatikane ili ajira ziweze zikapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakusudia kwamba watumishi hawa wote watakapokuwa wameajiriwa na kuanza kazi zao katika nafasi zao, basi tufanye kazi kwa uwiano ule wa Vyama saba kwa Mkaguzi mmoja, yaani 1:7. Kwa hiyo nadhani, kwa sababu zoezi lilishakubalika, tunaendelea kulishughulikia na hili ameliongelea Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa George Mlawa, pamoja na Mheshimiwa Henry Shekiffu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimesema kwamba hoja hizi nyingi ni ushauri na sisi tumesema kwamba tutaendelea kuzingatia, lakini lingine ambalo tumepewa hapa ni Mheshimiwa Aridi Uledi, alikuwa amezungumzia habari ya kuwepo kwa msimu wa ununuzi wa korosho kwa Vyama vya Ushirika na akawa ametufahamisha kwamba sasa hivi korosho inapatikana msimu wowote.

Sasa tunachotaka kusema tu ni kwamba, utaratibu wa ununuzi wa korosho msimu wote utaangaliwa na kama utakidhi mahitaji ya ufanyaji kazi kwa mujibu wa utaratibu, basi unaweza ukapewa nafasi. Lakini tujue kwamba katika suala zima hili la ununuzi wa mazao na kwa vile tunasisitiza suala la uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika ili Vyama hivi viwasaidie wakulima wa mazao yao, vyenyewe ndio vitakuwa sasa vinatambua matatizo na mazingira mbalimbali jinsi yanavyobadilika.

Kwa hiyo, kama kutajitokeza kwamba msimu sasa unakuwa ni wa kila mwaka, basi hilo litaangaliwa na kuweza kuzingatiwa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nijielekeze katika eneo lingine la masoko ambalo baadhi ya Wabunge wamelizungumzia kwa uchungu sana. Lakini pengine nianze kwenye eneo la Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

Kuna baadhi ya Wabunge ambao wanahusika na mazao haya yasiyo na Bodi maalum. Mazao mchanganyiko ni kama mazao ya mafuta, nafaka na kadhalika, hao wakiwemo Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Edward Ndeka, walilizungumza hili kwamba tumekuwa tukizungumza habari ya uundaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo itasaidia pengine utazamaji wa masoko sambamba na uundaji wa Vyama vya Ushirika na kadhalika.

Lakini sasa nataka niseme zoezi la uundaji wa Bodi hii ya Mazao Mchanganyiko hivi sasa tunavyosema, kusema kweli tumefikia hatua ya hali ya juu sana kwa sababu nyaraka zote zinazohusika na kufikishwa katika mamlaka za maamuzi zimekwishaandaliwa, kwa hiyo Wizara yetu ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, tunashirikiana kuandaa nyaraka zote zinazohusika.

Kwa hiyo, nadhani muda si mrefu Bodi hii ya Mazao Mchanganyiko itanza kufanya kazi, hatimaye iweze ikahudumia wakulima wa mazao hayo kama Waheshimiwa Wabunge walivyokuwa wamependekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *STABEX* limezungumziwa kwa nguvu sana pamoja na maelezo yote yaliyokuwa yameshatolewa jana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, pamoja na maswali ambayo tumekuwa tukijibu huko nyuma, lakini bado yamejitokeza.

Michango ya Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte na hapa mwisho Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, wote kusema kweli wamezungumzia suala hili la *STABEX* kwa mtazamo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nataka niseme kwamba maelezo yale ambayo Serikali ilitoa jana ndio maelezo muafaka na ndio yanasimama kama ndio maelezo rasmi ya Serikali. Isipokuwa tu, nataka niseme kwamba katika maelezo yale jana, kwa sababu baadhi ya mazungumzo hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanatia wasiwasi kwamba baadhi ya mazao yalikuwa hayakujumuishwa kwenye utaratibu huo wa *STABEX*, lakini katika maelezo yale tuliona mazao yaliyokuwa yamejumuishwa ilikuwa ni kahawa, pamba, chai, mkonge, korosho na karafuu. Isipokuwa kilichoonekana ni kwamba pengine ilikuwa mazao haya hayakupata *STABEX* toka wakati huo kwamba kwa kipindi hicho maana sharti mojawapo ni kwamba mazao haya lazima yauzwe katika Soko la Jumuiya ya Ulaya.

Kwa hiyo sasa, kama kwa mazao haya pamoja na kwamba yalikuwa yamejumuishwa katika mtiririko huo, lakini kwa ile miaka ambayo mazao hayo hayakupitia katika mkondo wa Soko hilo, ndio sababu kubwa ambayo ilifanya mazao haya yasiwe yanatajwa hivi sasa.

Kwa hiyo, kusema kweli hakuna upendeleo wa aina yoyote ile ambao pengine unaweza ukawa unaleta hisia kwamba ilihusisha zao la kahawa tu kwa sababu baadhi ya viongozi wanaohusika na zao hilo. Hii sio kweli hata kidogo, kwa sababu maelezo kusema kweli ni hayo, kama mazao haya mengine nayo yangukuwa yamepita kwenye mkondo wa Soko hilo, nayo yangukuwa yamejumuishwa katika mfumo huo wa *STABEX*.

Kwa hiyo, mgawanyo wa matumizi ya zile fedha ulishaelezwa jana na sina haja ya kurudia na kama mtakavyoona, yale maelezo yatakuwa yanakidhi hiyo haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na azma ya Bodi ya Pamba ya kufanya kampeni za kuongeza uzalishaji wa zao la pamba, je, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vya nguo ndani ili kuongeza viwango vya soko? Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Lucas Seleli.

Mheshimiwa Naibu Spika tunasema kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, itaendelea kuhamasisha wawekezaji kufufua viwanda vilivyopo na kujenga viwanda vipya vya kutumia teknolojia ya kisasa ili tuondokane na uuzaji wa pamba ghafi na kuongeza thamani ya pamba yetu.

Kwa hiyo, kama nilivyokuwa nimepata taarifa ya wiki moja iliyopita, kwamba wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, wanao mfuko wa kuendeleza hivi viwanda vidogo vidogo kwa ajili na kuhudumia mazao ambayo yanaweza yakabanguuliwa ikiwemo korosho na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msimu wa korosho nilikuwa nimeshahieze ambalo lilikuwa limeshatolewa na Mheshimiwa Aridi Uledi. Mheshimiwa Gideon Cheyo, ambaye ni Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, alizungumzia habari ya soko la pareto, kwa kutaka kuelewa vijiji vyake pamoja na vyama vyama vya ushirika vya Wilaya ya Ileje, tofauti na vyama vinginevyo vile ambavyo sasa hivi vimepata soko la pareto vile vya Mbeya Vijijini.

Maelezo tuliyonayo ni kwamba uchambuzi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika vitakavyoshirikishwa kupewa mkopo wa kununua pareto ikiwa ni pamoja na wakulima wa pareto wa Wilaya ya Ileje, unaendelea. Na kwa taarifa tu ni kwamba hivi sasa Serikali inaandaa mkutano wa wadau wote wa zao la pareto ambao utafanyika Mbeya tarehe 7 mwezi wa nane kuamkia ile siku ya Wakulima, Nane Nane. Ili kujaribu kuzungumza pamoja na mambo mengine suala hili la ufumbuzi wa tatizo la soko la pareto. Lakini wanunuzi binafsi wataendelea kupewa leseni za kununulia pareto kutoka Bodi ya Pareto ili kununua pareto maeneo ambayo ushirika haununui mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachotaka kusema hapa kwa upande wetu kama Serikali tunadhania kwamba ni vizuri tusaidie kuimarisha vyama vya ushirika ambavyo kwa namna moja au nyingine vinaweza vikasaidia utafutaji wa masoko vile vile na kuweza kuwahasisha wakulima waweze kujitafutia masoko kupitia kwenye vyao vya ushirika.

Michango mingine kusema kweli ilikuwa katika sura ya kimaombi. Mheshimiwa Paul Ntwina, ameomba Serikali ijaribu kuangalia vyama vya ushirika katika jimbo lake la Songwe na kuangalia chama kikuu cha *CHUTI* ili irudishe au isaidie kuanzisha chama kingine cha wilaya ya Chunya kwa maana ya Jimbo la Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka hili nijaribu kulifafanua ifuatavyo. Sasa hivi suala la uanzishaji wa vyama vya ushirika si suala la Serikali. Serikali haianzishi chama cha ushirika. Tunachofanya ni kuhamasisha kuelimisha wanachama wenyewe wajue matatizo yao. Wakishaamua kwamba wana tatizo hili ndiyo wanaamua sasa kuunda ushirika na ushirika wa aina gani.

Kwa hiyo, suala la kusema hapa kwamba Serikali isimamie kuanzisha chama cha ushirika kwenye jimbo lingine, hii itakuwa kusema kweli ni uamuzi wa wanachama wenyewe. Sasa hivi chama kilichoko kule Wilaya ya Chunya cha *CHUTI* kinasimia zao la tumbaku nafurahi kusema kwamba nimeshafika kule Lupa kuona maendeleo ya chama hiki.

Kwa hiyo, niseme kwamba wigo wa ushirika hauna kikomo, unaweza kuanzisha vyama vya ushirika vya aina mbalimbali kutegemeana na matakwa ya wanachama wetu na ndiyo maana nimesisitiza kwamba tukishaelimika sisi wenyewe pamoja na wanachama wetu, basi tutaibua matatizo yanayotukabili na hatimaye tutaanzisha ushirika ambao unaweza unajibu matakwa yetu.

Kwa hiyo, nataka tu niseme kwamba tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha wanachama wetu wanaelewa na wanataka ushirika wa aina gani ili wajianzishie ushirika wao wenyewe na waweze kuusimamia, kuumiliki kwa manufaa yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilijitokeza ni suala la ukaguzi wa vyama vya ushirika. Limeongelewa na baadhi ya Wabunge hapa, na wamependekeza hata hii Sheria ambayo inaongoza sasa hivi Shirika letu la Ukaguzi wa vyama vya ushirika yaani *COASCO*, iangaliwe upya na sisi ndivyo tulivyokuwa tumesema nadhani hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezwa waziwazi kwamba sheria ambayo inaongoza sasa hivi shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika inaangaliwa upya ili iweze kufanyiwa marekebisho hapo baadaye ili kukidhi na kwenda na wakati wa sasa ambapo vyama vya ushirika vinajiendesha kwa nguvu yake lakini ningependa tu kusisitiza hapa hata yeye Mheshimiwa Mbunge mmoja sikumbuki ni nani lakini alikuwa anazungumzia suala la ubovu wa viongozi na kuihimiza Serikali iwaondoe viongozi hao wabovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofanya ni kwamba Serikali haiondoi viongozi hao wabovu, Serikali inajaribu kuwabainisha hawa viongozi wabovu kwa njia ya kukagua, kufanya uchunguzi na kutoa taarifa kwa wenye mali. Sisi tunatoa taarifa kwa wenye mali, wanachama hawa sasa ndio wanachukua hatua ya kuwaondoa. Lakini inakuwa ni bahati mbaya sana mahali pengine ambapo wanachama wetu wanakuwa hawajaelewa vizuri, pamoja na kutoa taarifa hizi za ukaguzi zinazoonyesha maovu mbalimbali yanayofanywa na viongozi wetu hawa wabovu lakini bado utakuta kwenye uchaguzi wanarudishwa viongozi wale wale wabovu.

Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba tusaidiane, tusaidiane inapofika mahali kwamba tumeshabainisha viongozi ambao ni wabovu kwa namna mbalimbali basi tusaidie wanachama wetu waweze wakawawajibisha katika kuwatoa viongozi hao wabovu. Lakini tunayo mifano mizuri kwa mfano ya *SHIRECU* ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameipongeza leo asubuhi ni hiyo kwamba tumefanya kazi hiyo ya kuelimisha na wanachama wenyewe kwa hiari yao wenyewe wakaamua kusema kwamba sasa hapa nadhani tunataka tufanye mabadiliko na tunafanya mabadiliko na sasa hivi kazi hiyo mzuri inaendelea kuwasaidia hawa wakulima wetu. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie kwa kusema kwamba kwa ujumla kazi tunazozifanya sasa hivi pamoja na baadhi yetu wachache sana ambao wanadhani kwamba hakuna kinachoendelea. Kusema kweli kazi inayoendelea ni kubwa sana na mabadiliko ni makubwa na kwa wale ambao wamekuwa wakifuatilia mwenendo wa vyama vya ushirika hapa nchini watatambua kwamba sasa hivi kusema kweli kazi iliyofanyika ni kubwa na tungeomba tu muendeele kutuunga mkono tusaaidiane ili tuweze tukasimamia uundaji, ufufuaji, uimarishaji wa vyama vya ushirika na hasa katika eneo hili nililolizungumzia sasa hivi na kwamba tunapokuwa tumeibua wahalifu tungeomba sana tupatiwe msaada wa wenzetu wengine wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho ni kwamba nisiwe mtovu wa fadhila, nitumie fursa hii kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipa kutoka mwaka 1995, ushirikiano ambao kusema kweli umenisaidia sana kufanya kazi kwa nguvu zote na naahidi tu kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote kama mwakilishi wao na kwa hiyo niombe tuendeele kushirikiana nao pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nisema, mengi ya michango ilikuwa ni ushauri, tutaizingatia, tutaendelea kuifanyia kazi na kama nilivyosema tutatoa baadhi ya majibu kwa maandishi ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia na tuendeele kusaidiana. Narudia kusema tena, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii vile vile kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda pia kusema kwamba Wabunge wote waliochangia ni 50 na kati ya hawa 34 wamechangia kwa maandishi na 16 wamechangia kwa kuzungumza. Lakini pia wako Waheshimiwa Wabunge 42 ambao walichangia kupitia hotuba ya Bajeti ya Wizara mbalimbali hasa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafisishaji, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, ambaye siku ya leo aliwasilisha hoja kwa niaba ya Kamati. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Namshukuru pia Mheshimiwa Aisha Phillipo Magina, Waziri Kivuli wa Ushirika na Masoko, kwa mchango wake na ushauri wake mzuri na kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoyibu maswali mengi ambayo aliyazungumzia yamo tayari katika taarifa yetu ya Kamati Maalum ya Rais iliyochunguza matatizo ya vyama vya ushirika lakini hata hivyo, ningependa kuchukua fursa hii kumkaribisha kwa sababu ni Waziri mwenzangu aje Ofisini kwetu tuweze kuyaongea yale aliyoyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi ambao nitawataja hivi karibuni, wamezungumzia masuala mbalimbali ya Ushirika na Masoko kama alivyoeleza Naibu Waziri, masuala mengine yanahitaji ufafanuzi, lakini pia mengi yatalenga katika kuendeleza na kuboresha shughuli za Wizara yangu. Naomba ushauri wao usiishie hapa, usingojee hapa Bungeni. Ofisi ya kwangu na ya Naibu Waziri ziko wazi wakati wote. Msingoje kuja hapa wakati tunapokutana, wakati wowote tunakukaribisha mje Ofisini kwetu tuzungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingine kwa kweli imekuwa mahususi ambayo inaweza kuchukuliwa na kuwekwa katika mikakati ya utekelezaji. Nawashukuru sana kwa michango yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda moja kwa moja kuwatambua wote wale waliochangia katika hotuba yangu leo kwanza kabisa wale waliochangia kwa kuzungumza Bungeni ambao ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, ambaye alimwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Aisha Phillipo Magina, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga,

Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuandika ni wengi kidogo lakini kwa sababu ya rekodi ya *Hansard* napenda uniruhusu na wenyewe niwataje ambao ni Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwanga, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya tena, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. *(Makofi)*

Aidha, nawatambua Waheshimiwa 42, orodha ni kubwa. Lakini kwa sababu hawakupata nafasi ya kuongea leo, lakini waliongea wakati ule. Napenda nao niwatambue na wenyewe ni Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Benito Malangalila na Mheshimiwa Emmanuel Kipole. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Karim Said Othman na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nimepata *note* nyingine kwamba Mheshimiwa Ireneus Ngwatura ni katika waliochangia kwa kuzungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwa kweli si rahisi kujibu yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza lakini najaribu kupitia kwa haraka katika maeneo machache na hasa kwa sababu maeneo mengine Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelezea kwa ufasaha, namshukuru sana. *(Makofi)*

Lakini kabla ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge napenda kutoa shukrani maalum kwa pole za msiba tulizozipokea. Mimi mwenyewe na kwa niaba ya mke wangu, Mheshimiwa Janet Kahama na familia yangu yote naomba kwanza kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa shukrani nyingi kwa kutoa pole kwetu na pia kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na hasa Waheshimiwa Wabunge Wanawake kufika Dar es Salaam kuja kutufariji.

Shukrani zetu nyingi zikufikie wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliotupa pole wakiwemo waliochangia leo katika Bunge kwa kusema au kwa maandishi na wale waliofika nyumbani na ambao tunao leo hapa katika Bunge, wakiwemo pia waliopiga simu na *Sympathy Cards* na bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia kwa hali na mali.

Tunazidi kuwaombeni Waheshimiwa Wabunge mumkumbuke mtoto wetu, Marehemu Clement Kiiza Kahama, katika sala zenu na vile vile kutuombea na sisi tuliobaki tupate subira.

Kwa kuwa ndugu na Waheshimiwa Wabunge waliotuhidi ni wengi, ni vigumu kuwataja mmoja mmoja, hivyo naomba radhi kwa kuwashukuru kwa ujumla wenu. Nami pia naomba pamoja na Mheshimiwa Janet Kahama, nataka kuchukua nafasi hii vile vile kutoa pole zetu kwa Waheshimiwa Wabunge wengine waliopatwa na msiba wakati huu tukiwa katika Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe maelezo machache kuhusu masuala yafuatayo:-

Kwanza, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Aisha Magina na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, pia suala hili limetolewa na Dr. Diodorus Kamala, kuhusu kesi za vyama vya ushirika na maelezo ya ziada. Katika hotuba yangu nimetoa maelezo kwa kifupi na vile vile *cabale* ya kuonyesha mahali tulipo. Lakini ningependa kwa manufaa ya Waheshimiwa Wabunge, kutoa maelezo ya ziada.

Pia nataka kutoa maelezo machache kuhusu hoja ya kuundwa na kuwepo kwa Wizara ya Ushirika na Masoko kwa sababu tu kwa faida ya Mheshimiwa Magina na Thomas Ngawaiya, ambao walikuwa na mawazo tofauti. Nadhani baada ya mimi kuongea mawazo yao yatakuwa sawa na ya kwangu.

Vile vile nina madai ya Vyama vya Ushirika kwa Bodi za Mazao kwa mfano *Nyanza Cooperative Union* inaidai Bodi ya Pamba na *KNCU* inaidai Bodi ya Kahawa. Halafu nitasema machache tu kuhusu soko la Tengeru ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Talala Mbise na vile vile makato katika bei za wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kesi za vyama vya ushirika Wizara yangu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tumetayarisha taarifa hii ambayo tutapenda kuisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge wanaohusika kwa ile Mikoa tuliyokuwa tumeitaja kusudi wawe na kumbukumbu ya kazi ambayo tumeifanya. Lakini kuhusu kesi ambazo zinahusu *specifically* Mkoa wa Kagera kuna machache ambayo tungetaka kuyasema, pamoja na taarifa niliyoitoe leo asubuhi lakini pengine watapenda kujua kwamba kuna kesi zinazowahusu viongozi wa juji juji ambazo hazijafutwa na bado zinaendelea na hizi zinahusu aliyekuwa Mwenyekiti, Ndugu Mashobe na aliyekuwa *General Manager*, Leopord Rweyemamu na wenzao wanne. Hii kesi bado inaendelea na tutaendelea kuifuatilia kwa karibu.

Vile vile kuna kesi ambayo inahusiana na *KDCU* ya Karagwe ambayo inahusu Simon Byamungu ambaye alikuwa ni Meneja wakati ule, Faridu Kashagama, Mkaguzi wa Ndani na Henry Lusemwa, alikuwa Mwenyekiti kabla ya sasa, kesi ambayo inaendelea katika Mahakama ya Wilaya ya Karagwe. Vile vile iko *criminal case* moja Na.174 ya mwaka 2000 ambayo inawahusu hawa wafuatao, ambayo inahusu *KDCU* ya Kagera ambayo ni Hawa Jovini, Difabusha Andrew Kakama, Doines Kashushura, Sosthenes Maganga, Aaron Kabunga na Chrisant Bagia.

Wahusika walifikishwa Mahakamani kwa mashtaka ya wizi wakiwa watumishi wa *KDCU* au viongozi wa *KDCU*. Kesi hii ilisikilizwa na mashahidi kadhaa walitoa ushahidi, cha kushangaza ni kwamba tarehe 20 Agosti, 2001 Hakimu wa Wilaya wakati ule akiitwa Jet Ishengoma, aliifukuza yaani *dismiss case* chini ya kifungu Na. 222 cha Sheria ya *Criminal Procedure up to 1985*. Sababu alizotoa Hakimu ni kwamba Jamhuri haikuwasilishwa siku hiyo, na pia eti kesi imechukua muda mrefu bila mashahidi kuletwa Mahakamani. Hizo ndizo sababu alizotoa.

Siku hiyo hiyo yaani tarehe 20 Agosti, Jamhuri ilitoa ilani ya kukata rufaa Mahakama Kuu, Mahakama baada ya muda iliwatumia Polisi nakala za *proceedings* na *judgement* kwa ajili ya kuandaa rufaa, cha kushangaza vile vile ni kwamba Polisi yaani *RCO*, alikaa na kumbukumbu hizi kwa muda mrefu bila kuchukua hatua yoyote mpaka muda wa kukata rufaa ukapita. (*Kicheko*)

Sasa kutokana na uzito na unyeti wa kesi hiyo, *DPP* amemwelekeza *Director of Criminal Investigation* ampelekee jalada la kesi hii ili kesi hiyo ifufuliwe aidha kwa njia ya rufani ya muda au kuiomba Mahakama ifanye mapitio yaani *revision* ya uamuzi wa Hakimu Ishengoma kwa kuitupilia mbali

kesi hii bila sababu ya msingi. Sasa ningependa kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaotoka sehemu za Kagera waweze kujua tuko sehemu gani. Lakini ningependa mfahamu kama hii ripoti ipo, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, alikuwa anahoji kwamba *Attorney General* kwamba uliosema kwamba ripoti ipo kweli? Sasa namhakikishia kwamba ripoti ipo ni hii. Kwa hiyo, tutawakabidhi wale wanahusika. (Makofi)

Mheshimiwa Aisha Magina, pamoja na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, walisema kwamba wangependelea ushirika urudi Kilimo. Nataka kuwapa maelezo ambayo yanaweza kuwasaidia kubadilisha mawazo yao. Chimbuko na sababu za kuunda Wizara maalum yenye dhamana ya ushirika ilikuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni uamuzi wa busara wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Benjamin Mkapa. (Makofi)

Halafu ushirika ni Sera ya CCM na ushirika upo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 1995 na mwaka 2000, kama Taasisi mojawapo ya kuunganisha nguvu za wanyonge ili kuwaondolea umaskini. Baada ya kudumaa katika maeneo mengi ya nchi, ushirika ilibidi upewe uhai mpya kwa kuundia Wizara ya pekee ya ushirika na masoko kama ilivyokuwa miaka ya nyuma hadi mwaka 1966, ushirika uliposhamiri na kuwa mfano wa kuigwa Barani Afrika. Nadhani tungekuwa tunasoma historia, machafuko yote haya yaliyotokea usiku zikaanza kupigwa mpira kupelekwa kama ni *Appendix* katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Rais wetu aliyaona yote hayo maana yake yeye anasoma sana. Akasema kwa hili lilikuwa kosa kwa hiyo lazima tulirekebishe na akalirekebisha. Taarifa ya mwaka 2001 ya Kamati Maalum ya Rais ya kumshauri juu ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika Tanzania, ilitoa pendekezo kwa Mheshimiwa Rais ambaye alilipokea, ambalo lilisema kama ifuatavyo:-

“Kamati inapendekeza iundwe Wizara Maalum yenye dhamana ya Ushirika itakayohusika na usimamizi na utekelezaji wa maendeleo ya Ushirika, kama ilivyopendekezwa pia na Tume zilizotangulia, Tume ya Nyirabu mwaka 1990 na Kamati ya Ngwilulupi ya 1981 kuundwa kwa Wizara yenye dhamana ya ushirika kutawezesha kuratibu na kuhamasisha maendeleo ya ushirika kwa karibu zaidi.”

Kwa mantiki hiyo Kamati inapendekeza Wizara hiyo iitwe, “Wizara ya Ushirika na Masoko.” Majukumu ya Wizara hiyo yahusishe pia mambo yafuatayo, kusimamia utekelezaji wa maagizo na programu zitokanazo na mapendekezo ya Kamati ya kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini na shughuli zote zinazotekelezwa na Idara za Ushirika na Taasisi zake hivi sasa. Kusimamia na kuratibu masuala ya ununuzi, usindikaji na uuzaji wa mazao yanayopitia vyama vya ushirika na vikundi vingine vya wananchi hata kama havijasajiliwa kama vyama vya ushirika. Kuvisaidia vyama vya ushirika katika jitihada zao za kujipatia fedha za kununulia mazao, uhamasishaji na uendelezaji wa shughuli za viwanda na biashara ndogo ndogo mijini na vijijini kwa njia ya ushirika.

Pia kuratibu juhudi za Wizara nyingine katika kuanzisha na kuendeleza ushirika katika sekta zote. Kutumia mbinu na ushiriki wa jamii, *Community Facilitation Skill*, kuchambua hali ya uchumi wa jamii vijijini na mitaani ili kupanga mipango ya jamii ya maendeleo na kubaini nafasi ya ushirika katika mchecheto huo.

Halafu akasema jambo la kwanza linahusu Wizara yenye dhamana ya ushirika. Ingawa hivi sasa Wizara ya Kilimo na Ushirika ndiyo yenye dhamana ya ushirika. Imedhihirika kuwa ndani ya Wizara ya Kilimo na Ushirika, suala la ushirika halijapewa kipaumbele. Idara ya Ushirika katika Wizara hiyo imekuwa kama mtoto yatima. Matokeo ya hali hii ni kushindwa kutoa uzito unaostahili kuyakubali matatizo yanayohusiana na maendeleo ya ushirika kama yalivyoainishwa hapo juu. (Makofi)

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kama unataka kurudi huko nyuma, ni hiari yako. Nitajaribu kumshawishi Mheshimiwa Waziri Kivuli aweze kwenda mbele siyo nyuma. Pili, ni deni la wakulima wa *KDCU, KNCU* na *NCU*. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, tumezungumza kwa muda mrefu. Uchunguzi umefanywa na tumebaini kwamba *KNCU* inaidai *Tanzania Coffee Board* shilingi milioni 548. Lakini *Tanzania Coffee Board* inakataa kwamba haidaiwi na inasema kwamba fedha hizo zilitokana na utaratibu

wa Serikali uliokuwa wakati ule, ulikuwa unaitwa *full system*, walitoa dawa, walitoa vingine na vingine kwa hiyo wamekataa. Sasa kama kuna vyombo viwili vinakataa, mnajua la kufanya kwa kawaida mnakwenda kortini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi hatutaki kutumia utaratibu huu kwa sababu vyombo vyote ni vyetu. Kwa hiyo, tumetumia utaratibu wa kuchagua *Independence Frame of Consultance*, siyo COASCO, siyo chombo cha Serikali ambao watakwenda watuambie ukweli uko wapi, tukisha ujua kama itaonekana kwamba KNCU kwa kweli wanadai, tutahakikisha kwamba fedha hizo zinapatikana na KNCU wanalipa. Nitalifanya hili jambo kwa haraka sana kwa sababu sasa tunazo fedha za kuweza kufanya kazi hiyo. (Makofi)

Jambo lingine nadhani kuna Waheshimiwa Wabunge, Profesa Daimon Mwaga, alikuwa ana wasi wasi kwamba Chuo cha ushirika, kikiwa *University* kutatokea matatizo na wasi wasi huo ameusemea vile vile Mheshimiwa Aisha Magina. Nataka kuwahakikisha kwamba mabadiliko ya hadhi ya Chuo cha Ushirika kuwa Chuo Kikuu yanapanua tu taaluma, haitoi majukumu mapya, chuo kitaendelea na majukumu yake yote ya awali na mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi yafuatayo yamefanywa na Serikali ambayo ni kuimarisha Matawi yote ya Elimu ya Ushirika 18 pamoja na Kizumbi, Shinyanga alioisemea Mheshimiwa Mbunge. Hii itafanya Elimu ya Ushirika kuwafikia wakulima na wanachama milioni 10 nchi nzima. Mfumo wa Elimu ya Ushirika umebadilika ili wanachama wawe jasiri katika kuleta Utawala Bora na ujasiri yaani *entrepreneurship*. Taaluma za chuo ni zile zitakazokidhi mahitaji ya ubunifu wa kufanya biashara ya ushirika Kimataifa. Chuo kina majengo na walimu wa kutosha kuanza kuendesha taaluma zote za ushirika. Kwa hiyo, kuwa Chuo Kikuu hakutaondoa zile kazi zake walizokuwa wakifanya hapo zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningetaka kulielezea kwa kifupi, nadhani linahusiana na hoja ya Mheshimiwa Talala Mbise, kuhusu soko la Tengeru. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Talala Mbise, kwamba soko hilo tuko katika programu katika kile tulichokiita *project* yetu ya *Market Development Program* ambayo iko chini ya *Prime Minister*. Naona kabla haujaondoka uje Ofisini tuweze kuongea ili tuweze kui-*program* vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu jambo lingine ni kwamba kuna makato mengi kwa bei inayotolewa kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani katika hotuba yangu nimesema kwamba Wizara imefanya utafiti ili kubaini gharama za mauzo yaani *Marketing Costs*. Tumekwishatayarisha gharama za kuhusu zao la pamba, kahawa, korosho na tunaendelea na mazao mengine. Nia yetu ni kwamba tukishazipata hizo, tuweze kuwashauri wanunuzi binafsi, Vyama vya Ushirika na Bodi za Mazao ni wapi zipunguze yale makato ambayo yanakatwa kwa bei ya mkulima kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa kabla hatujafika kwenye hatua inayofuatia, nimepata vi-*note* vingi sana hapa ambavyo kimojawapo kinasema, Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba wakati tutakapofika kwenye Kamati, tupitishie Fungu zima. Hii ni kwa sababu mwenzetu amekuwa na msiba hata nguvu za kusimama hapa tunazishangaa. (Makofi)

Sasa mimi nafuata ushauri wenu, lakini la msingi wote mnajua ile Kanuni ya 81(2)(a)(b) ambayo inaeleza utaratibu wa kupitia katika hivi vifungu. Kwa hiyo, tutahoji kama mlivyotaka kwa ujumla wake lakini bado haimzuui Mbunge yeyote popote alipo kusimama na kuhoji kifungu chochote anachohitaji. Hili naona liwe wazi ili shughuli zetu ziwe na uhalali, lakini pia tuwe na ule moyo wa nia ya kumwonea mwenzetu imani, uwe pale pale. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko... .. Shs. 5,085,486,900/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 24 - Wizara ya Ushirika na Masoko... Shs. 395,747,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirika na Masoko ya Mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko, hivyo naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ushirika na Masoko kwa Mwaka 2003/2004  
yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.08 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 1 Agosti, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*